

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**Kikao cha Pili - Tarehe 30 Oktoba, 2013**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

Naibu Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:**

Maoni ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti juu ya Mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015.

**MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA FEDHA NA UCHUMI):**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Fedha na Uchumi juu ya Mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu na atakayeuliza swali letu la kwanza ni Mheshimiwa Ismail Aden Rage.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana awali ya yote ninakupa pole ya msiba uliopata na ninaomba swali sasa lijibiwe.

Na.15

### Kusimama kwa Ujenzi wa Hospitali ya Kitete

**MHE. ISMAIL A. RAGE** aliuliza:-

Hospitali ya Kitete ilikuwa kwenye ukarabati lakini Mkandarasi amesimama muda mrefu:-

Je, Serikali ni nini hatma ya kukamilisha majengo hayo?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

### NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA(ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa miundombinu katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora Kitete unafanyika kwa hisani ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), utekelezaji wa mradi huu katika awamu ya kwanza ulianza tarehe 1/8/2009 na ultakiwa kukamilika tarehe 27/4/2011.

Katika kutekeleza awamu hii, Wizara ya Afya ya ustawii wa jamii ilifanya mchakato wa kupata mkandarasi wa kutekeleza mradi huu ambapo kampuni ya *Humphrey Construction Ltd.* ilishinda zabuni.

Mheshimiwa Spika, sababu za kusimama kwa mradi huu ni Mkandarasi kushindwa kutimiza masharti ya mkataba wake kama ilivyokusudiwa. Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Tabora alikagua mradi huo mwezi Julai, 2012 na kuagiza Mkandarasi awe amekamilisha kazi hiyo ifikapo Agosti, 2012. Hata hivyo, Mkandarasi alishindwa kukamilisha kazi hiyo. Hatua ambayo Serikali ilikusudia kuchukua ni kusitisha mkataba wake na kutafuta Mkandarasi mwingine.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutangaza upya kazi hiyo, Serikali iliendelea na zoezi la kufanya tathimini ya kazi zillizobaki ili kujuza gharama halisi za kukamilisha mradi huo ambao kwa sasa umesimama. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2014.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, nina masikitiko makubwa sana kwa sababu majibu niliyoyapata hayakunifurahisha wala hayakuniridhisha, mimi binafsi nimefika mpaka Wizarani nikaonana na Idara inayohusika na masuala ya ukarabati jambo la kushangaza Hospitali hii ya Tabora ndiyo Hospitali ya Rufaa na ndiyo Hospitali ya Manispaa inayotegemewa, matokeo yake imeshindwa kutoa huduma kwa wananchi na wananchi wamekosa imani na watendaji wa Hospitali hiyo.

Je, haioni kuwa sasa ni wakati muafaka Waziri atamke katika Bunge hili rasmi Mkandarasi mpya ambaye ninaambiwa amekwishapatikana ataanza kazi lini na itakwisha lini?

Mheshimiwa Spika, hela zipo ni za *Africa Development Bank* na Serikali inachangia na kwenye Bajeti iliyopita tulitenga pesa kwa ajili hiyo, ni maswali hayo tu Mheshimiwa Spika.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rage kama ifuatavyo:-

Kilichochelewesha kupatikana kwa Mkandarasi mpya ili aanze kazi mara moja ni utaratibu wa Kisheria wa kuvunja Mkataba wa Mkandarasi wa kwanza. Lakini ninapenda kutoa taarifa kwamba hatua hiyo imeshakamilika yule Mkandarasi wa kwanza Mkataba wake umeshavunjwa. Mkandarasi wa pili ameshapatikana kwa sababu wamechukua walewale ambao wamefanya kazi katika sehemu nyingine na wakafanya kwa ufanisi.

Kwa hiyo, walifanya *selective tendering* na imeshakamilika muda wowote kuanzia sasa atakwenda katika eneo ili akakamilishe hatua iliyobaki. Ninaomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira na tutampa tarehe kwa ufasaha baada ya kutoka hapa.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali dogo la nyongeza. Suala alilozungumzia Mheshimiwa Rage linafanana sana na tatizo la Hospitali ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi ambayo kwa muda mrefu imefanyiwa ukarabati lakini kubwa zaidi ni ujenzi wa *theater* kwa ajili ya akina mama ambayo imechukua muda mrefu sana, hivyo kusababisha akina mama wengi kupoteza maisha wakati wanapopelekwa *KCMC* au hospitali nyingine. Nilitaka maelezo au kauli ya Serikali ni lini *theater* hiyo itamalizwa ili akina mama wasipate matatizo kama ambavyo yanapatikana sasa hivi, hususani ya vifo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri maelezo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mara nyingi tumekuwa tukizungumza katika Bunge hili suala la ujenzi wa Hospitali ya Mawenzi na hasa ukamilishaji wa *theater* na majengo mengine. Jambo hili bado lipo linashughulikiwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro na kwa maana hiyo tunayo nafasi ya kupata maelezo kutoka kwa Katibu Tawala wa Mkoa.

Ninamhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa baada ya *session* hii ya maswali tutafanya mawasiliano na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro ili nijue *position* ya ujenzi inayoendelea kwa sasa ili tupate majibu sahihi.

Mheshimiwa Spika, tutafanya msukumo mkubwa kwa hatua iliyobaki ili jambo hili liweze kukamilika mara moja.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kabati sasa na wewe utauliza kuhusu Hospitali ya Iringa halafu mnasema yanafanana, haya Mheshimiwa Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Hospitali ya Wilaya iliyopo katika Manispaa ya Iringa ilianzishwa ili kupunguza msongamano uliopo katika Hospitali Kuu na kwa kuwa sasa hivi kuna ujenzi ambao unaendelea wa mawodi ya kulaza wazazi.

Ni lini Serikali itatuletea pesa ili kukamilisha ujenzi huo kwa sababu kuna nguvu ya wananchi na ya Manispaa ambayo imeshatumika kwa muda mrefu? Ili msongamano huo uishe unategemeana na kukamilishwa kwa hayo mawodi.

**SPIKA:** Maswali ya namna hiyo mkipata majibu hayaridhishi mkubali, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu hayafanani na lile la kwanza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Sera ya Serikali ya ukamilishaji wa Zahanati katika kila Kijiji na vituo vya afya katika kila Kata na Hospitali za Wilaya katika ngazi za Wilaya bado unaendelea na uimarishaji unaendelea, kupitia Bajeti yetu ya mwaka huu tumetenga fedha kupitia mipango miwili. Kuna *basket fund* kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu na vifaa tiba.

Lakini pia tuna *MAMambayo* inashughulikia ukarabati ambao kwa sasa tumeshafanya mgao na kwa kuwa swali limekuja sasa nitafanya mapitio ya kuona ni kiasi gani cha fedha tulitenga kwa ajili ya Mkoa wa Iringa na Hospitali ya Wilaya ili tuweze kukamilisha kazi hiyo.

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea na Mheshimiwa Paul Lwanji kwa swali linalofuata.

Na. 16

### **Ahadi ya Kuupatia Mji wa Itigi Maji ya Kutosha**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kuupatia Mji wa Itigi maji ya kutosha.

Je, Serikali imefikia wapi katika kutekeleza ahadi hiyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mnamo mwezi Novemba, 2012 Mheshimiwa Rais akiwa katika ziara katika Mji wa Itigi alitoa maagizo kwa uongozi wa Mkoa na Wilaya kushughulikia Mji wa Itigi. Mahitaji ya maji kwa wakazi wa Mji huo ni lita 1,300,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwapatia maji wananchi wa Mji wa Itigi, Halmashauri katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 kupitia programu ya Tekeleza kwa matokeo Makubwa Sasa (*BRN*), ilidhinishwa shilingi 258,000,000 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa visima viwili ambavyo ni SG 37/73 na SG 15/73. Ukarabati huu utaongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa asilimia 25 ya mahitaji.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji (*WSDP*) kwa mwaka 2014/2015 Mji wa Itigi utapewa kipaumbele katika mradi itakayotekelawa kupitia utaratibu wa maji mjini. Katika awamu hii kazi itakuwa ni kufanya usanifu upya ili kupata vyanzo vya maji vya uhakika vitakavyokidhi mahitaji ya maji kwa wakazi wa eneo hilo la Itigi.

**MHE.JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Mkutano wa Bunge uliopita Naibu Waziri wa Maji alipata nafasi ya kutembelea Mji wa Itigi na akajionea tatizo kubwa la maji ukilinganisha na idadi ya wakazi wa Mji huo. Mimi ningependa kujua katika Bajeti ya 2013/2014 kila Mbunge aligombea sana na tukaongeza Bajeti Wizara hii ya Maji zilliongezwa shilingi bilioni 184.5.

Tunachohitaji katika Mji wa Itigi ni shilingi milioni 200 ningependa kujua katika nyongeza hiyo sisi katika Jimbo la Manyoni Magharibi tumepata kiasi gani na kwa nini Serikali isingekuja na takwimu kuonyesha katika hizo fedha zilizoongezwa kila Jimbo limepata Fedha kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Paul Lwanji, kama ifuatavyo. Lakini kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Lwanji kwa namna ya pekee anavyofuatilia miradi ya maji katika Jimbo lake.

Ni kweli kuwa nilifanya ziara na nikatembelea Mji Mdogo wa Kintingu na kweli kuwa kuna tatizo kubwa la maji tulifanya maagizo pale kuwa pale kuna visima viwili ambavyo vilikuwa vinatumiwa na Wachina waliokuwa wakijenga barabara kisima kimoja kina mita za ujazo 6000 na kingine kina mita za ujazo 10,000. Kwa hiyo, tuliagiza Halmashauri iombe kibali ipate vile visima ili viweze kusaidia maji pale Mjini. Nimefuatilia na nina taarifa kuwa Wachina wameruhusu kile kisima cha lita 10,000 kitumike kwa ajili ya kutoa maji pale Mjini Itigi.

Kwenye miradi ya matokeo ya haraka sasa tumewatengea millioni 258 kama anavyosema Mheshimiwa Waziri na hizo fedha ni kwa ajili ya Itigi tu, ili waweze kupata maji na hizi fedha zitaelekezwa kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye kukarabati visima vilivyopo. Lakini milioni 250 zinakwenda kwa ajili ya hiki kisima ambacho kitatoa maji ya kutosha.

Kwa hiyo, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Lwanji kuwa Serikali imejali tatizo la wananchi pale Itigi na imetenga shilingi milioni 258 lakini vilevile ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa tutaleta orodha ya mgao za zile fedha jinsi kila Mkoa walivyopa na kila Wilaya ilivyopata kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kibona nilikuona umesimama, sikukuona Kibona? Mheshimiwa Kibona nimekuita.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi kwasababu swali langu lilikuwa ni kutaka kujua ni kiasi gani Wilaya ya lleje na hasa Mji wa Isongole tumepata na majibu haya tayari yameshatolewa ninaomba sasa nieleweke kuwa nimesharidhika ahsante sana.

**SPIKA:** Kwamba atatoa orodha ya mgao kwa Mkoa na Wilaya zote, Mheshimiwa Natze.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi hii niulize swali moja. Tarehe 18 Machi, 2013 Mheshimiwa Waziri wa Maji alifika Karatu katika kusaidia Mji wa Karatu kupata maji na akaagiza baada ya siku kumi visima viwili vitakuwa vimechimbwa na watu wataanza kutumia maji. Cha kushangaza katika Matokeo Makubwa Sasa jumla ya shilingi milioni (475,000,000/=) zimekwisha kutumika hakuna maji, amekuja Waziri Mkuu kuzindua ule mradi hakuna maji ameondoka.

Je, Serikali inatoa kauli gani sasa ili kuhakikisha wananchi wa Mji wa Karatu wanapata maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kutoa majibu kwa Mheshimiwa Mbunge Natze, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Kwanza nimwombe Mheshimiwa Mbunge akubali kazi ambayo inafanyika pale sasa hivi kwa sababu katika hizo shilingi milioni 475,000,000/= alizozitamka tayari kuna kazi imefanyika, tumekwisha kujenga tenki pale Galkum huo ni Mji wake anaufahamu na Mheshimiwa Waziri Mkuu ameenda akaweka jiwe la msingi pale tumekwishaanza kuchimba visima viwili na *DBCA* wako kule mpaka kule Karatu na ye ye alikuwa ni shahidi wakati Waziri Mkuu akishuhudia ile kazi ikifanyika.

Tumekwisha laza mabomba kutoka kwenye tenki mpaka kwenye kisima ambacho kitatoa hayo maji na shughuli za umeme zimekwishafanyika kilichobki ni kujenga vituo na alivyofika Mheshimiwa Waziri Mkuu ilionekana kuna upungufu wa fedha na sasa hivi ninavyoongea tayari Wizara yangu imeshapeleka shilingi milioni 150 ili Mamlaka ya Maji ya *AUSA* iweze kumalizia kazi zilizobaki na wananchi wa Karatu wapate maji.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Moza, swali kwa ufupi.

**MHE. MOZA ABEIDI SAIDY:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Ninapenda kuuliza swali langu Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika katika Wilaya ya Kondoa na kutoa ahadi kuhusu maji na kuchangia katika mradi wa Ntomoko, ninapenda kujua Serikali ina mpango gani katika Wilaya ya Kondoa kuweka miundombinu ya kisasa ya maji kuondokana na miundombinu chakavu iliyokuwepo kwani sasa hivi na mpaka Wilaya ya Kondoa ina hali ngumu ya maji hasa Kondoa Mjini?

**SPIKA:** Maswali yote haya ni mapya lakini bahati nzuri ufundi wa Waziri ndiyo unamruhusu ajibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuna tatzivo kubwa la maji pale mjini kondoa na kwenye vijiji na hasa ule mradi wa Ntomoko. Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi na hivi ninavyoongea Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekwishatoa bilioni moja. Bunge lililopita liikuja kufahamu kwamba Halmashauri ilikuwa haijaanza kuzitumia zile fedha. Kwa hiyo, hivi ninavyoongea nimemwagiza Mkurugenzi na Mhandisi, nakaa nao kesho kujua wamefikia wapi katika utekelezaji wa mradi huo. Lakini kuhusu maji mjini hatua zitaendelea kuchukuliwa, hela zikipatikana tutawatengea, ili waweze kuboresha miundombinu kwa ajili ya maji pale mjini Kondoa.

**SPIKA:** Upande wa majibu tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu. Kwa niaba yake atauliza nani Mheshimiwa Rage unaweza kuuliza kwa niaba.

**MHE. ISMAIL ADEN RAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba swali la Mheshimiwa Mbunge Ijibiwe kama liliivoandikwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri swali ni Namba 17. Namsamehe kwa sababu nimemwita mwenyewe akasimama.

Na.17

**Mji wa Igunga kuwa Mamlaka ya Mji mdogo**

**MHE. DKT. DALALY PETER KAFUMU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa kuufanya Mji wa Igunga kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu.**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kwamba Mji wa Igunga ni mionganoni mwa Miji inayokuwa kwa kasi hapa nchini kutokana na ongezeko kubwa la Idadi ya watu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sheria zilizopo, utaratibu wa kuanzisha Mamlaka za Mji Midogo unaanza kwa wananchi wenyewe na kuperishwa katika vikao vyta kisheria ambavyo ni Kamati ya Maendeleo ya Kata, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya (*DCC*) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia utaratibu huo, Halmashauri ya Wilaya ya Igunga imeshaanza kufanya mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Igunga ambapo pendekezo hili liliwasilishwa na kujadiliwa katika kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata tarehe 10 Agosti, 2011, Kamati ya Huduma za Uchumi tarehe 21 Oktoba, 2013, Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 22 Oktoba, 2013 na Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo tarehe 23 Oktoba, 2013.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Hata hivyo, pendekezo hili lilipaswa kuwasilishwa Katika vikao vya Kamati za Ushari za Wilaya na Mkoa na hatimaye kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kwa ajili ya kupata ridhaa yake.

Mheshimiwa Spika, hatua zote hizo zikikamilika na kuonekana Mji wa Igunga unakidhi vigezo kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo. Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI itatuma wataalam kwa ajili ya kufanya uhakiki wa vigezo vinavyozingatiwa ili hatimaye Mamlaka hiyo iweze kuanzishwa sambamba na Mamlaka nyingine ambazo maombi yatakuwa yamepokelewa.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Marombwa swali la nyongeza.

**MHE.ABDUL JABIRI MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mchakato wa kuufanya Mji wa Kibiti kuwa mamlaka ya mji mdogo ulishakamilika katika ngazi ya Kata, Wilaya na Mkoa. Tangu tupeleke maombi hayo, Ofisi ya Waziri Mkuu imechukua muda mrefu kuweza kutoa majibu yake. Sasa swali dogo.

Je, ni lini serikali itatangaza Mji wa Kibiti kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Marombwa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, tunayo maombi ambayo tayari yamekamilisha taratibu kwenye Miji kadhaa ilikiwemo Madaba Mafinga, Nzega na hata kule Handeni. Taratibu zinaendelea na pamoja na yale maeneo ambayo yanaendelesha mchakato huu, ikiwemo na ile Igunga kama ambavyo nimesema kwenye jibu la

msingi. Utaratibu huu ukikamilika na kwa sababu ikishakabidhiwa kwa Waziri mwenye dhamana. Mpango wa Waziri wa eneo hili ni kwamba Miji hii yote itapata kibali chake kabla mwaka 2015 kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, tumekuwa tunahoji kuhusu hii michakato. Kwa mfano Mji wa Kibondo mchakato ulianza mwaka 2004 sasa hii michakato inachukua muda gani?

Kama hii Serikali ipo *serious*, kwa nini msifanye hili jambo kwa miezi mitatu?

Kwa Miji watu ambao wamefanya maombi. Ili tuje mnafanya mambo kwa muda mfupi na *serious* kwa sababu ni mambo ambayo hayahitaji muda wa kupoteza.

**SPIKA:** Matokeo ya haraka, matokeo makubwa ya haraka. Mheshimiwa Mkosamali. (*kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkosamali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nikuhakikishie kwamba Serikali ipo *serious* na ipo makini katika kufanya kazi yake, ili kupata matokeo yaliyo sahihi. Unapoendesha mchakato wa namna ya kufanya Miji midogo kuweza kuipitia Miji midogo Mamlaka zake ni lazima hatua kadhaa ziptitiwe. Ikiwemo na vile vigezo ambavyo vinavyotakiwa.

Lakini pia baada ya taratibu zote kukamilika na hatimaye kukamilika kwenye Kamati ya ushauri wa Mkoa sasa mnapopeleka maombi yale Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Waziri mwenye dhamana lazima atume timu ili ikajiridhishe kama vigezo viliviyotakiwa vimekamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na swala la Bajeti, pia linakuwa lipo mionganoni, huwezi kuanzisha Miji tu halafu baadaye uje kutuletea ugumu. Kwa hiyo baada ya kukamilika na Bajeti kuwepo. Tumesema Miji hii mingine yote ikiwemo na Miji Kasulu ambao sikuutaja awali ya Kibondo ndio ile Miji sasa itapewa kibali chake kwa pamoja tukiwa tumeshaandaa na Bajeti zake ili waanze taratibu kwa pamoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresto.

**MHE. CECILIA DANIEL PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri za Wilaya zilizopo Nchini sasa hivi, bado hazijaimarika kimapato na Rasilimali Watu na kwa kuwa kumekuwa na maombi mengi ya kuanzisha Mamlaka ya Miji Midogo katika Halmashauri hizo hizo ambazo bado hazina ukomavu wa kutosha kujindesha.

Je, serikali haioni umuhimu wa kusitisha kwanza uanzishaji wa Mamlaka ya Miji Midogo na kuziimarisha Halmashauri zilizopo kwanza?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mchakato huu tunakuwa makini katika kuupatia vibali vya Miji midogo ambayo inaombwa likiwemo na hili ambalo umelisema linalokwenda sambamba na swala la Mheshimiwa Mkosamali.

Mheshimiwa Spika, huo makini ndio tunaufanya na ndio maana tumekubaliana kwamba Miji yote hii iliyoomba baada ya kufanya tathmini na kufanya mapitio ya Bajeti, ndipo ambapo tutaweza kutoa kibali chake mwaka 2015. Moja ya vigezo ni uwezo wa Miji yenewe kwanza kujipatia mapato yake wenyewe hiyo ndiyo itakayopelekea hata Miji midogo kupewa mamlaka ile.

Mheshimiwa Spika, Bila kuwa na uwezo wake wenyewe inaweza kuwa mzigo mkubwa kwa Serikali na kwa kuwa Bajeti zetu zinaandaa kwa ajili ya kutoa huduma zingine za jamii kwenye maeneo ambayo yalikuwa tayari na yale machache ambayo tutayatolea kibali. Pamoja na hayo Miji mingine huwa haipati kibali kwa haraka kama inavyotakiwa na wengine kwa sababu ya uwezo wa Halmashauri zenyewe.

**SPIKA:** Ahsante tutanaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Mheshimiwa Mohamed Minyaa, atauliza swali hilo.

Na.18

**Mikakati ya Hifadhi ya Mazingira Pwani ya Bahari  
ya Tanzania, Mito na Maziwa**

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA** aliuliza:-

Serikali ilipojibu Swali Na. 280 katika Mkutano wa Nane (8) Kikao cha Thelathini na Sita (36) ilisema kuwa, kwa kuzingatia umuhimu wa Ukanda wa Pwani, Bahari na Maziwa wa mwaka 2008. Serikali iliweka mkakati wa hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ambao haukizingatia eneo kubwa la uchafuzi huo unaofanyika sasa hivi katika Bahari kuu ya Tanzania unaosababisha na utafutaji wa Mafuta na Gesi baharini:-

Je, wataalam wetu wa *EIA* wanasesmaje juu ya hali hiyo na ni juhudhi gani zinachukuliwa kukabiliana na hali hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Raisi Mazingira naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa hatua za haraka za kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mabwawa na Mito umezingatia uchafuzi wa mazingira utokanao na shughuli za utafiti wa Mafuta na Gesi katika Bahari Kuu. Mkakati umeainisha hatua mbali mbali za kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa maeneo ya ukanda wa pwani na Bahari ikiwa ni pamoja na uchafuzi wa bahari utokanao na shughuli za utafutaji Mafuta na Gesi.

Mheshimiwa Spika, kulingana na sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 na matakwa ya kanuni za Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Ukaguzi mwaka 2005, shughuli za utafutaji na uzalishaji wa Mafuta na Gesi ni lazima zifanyiwe tathmini ya athari kwa mazingira (*TAM*). Kwa muktadha huo, miradi yote ya utafutaji wa Gesi inayofanyiwa Nchini imefanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira.

Aidha katika kipindi cha utekelezaji wa miradi hii ufuatiliaji (*monitoring*) unafanywa na Mamlaka husika ili kuhakikisha kuwa waendeshaji wa miradi hiyo wanazingatia masharti ya kuzuia uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahakikisha kuwa, utafutaji wa mafuta na gesi hufanywa kwa kufuata mipango maalum ambayo haiathiri mazingira ya baharini na viumbi hai. Mipango hii ni pamoja na utumiaji wa teknolojia

zinazozingatia hifadhi ya mazingira. Aidha tahadhari zote huchukuliwa wakati wa shughuli za utafutaji mafuta na gesi kuepuka athari kwa mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwafahamisha, Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuwa wataalamu wetu wa *TAM* wanafuatilia kwa karibu shughuli zote za utafiti wa mafuta na gesi katika kuhakikisha kuwa mazingira ya bahari hayaharibiki. (*Makofii*)

**SPIKA:** *Engineer Mohamed Haib Juma Mnyaa.*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nasikitika kwamba Serikali haikujibu swala hili ipasavyo na ni maneno mengi ya kuzungusha zungusha. Sasa niombe nmwulize maswali mawili *specific* labda atalifahamu na tutapata majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uchafizi wa mazingira baharini yaweza kufanywa na utafutaji wa shauri za mafuta na gesi. Ni tofauti sana na uchafizi wa mazingira unaofanywa nchi kavu, unakofanywa na utafutaji wa madini ambapo huku nchi kavu, uchafizi wa mazingira unajulikana na watu wa *environmental impact assessment* wana taratibu zao kwamba yule ambaye anatafuta madini baada ya kuchafua mazingira afanye vipi ikiwemo, pamoja na kupanda miti na kufukia mashimo. Kuleta hali sura ya kawaida. Sasa swalii langu hapa nimelenga kwamba huu uchafizi wa mazingira baharini unapofanywa na mameli makubwa wanaochoronga ile miamba na kuzusha vumbi kubwa ndani ya bahari.

Je, uchafizi huu wa mazingira *remedy* zake baada ya utafiti zake wana *cover* vipi inarekebishwa vipi, upande wa baharini? Hilo swalii la kwanza.

Mheshimiwa Spika, labda itafahamika vizuri lakini na pili kile kitendo cha kuchoronga miamba na ikazusha vumbi ndani ya bahari. Zile viumbe hai wakiwemo samaki

wanakimbia. Sasa hivi upatikanaji wa samaki umekuwa ni mgumu sana kwa sababu hao samaki wanakimbia kwa athari za hizi meli na mambo wanayofanya huko baharini.

Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuwahuisha hawa wavuvi wetu ili wapate kipato wakati hawa samaki wanakimbia katika shughuli za utafiti? Mfano Serikali ingeweza kuweka? Je, Serikali inasema nini kuhusu hilo?

**SPIKA:** Umeamua kutuhutubia haya, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Ofisi Ya Rais, Mazingira, napenda kujibu maswali mawili kwa pamoja ya Mheshimiwa Mnyaa kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi. *Environmental Impact Assessment* inapofanyika inatoa conditions ambazo zinakuwa zinalenga kuhakikisha kwamba uharibifu wa mazingira haufanyiki. Ikiwa ni pamoja na kutumia teknologia iliyo bora.

Kwa mfano wanapoanza kufanya utafiti wanatumia teknolojia ya sesmolojia. Teknolojia hii inatumia sauti na mwangwi, kwa hivyo ule mtetemo ule unaotokea ndio wanatambua kwamba eneo hili linaweza kuwa na gesi au mafuta.

Mheshimiwa Spika, wanapokwenda kuchimba wanatumia tenolojia ambayo ni *mag drilling* ambapo wanatumia tope kupaka kwenye kingo la mashimo ili vumbi isitokee na kusitokee mmomonyoko. Lakini Vile vile wanatumia teknolojia ya kuweka sementi ili pakaitokea mlipuko pasiwe na athari kubwa. Hili swala la viumbi vyote vimelindwa kutumia teknolojia ambayo ni nzuri, kuhakikisha kwamba hawa watafutaji wanatekeleza hilo, ila watu wa baraza la mazingira wanakuwa wanafutatilia. Kuna meli maalum kubwa zinazokusanya ule uchafu wa maji maji. Kwa

mfano kwenye kuchimba kunakuwa na greese na vyote vinachukuliwa na meli kubwa zinazoleta nchi kavu kuweza kutupa hizi taka taka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Betty bMachangu.

**MHE. BETTY ELIEZER MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali kwa Waziri wa Mazingira Mheshimiwa Spika kuna uchafuzi wa hali ya juu unafanyika Bahari ya Hindi mkabala kidogo na nyumba ya Waziri Mkuu. Nakumbuka nyuma kidogo kamisheni ya Keenja ilikuwa imetenga eneo hilo serikali ilichukua vile viwanja. Mheshimiwa spika kuna majiko, kuna biashara mbali mbali kila siku kuanzia asubuhi.

Je, serikali imeliona hili?

**SPIKA:** Mbona mnauliza maswali yasiyofanana ilikuwa uchafuzi kwa ajiil ya gesi, sasa huyu atakujibu nini kule hakwenda?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Ofisi ya Rais, Mazingira, napenda kujibu maswali mawili kwa pamoja ya Mheshimiwa Betty Machangu, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kando kando mwa bahari karibu na ilipo nyumba ya Waziri Mkuu kuna shughuli za biashara ambazo zinaendelea. Lakini hilo sisi tumeliona kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI. Tunazungumza na wenzetu wa Halmashauri ya Kinondoni ili tuone utaratibu mzuri zaidi au kuondoa shughuli za kibashara eneo hilo. Aidha kuboresha zaidi ili kuhakikisha hakuna uchafuzi wa Mazingira.

Lakini utakapopita asubuhi pale utakuta sehemu lle imesafishwa kabisa kwa hivi sasa. Lakini bado tutaendelea kujadiliana na wenzetu wa TAMISEMI tuone kwa namna gani tunaweza kuboresha sehemu ile. (*Makofii*)

**Mafuta na Gesi Nchini Kuwa Katika Mambo ya Muungano.**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Katiba ya Tanzania ukurasa 18, suala la Mafuta na Gesi ni mionganini mwa Mambo ya Muungano na Tanzania Bara kwa muda mrefu imeanza kuvuna Gesi asilia bila Zanzibar kunufaika nayo:-

(a) Kwa kuwa suala hili bado limo kwenye orodha ya mambo ya Muungano. Je, Zanzibar ilistahili kunufaika na kiasi gani hadi sasa tangu Gesi hiyo ianze kuvunwa?

(b) Kwa kuwa Zanzibar imeamua suala la Mafuta na Gesi asilia liondolewe katika Mambo ya Muungano:-

Je, ni lini marekebisho ya Katiba yataletwa Bungeni badala ya kusubiri mchakato wa Katiba Mpya?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Spika, mapato yote yatokanayo na gesi asilia pamoja na vyanzo vingine vya mapato huingizwa katika Mfuko Mkuu wa Mapato wa Serikali-Hazina na Zanzibar inapata mgao wake kutoka mfuko huo. Aidha, sehemu kubwa ya gesi asilia ambayo huzalishwa kutoka Songo Songo hutumika kufua umeme unaoingizwa katika gridi ya Taifa. Zanzibar hunufaika na umeme unaosafirishwa kuititia *submarine cable* iendayo Zanzibar.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Kamati ya kushughulikia kero za Muungano chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeundwa Kamati Maalumu inayoongozwa na wanasheria wakuu

kutoka pande zote mbili za Muungano kushauri namna gani pande mbili za Muungano zitakavyoweza kuendesha shughuli za utafutaji na uzalishaji mafuta na gesi asilia kwa kujitegemea.

Moja ya maeneo ambayo yanaangaliwa na kamati hiyo ni pamoja na kurekebisha Sheria ya Mafuta ya mwaka 1980, ili kuiwezesha Zanzibar kuendesha shughuli za utafutaji na uzalishaji mafuta yenye.

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Mbunge avute subira mpaka taarifa ya kamati maalum itakapokamiliika kwani Mwenyekiti wa kamati amekwishawasilisha taarifa hii kwa mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri kutokidhi swali la msingi naomba nimwuulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Waziri unaposema Zanzibar imenufaika ikiwemo upatikanaji wa huduma za umeme. Je, Zanzibar umeme ule wanununua au wanagawiwa bure?

(b) Kamati ya Wanasheria katika hadidu rejea zao watatumia muda gani kumaliza tatizo hili la muda mrefu au imekuwa sawa na Mkulima anayelalamika njaa wakati chakula kahifadhi juu ya dari?

**SPIKA:** Hukusikia swali la pili, Mheshimiwa Jaku swali la pili Naibu Waziri hakusikia.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, Kamati ya Wanasheria katika hadidu rejea zao imekuwa ni ya muda mrefu, ni lini watamaliza tatizo hili au itakuwa ni hadithi ya mkulima anayelalamika njaa wakati chakula kahifadhi juu ya dari?

**SPIKA:** Haya Naibu Waziri ujibu, mimi pia sikusikia sehemu ya pili.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, hakuna mtu ye yote katika nchi hii ambaye anatumia umeme bure, hayupo.

Kwa hiyo, watu wote wanatumia umeme kwa kulipa hata Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwenye Bajeti zetu, kwenye vitabu vyetu tunatenga bajeti za kulipia gharama nyinginezo ambazo ni pamoja na umeme. Kwa hiyo, hayupo ye yote ambaye anatumia umeme bure.

Shirika la *TANESCO* linachofanya pale linazalisha na sisi wote tunafahamu kwamba shirika hili lina madeni chungu nzima tunadaiwa. Hata hivyo, *TANESCO* inadaiwa na *suppliers*, *TANESCO* inadaiwa na wazalishaji wa umeme, lakini kubwa hapa ni upatikanaji wa umeme kwa ajili ya kuendesha uchumi ndiyo jambo la maana zaidi.

Kwa hiyo, leo tusingekuwa na gesi hii hata Zanzibar umeme usingeweza kupatikana, lakini kwa sababu ya gasi ya Songsongo ndiyo maana leo hii Zanzibar kuna umeme na ndiyo maana Tanzania Bara tuna umeme.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Jaku aelewé kwamba tunapozungumza hapa hakuna ye yote ambaye anatumia umeme huu bure. Lakini kubwa ni upatikanaji wa umeme kwa kutumia rasilimali hii kwa ajili ya pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba Kamati itamaliza lini, kwa sasa taarifa hii inapelekwa kwa Wanasheria wakuu wa pande zote mbili ili waweze kupeleka kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ajili ya taratibu na hatua zinazofuata kwa maana ya maamuzi ya kisiasa na ya kisera.

**MHE. JOHN J. NYIKA:** Mheshimiwa Spika nashukuru. Katika sehemu a ya swali msingi wa swali ni manufaa ya wananchi kwenye suala la gesi na katika swali b ya swali

msingi wa swali ni marekebisho ya Katiba. Katika majibu ya Naibu Waziri kwenye suala la mapato ametaja suala la Songosongo na itakumbukwa katika Bunge hili kulitolewa ripoti mwezi Novemba 2011 iliyoeleza ujisadi kwenye mapato ya Songosongo uliohusu kampuni ya *Pan Africa* ambayo ilikosesha manufaa wananchi na Bunge likapitisha maazimio.

Ningependa kupata majibu kutoka Serikalini, maazimio ya Bunge ya mwaka 2011 yalikuwa ni kwamba mwaka 2012 Serikali iwe imefanya marekebisho na kutunga sheria maalum ya gesi na kushughulikia ule ujisadi kwenye mapato. Ni kwa nini mpaka sasa Serikali hajaleta sheria ya gesi, hajashughulikia kwa ukamilifu ujisadi uliotajwa wa mapato na kutungwa kwa sheria kungeondoa vile vile kasoro kwenye jambo hili juu ya masuala ya Muungano.

Ni kwa nini Serikali isiwajibike kwa kuendelea na taratibu za mizunguko ya leneni na taratibu zingine za gesi bila kwanza kushughulikia kasoro ambazo Bunge lilishaazimia lishughukiwe.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, sidhani kama ni rahisi sana kutunga sheria ya ujisadi na ujisadi hauwezi ukashughulikiwa na sheria moja. Lakini katika eneo hili nikubaliane na Mheshimiwa Mnyika kwamba yalikuwepo maazimio ya Bunge juu ya hatua za kuchukua dhidi ya *Pan Africa* kwa kuwa ilikuwa inasemekana inaipunja TANESCO kwa maana ya mapato na migawanyo yake.

Mheshimiwa Spika, hapa ielewewe wazi kwamba tuna deal na Pan Africa katika mambo mawili, wao wanatupa umeme na sisi tunauza umeme, lakini kwa namna ambavyo tunaishi na mahusiano haya ya kibiashara tuna madeni ya huko ndani.

Kwa hiyo wao wanatudai na sisi tunawadai, sasa katika hili ni jambo la kitaalam sana na tumeweza kufanya

na tumefikia katika hatua nzuri ya maelewano na katika hesabu zile sasa kama watu mnadaiana na katika deni lile ndani humo kuna kuvumiliana kwa sababu kimsingi wao wanatudai hela nyingi kuliko sisi ambazo tunawadai wao.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Mnnyika kwamba hatua zimechukuliwa na jambo hili tunaweza tukalitolea taarifa wakati muafaka kwa sababu taarifa yake ni ndefu, kwa sababu ina involved majadiliano yaliyofanyika kipindi kirefu na *negotiation* na *calculations*. Kwa hiyo, si rahisi kulisema hapa.

Mheshimiwa Spika, maana yameulizwa maswali mawili, sasa sijui nijibu hili hili moja?

**SPIKA:** Jibu swali moja.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, Ahsante sana.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi.

Na. 20

#### **Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Barabara**

**MHE. ISMAIL A. RAGE (K.n.y. MHE. MUNDE T. ABDALLAH)** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikikata fedha za mafuta kwa kila lita na kupelekea fedha hizo kwenye '*Road Toll*'

Je, Serikali haioni umuhimu wa kusimamisha makato hayo haraka kwa ununuzi wa mafuta ya gari moshi ili kupunguza makali ya gharama kwenye shirika la reli ambalo kwa sasa Serikali ina dhamana ya kulifufua.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sheria ya tozo ya mafuta na barabara inatokana na *Amendment Act No. 2* ya mwaka 1998 sura ya 220 iliyorekebishwa mwaka 2006 katika kifungu cha Nne, kifungu kidogo cha tano na imetamka bayana kwamba pesa za mfuko wa barabara zitatumika tu kwa ajili ya gharama za matengenezo na maendeleo ya barabara na si vinginevyo. Hivyo kusimamisha makato hayo kwa ununuzi wa mafuta ya gari moshi itakuwa ni kuvunja sheria iliyopitishwa na Bunge.

Aldha, maksudi na sababu zilizoifanya Serikali na Bunge ipitishe sheria hii bado zipo hazijabadilika. Fedha zinazokusanywa na Hazina kutokana na mfuko wa barabara bado hazitoshelezi mahitaji ya barabara zetu zinazohudumiwa na Wizara ya Ujenzi pamoja na TAMISEMI. Bodi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo *Development partners* inafanya utafiti wa kuongeza mapato ya mfuko ikiwemo kutafuta vyanzo vipyta.

Mheshimiwa Spika, iwapo Mheshimiwa Mbunge anaona sheria hii ina mapungufu anashauri kupeleka hoja yake Bungeni ili sheria iweze kufanyiwa marekebisho kwa kuwa ni Bunge pekee lenye uwezo wa kutunga ama kurekebisha sheria.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri. Je, Waziri hafahamu kuwa Shirika la Reli ni mali ya Tanzania na kama pesa zinapatikana kwenye *road toll* kwa nini na yeye asilete hoja ili tufanye *amendments* na shirika la reli liweze kufaidika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba sheria iliyotunga Mfuko wa Barabara ilikuwa ina maana ya kufanya kwamba

barabara hizi tunazoendelea kujenga mara nyingi tumekuwa tunakosa fedha za matengenezo, sasa ili mfuko uwe endelevu ulibuni kwamba *tu-ring fence* fedha kiasi fulani kutokana na matumizi ya mafuta ili ziweze kupatikana fedha za kufanya matengenezo na ndiyo ilikuwa lengo la kutunga sheria ya Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba lengo lile bado halijabadilika na kwamba fedha hizi mpaka sasa hazitoshelezi mahitaji. Tunapata fedha ambazo ni asilimia sabini tu ya mahitaji ambayo tunazihitaji kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kama unavyojua barabara hata kama ni ya lami tunafanya usanifu itumike kwa miaka 20, lakini kama unatumlia ilelami nyepesi inataka ikifika miaka saba utandike tabaka lingine la lami, lakini sasa kama huna fedha ina maana hautaweza kufanya kazi ile, na barabara zile zitashindwa kumudu ule muda ambaao umesanifiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba sana Mheshimiwa Rage na Wabunge wengine tunahitaji tuwe na mfuko maalum kwa ajili ya kutengeneza barabraa hizi kwa kutumia hii *fuel levy*.

Na. 21

**Ujenzi wa Terminal Three Uwanja wa Ndege  
wa J. K. Nyerere.**

**MHE. IDD M. AZZAN (K. n. y. MHE. ABASI Z. MTEMVU)**  
aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa *Julius K. Nyerere Terminal Three* uliopo Kipawa Jijini Dar es Salaam utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi napenda kujibu swali la Mhehsimiwa Abasi Zuberi Mtemvu, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Julius Kambarage Nyerere *Terminal three* uliopo Kipawa Jijini Dar es Salaam awamu ya tatu utahusisha ujenzi wa jengo jipya la abiria, *Terminal Building No. 3* pamoja na miundombinu yake. Mkandarasi wa ujenzi amekwishapatikana na kusaini mkataba wa kazi tarehe 18 Mei, 2013.

Sehemu ya eneo la kazi lilikabidhiwa kwa Mkandarasi yaani *partial site hand over* ili aweze kufanya tathmini mbalimbali za kazi tarehe 29 Mei, 2013.

Mheshimiwa Spika, makabidhiano ya eneo lote la kazi yalichelewa kwa sababu ya kuwepo kwa makaburi ndani ya eneo la mradi, hivyo ilibidi tukamilishe kulipa kifutajasho kwa Ndugu wa wafu tarehe 8 Oktoba, 2013.

Mheshimiwa Spika, kazi za ujenzi yaani *physical works* zinatarajiwa kuanza mwezi Januari mwaka kesho na kukamilika mwezi Oktoba mwaka 2015. Kazi hizi zinatarajiwa kufanyika kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa jengo la abiria na usimikaji wa mitambo mbalimbali kama vile mifumo ya ulinzi na usalama, habari na mawasiliano na ya kubeba au kusogezza mizigo.

Jengo hilo litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuhudimia abiria milioni tatu na laki tano (3,500,000) kwa mwaka, maegesho ya ndege na madaraja *air bridges* yatakayokidhi ndege kubwa tano aina ya *B777- 300ER*.

Awamu ya pili itahusisha ujenzi na ufungaji wa mitambo ya kuhudimia abiria milioni mbili na laki tano (2,500,000) kwa mwaka na maegesho ya ndege yatapanuliwa kuweza kukidhi kuegesha ndege kubwa ta

abiria aina ya *Airbus* 380. Awamu hii itaanza mara tu baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba pindi mradi huu utakapokamilika uwanja wa ndege ya kimataifa wa Julius Nyerere utaweza kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka na kuegesha aina zote za ndege zilizopo katika matumizi duniani.

**MHE. IDD MOHAMED AZZAN:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mradi huu ulikuwa uanze siku nyingi sana, lakini ulichelewa kama alivyosema Waziri kwa sababu ya kulipa fidia kwa yale makaburi ama kifuta jasho kwa yale makaburi kitu ambacho kilikuwa kinajulikana mapema sana lakini kilicheleweshwa mno.

Nataka *commitment* ya Serikali sasa kwa sababu umesema kwamba mnatarajia Januari, 2014 ndiyo mtaanza lakini nataka uthibitisho ndani ya Bunge hili kwamba ni kweli lini ujenzi wa uwanja huu wa ndege utaanza, kwa sababu ni kitu ambacho kinatia aibu Taifa letu kwa wageni wanaokuja nchini.

Swali la pili, kwa kuwa uwanja unaotumika hivi sasa uko kwenye hali mbaya sana, hauna viroza hewa na mara nyingine unavuja wakati wa mvua. Kuna mkakati gani wa kuufanya marekebisho wakati unashubiri uwanja huo mpya uanze kufanya kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba tu kama nilivyojibu katika swali langu la msingi nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote

kwamba ujenzi wa uwanja huu utaanza mwezi Januari mwaka kesho (2014) kama nilivyosema. Hatuna shaka na hili jambo kwa sababu fedha kwa ajili ya ujenzi zipo. Benki ya HSBC ya Uingereza itatoa asilimia 85 ya gharama ya mradi wa awamu ya kwanza na benki yetu ya CRDB itatoa asilimia 15 ya gharama ya mradi awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, labda tu niseme kwamba awamu hii ya kwanza itagharimu shilingi bilioni 290 hivi na hizi fedha zipo. Kwa hivyo, sasa hivi ni hizi taratibu tu za kawaida ambazo zinafanyika na hivyo mwezi Januari tuna hakika ujenzi utakuwa umeanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwanja wa sasa *terminal two* na *terminal one*, sasa hivi tupo katika hatua ya kufanya tathmini Mhandisi mshauri amekwishapatikana anafanya tathmini ili tuje ukarabati na gharama zake zitakuwa kiasi gani ili na yenye we tuiingize katika *program* ya kufanya matengenezo.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa, usafiri wa anga ni jambo la muhimu sana na kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa letu, na kwa kuwa, Serikali kuititia Wizara ya Maliasili inatangaza vivutio vilivyopo upande wa Kusini, na kwa kuwa uwanja wa ndege wa Nduli ni kiunganishi muhimu sana kwa upande wa Kusini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kasi kuutengeneza na kuukarabati uwanja wa Nduli uliopo katika Manispaa ya Iringa, Jimbo linalotoka Mheshimiwa Spika. Naomba majibu.

**SPIKA:** Ningejua nisingekupa nafasi, Waziri majibu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nimekwishasema hapa Bungeni mara nydingi kwamba pamoja na viwanja saba ambavyo vinafanyiwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

matengenezo na ukarabati kwa sasa, Serikali kuitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inatarajia pia kufanya matengenezo kwa viwanja vingine 11 kiklwemo kiwanja cha Nduli cha Iringa.

Sasa hivi, hatua tuliyofikia kwenye hili jambo ni kwamba *no objection* imekwishapatikana kutoka Benki ya Dunia na sasa hivi tupo katika kuandaa *documents* kwa ajili ya kutangaza mzabuni ambaye atakuja kufanya *design* na *feasibility study* katika viwanja vyote hivi 11.

Mheshimiwa Spika, labda tu kwa idhini yako naomba nimtoe hofu pia Mzee Ndesamburo, aliniuliza jana.

**SPIKA:** Hapana. Siyo suala la kutoana hofu hapa. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Christowanja Mtinda, atauliza swali linalofuata.

Na. 22

### **Wafungwa Wenye Ujuzi Mbalimbali**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA** aliuliza:-

Baadhi ya Wafungwa walioko Magerezani huwa wana ujuzi mbalimbali hususani Ufundu Seremala:-

Je, Serikali inautumiaje ujuzi wa Wafungwa hawa hususani wale Wafungwa wa muda mrefu na wenye kifungo cha maisha?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza lina jukumu la kuwahifadhi mahabusu na wafungwa wa aina zote pamoja na kuwarekebisha tabia kwa wale ambao wamehukumiwa vifungo. Urekebishi hajiwatia za wafungwa hufanywa kuitia *program* za mafunzo kwa njia ya vitendo katika miradi ya kilimo, viwanda vidogovidogo, ujenzi na mafunzo ya ufundi katika chuo cha ufundi cha Magereza Ruanda Mbeya, pamoja na gereza la Vijana Wami Morogoro.

Mheshimiwa Spika, lengo la *program* hizi ni kuwafanya wafungwa wawe raia wema ili watakaporudi uraiani au katika jamii waweze kutoa mchango katika kukuza maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu hayo Jeshi la Magereza linao utaratibu wa kuwatumia vizuri wafungwa walio na ujuzi katika kufanyakazi za uzalishaji kama vile ujenzi, kilimo, utengenezaji wa samani na kadhalika. Aidha, kuitia shughuli hizo husaidia pia kuwapa ujuzi walionao wafungwa wenzao.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi sana katika Wizara zake mbalimbali na Idara kwenye Bajeti zake za kununulia samani za maofisini na mara nyingi Serikali imekuwa ikiagiza samani hizi kutoka nje ya nchi tena zikiwa hazina ubora kuliko hizi ambazo zinatengenezwa na wafungwa waliopo katika Magereza zetu na kwa kuwa, shule nyingi za Msingi na Sekondari katika nchi yetu zinakabiliwa na uhaba mkubwa sana wa madawati na samani za maofisi.

Je, ni kwa nini sasa Serikali isiingie mkataba wa kudumu na Magereza zetu ili ziweze kuwatumia wafungwa hawa waweze kutengeneza samani pamoja na madawati kwa bei nafuu na zenye ubora kama ambavyo tunashuhudia? (*Makof*)

Swali la pili, kwa kuwa katika nchi yetu kila mkoa kuna magereza na katika magereza hayo kuna wafungwa wenye ujuzi na taaluma mbalimbali kuliko ile ya ufundi seremala ambayo nimeitaja. Kwa mfano walimu, udaktari, uhasibu.....

**SPIKA:** Swali liwe fupi.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Je, Serikali inawatumiaje wanataaluma hawa amba ni wafungwa katika kuzalisha mali na kufanya shughuli za nchi yetu ili kuweza kuendeleza taifa letu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, wazo la kuwa na Serikali isitumie fedha kuwalipa baadhi ya wazalishaji wa samani, lakini pia kuingiza samani ambazo pengine hazina thamani kutoka nje limeshazingatiwa na Serikali na kwa sasa tayari Idara ya Magereza kwa kutumia wafungwa wameshaanza kupewa tenda za namna hii ili kuhakikisha kwamba samani za Serikali sasa zitafanywa hasa na wafungwa au Shirika la Magereza kama ilivyokubaliwa.

Naomba nipongeze Bunge hasa Mheshimiwa Spika kwa kutoa mfano mzuri katika hili katika Ofisi za Wabunge Wilayani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya watu wenye taaluma nyingine kama walimu. Moja katika taratibu ndani ya magereza ni kwamba wale ambao hawana hata elimu ya kuandika na kusoma huwa wanapata mafunzo kule.

Kwa hiyo, kila mwenye elimu ambayo inaweza ikatumika magderezani inatumika na walimu wanatumika kwa kuwafundisha (a), (b) na (c) na mambo mengine wenzao ambao hawakuweza kupata wakiwa uraiani.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna nguvu kazi hii ya wafungwa wenye ujuzi hasa ujuzi wa ujenzi na kwa kuwa Serikali sasa inatumia fedha nyingi sana kujenga madarasa, hospitali na kadhalika katika Wilaya mbalimbali.

Je, ili kuokoa sasa fedha hizi nyingi ambazo zinalipwa kwa Wakandarasi ni kwa nini Serikali isitumie utaratibu nzuri, isiwe na utaratibu nzuri wa kuwatumia wafungwa hawa ili kuokoa hizo fedha na kuweza kufanya kazi nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba tayari tunatumia wafungwa kwenye samani, niseme pia tunatumia wafungwa katika kandarasi za ujenzi. Ndani ya Magereza kuna Shirika ambalo pamoja na mambo mengine linachukua kandarasi za kiujenzi na baadhi ya watu ambao wanatumika ni hao.

Katika maeneo ya shule na sehemu nyingine kwa sababu kila sehemu kuna mikoa ni suala la kuwasiliana kwa vipi tunaweza kuwatumia hawa ambao wapo katika utaratibu unaokubalika ili waweze kusaidia katika ujenzi wa nchi hii.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi. Kwa ridhaa yako Mheshimiwa Spika naomba kwanza nitoe pole kwa wapiga kura wangu katika Kijiji cha Mvugwe na Kitanga kwa mauaji ambayo yametokea kutokana na Operesheni Kimbunga.

Mheshimiwa Spika, bila kuathiri maamuzi ya Mahakama nilikuwa ninaomba kujuu kwa kuwa kuna msongamano mkubwa katika Magereza yetu hasa Mkao wa Kigoma ambako kunaendelea Operesheni Kimbunga. Ni kwa nini Serikali isilione hili na kuweza kupunguza

msongamano kwa wale wafungwa ambao wamehukumiwa miezi sita waweze kufungwa kifungo cha nje ili kupunguza msongamano katika Magereza yetu na kupunguza athari za kiafya ambazo zinaweza zikajitokeza mle? Ahsante sana.

**SPIKA:** Haya swalii lingine kabisa kabisa kabisa. Lakini naomba ujibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nami nitoe pole kwa hilo alilolisema. Lakini niahidi kwamba nitalifuatilia na kuweza tushauriane nini kilitokea ili haki itendeke kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msongamano wa wafungwa Magerezani kswa kweli hili ni tatizo kubwa na ni changamoto ambalo tunalishughulikia kwa kutumia mbibinu zaidi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameipendekeza.

Ni jambo ambalo tunalifanyia kazi na ni dhahiri kwamba tayari tuna mafanikio katika hilo. Kwa sababu kwa jumla msongamano unapungua na tutaendelea kuhimiza matumizi ya Sheria na vifungo mbadala ili kupunguza msongamano Magerezani.

**SPIKA:** Naomba tuendelee muda uliyopo hautoshi. Twende Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, atauliza swalii hilo.

Na. 23

### **Usumbuu wa upatikanaji wa viza ya Israel**

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE** aliuliza:-

Watu wengi wanayo nia ya kutembelea nchi ya Israel lakini hupata usumbuu mkubwa wa kupata visa za nchi hiyo ambazo hutolewa Nairobi nchini Kenya:-

Je, Serikali itasaidiaje kuondoa usumbuu huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Luckson Mwanjale, kama ifuatayo:-

Ni kweli kuwa kumekuwepo na usumbufu wanaoupara Watanzania wakati wa kuomba visa kwenye baadhi ya Balozi ikiwemo Balozi ya Israel. Ikumbukwe kuwa Ofisi ya Ubalozi wa Israel iliyopo Jijini Nairobi nchini Kenya ni moja ya Balozi kumi na moja (11) tu za nchi ya Israel katika Bara lote la Afrika.

Mheshimiwa Spika, kila nchi kwa mazingira yake ya kibajeti, kijamii, kiulinzi na usalama imojiwekeea masharti yake katika utoaji wa visa kwa wageni wanaotembelea nchi hiyo. Sharti mojawapo la utoaji wa visa kwa nchi ya Israel linamtaka mwombaji wa visa aende Nairobi kwa ajili ya kufanya mahojiano ya ana kwa ana na maafisa wa Ubalozi wa nchi hiyo. Hivyo, usumbufu unaopatikana wa kusafiri kwenda Nairobi ili kupatiwa visa hiyo unatokana na uamuzi wa kisera wa nchi ya Israel amba hauwezi kulingiliwa na nchi nyingine.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ya Serikali nina swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inakiri kuwepo kwa usumbufu huo hasa kwa wananchi amba wanaosafiri Israel.

Je, haiwezi Serikali ikaishauri Serikali ya Israel kufungua Ofisi angalau ndogo au kuungankisha shughuli za Ofisi ya Israel kwa ofisi nyingine ya Ubalozi hapa Tanzania ili wananchi waweze kuondolewa usumbufu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inaweza kuishauri Israel kuweza kufungua Ofisi hapa Tanzania. Lakini bado uamzi wa mwisho utaendelea kubaki kwa nchi hiyo ya Israel.

Na. 24

**Kusuasua Kwa Mradi wa Maji wa Maji wa Vijiji Kumi  
Kwa Kila Wilaya**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Utekelezaji wa mradi wa maji wa Benki ya Dunia katika vijiji kumi kila Wilaya umechukua muda mrefu sana na katika Wilaya nyingine utekelezaji hujaanza na hivyo kusababisha malalamiko na lawama nydingi kwa Serikali toka kwa wananchi:-

- (a) Je, Serikali inawaambia nini wananchi kuhusu ucheleweshaji huu hususan katika Wilaya ya Kahama?
- (b) Katika Jimbo la Kahama kuna miradi mitano (5) kati ya kumi (10) iliyopangwa katika Wilaya hiyo.

Je, ni miradi mingapi imekamilika na mingapi bado na kwa sababu gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Daud Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, ni kweli utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji kumi (1) ijlikanayo kama miradi ya vijiji ya Benki ya Dunia kwa kila Halmashauri ikiwemo Halmashauri ya Kahama umechukua muda mrefu. Miradi ya vijiji 10 inatekelezwa kwa kufuata taratibu za manunuzi za Benki ya Dunia.

Taratibu hizi zilikuwa ni mpya kwa Halmashauri zote nchini na Halmashauri hazikuwa na wataalamu wenye ujuzi wa kutumia taratibu hizi mpya ambazo zilihusisha Halmashauri kupata vibali mbalimbali kabla ya kuanza ujenzi yaani *No Objection*.

Kwa sasa Halmashauri zimeshajengewa uwezo wa kutosha na Serikali imeondoa taratibu za upatikanaji wa vibali vyta miradi ya maji ya vijiji 10 na hivyo kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hii.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kahama inatekeleza miradi ya maji ya vijiji 10, kwenye vijiji nya Bulige, Segese, Chela, Kagongwa na Lunguya katika Jimbo la Msalala na vijiji nya Nyamilangano, Iboja, Kangeme, Mbika na Shaka katika Jimbo la Kahama.

Ujenzi wa miundombinu ya maji umekamilika katika vijiji nya Bulige, Segese na Chela. Kwa vijiji vitatu (3) nya Shaka, Nyamilangano na Kagongwa ujenzi wa miundombinu ya maji unaendelea na unatarajiwa kukamilka mwezi Januari, 2014.

(c) Aidha, utafiti wa kupata vyanzo vipyta nya maji kwa vijiji nya Iboja, Kangeme, Mbika na Lunguya viliviyokosa vyanzo nya maji sasa hivi unaendelea.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa utafiti wa vyanzo vipyta nya maji katika vijiji nya Iboja, Kangeme na Mbika katika Jimbo la Kahama umechukua muda mrefu na kwa kuwa watafiti wanaofanya utafiti huo mpya wamekuwa wakipuuza ushauri ambao umetolewa na wenyeji katika maeneo hayo juu ya maeneo yenye vyanzo nya maji nya asili. Hivyo kuwafanya wakate tama.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuona kwamba kasi ya kutafuta hivyo nya maji inaongezeka ili hatimaye miradi hiyo iweze kuanza kutekelezwa? Nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli miradi hii kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba imechukua muda mrefu. Lakini hatua mojawapo ambayo ilikuwa inafanywa ilikuwa ni kutafuta vyanzo vya maji na hii ilikuwa ina-engage wataalam.

Kwa hiyo hii hatua ilipokwisha ikaonekana vile vijiji alivyovitaja vimekosa vyanzo vya maji na tukasema kwamba tutarudia kuangalia maeneo mengine yanayoweza kuwa na vyanzo vya maji.

Kwa hiyo, sasa hivi ninavyoongea utafiti huu umeanza kufanywa na unafanywa na Maafisa wangu wa bonde la maji la Kati ambao wana vifaa vya kutosha na kazi hii wameshaanza na nimeongea na Mkurugenzi kwamba tayari wanafanya hiyo kazi.

Nichukue ushauri kwamba nitawaagiza watu wangu kwamba washirikiande na wananchi wa maeneo husika ili waweze kutumia huo ushauri ili waweze kupata vyanzo vya maji vinavyotakiwa.

Lakini Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwaomba Halmashauri zote kwamba watu wenye vifaa vya kutosha na vizuri vya kisasa ni Ofisi zetu za Mabonde ziko tisa (9) na Halmashauri inafahamu hizi Ofisi. Watumie wale wataalam ambao wanaweza wakafanya utafiti wa uhakika na kuainisha maeneo yenye maji. (*Makofii*)

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika aHsante. Mheshimiwa Spika katika Jiji la Arusha wakazi wanaopata maji tena kwa mgao ni chini ya asilimia 38 na kwa sababu maji ni uhai na kuna mipango mingi ambayo inaendelea lakini ukiongea na wataalam kule chini wanassema kwamba *bureaucracy*iko Wizarani. Nini kauli ya Serikali juu ya matatizo ya maji Arusha Mjini huku Serikali ikitambua kwamba bila maji watu hawawezi kuishi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza sikubaliane kwamba kuna *bureaucracy* Wizarani na kama hili lipo tumwombe Mheshimiwa Mbunge na wengine wote tupewe taarifa sisi viongozi ili tuweze ukufanya mambo kama hayo kama yapo badala ya kuja kuyasema hapa bila kutoa uthibitisho.

Lakini ni kweli lipo tatizo la maji Mjini Arusha sasa hivi na pale tuna Mamlaka ya Maji *AUSA* ambayo ndiyo inayosimamia kwa niaba ya Wizara ya Maji. Tatizo kubwa la maji sasa hivi lipo kwenye kiangazi ambako vyanzo vingi nya maji vinakauka.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na viongozi wote wa Arusha wasimamie vile vyanzo nya maji, watu wasifanye kazi kwenye vyanzo nya maji kwa sababu maji yanapungua. Lakini Serikali imeweka mikakati ya kuona kwamba mamlaka hii inaboresha huduma ya maji na hivi karibuni tulikuwa tunaongea na wafadhili ili waiwezeshe hii mamlaka iweze kupata fedha za kutosha iweze kupanua mtando wa maji.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Alhaj Jafo. Nafikiri Alhaj. Alhaj Jafo.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Asante Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa mpango wa maji hivi sasa katika vijiji 10, tumeanza na vijiji vitano na kwa kuwa kwa baadhi ya makampuni yaliyopata tenda hizi uhalsia katika utendaji wao wa kazi unaonekana kwamba hawawezi kufanya kazi vizuri kufanikisha hii miradi kwisha ndani ya muda.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka sasa katika hawa wakandarasi waliopewa katika kazi ya kujenga miundombini kwamba kuwatathminia kufanya tathmini ya haraka ili mradi kwamba wasije wakakwamisha hii miradi kiasi kwamba wananchi wakapata kadhia ya kukosa maji kuitia miradi ya *World Bank*?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI;** Mheshimiwa Spika, kazi ya kusimamia utekelezaji wa miradi hii ipo kwenye Halmashauri. Halmashauri ndiyo inafanya mchakato mzima wa kumpata mkandarasi na ndiyo inayemwosha kazi na inamsimaia. Kwa hiyo, niwaombe viongozi wote kwamba kama Halmashauri zitasimamia vizuri na zitachagua wakandarasi vizuri maana yake zitapata watu ambao wanaweza wakafanya ile miradi vizuri.

Lakini sisi tumeagiza kwamba wale wakandarasi wote ambao itaonekana kwamba hawafanyi kazi yao vizuri wasipewe kazi tena illi wapewe watu wenye uwezo kwa ajili ya kutengeneza miradi hii kwa kasi inayotakiwa.

**SPIKA:** Tuna muda mfupi naomba twende Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na atakayeuliza swali hilo ni Mheshimiwa Rukia K. Ahmed.

Na. 25

**Tanzania Kutoshirikishwa Katika Mambo  
Yanayohusu Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. RUKIA K. AHMED** aliuliza:-

Katika mkutano uliofanyika Mombasa siku ya ufunguzi wa bandari ya Mombasa mambo yaliyojadiliwa ni pamoja na biashara, miundombinu na Shirikisho la Afrika Mashariki.

Je, ni nini msimamo wa Serikali juu ya mambo yanayohusu Jumuiya ya Afrika Mashariki kujadiliwa na kutolewa uamuzi bila ya Tanzania kushiriki?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, jibu la swali la Mheshimiwa Rukia Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, ni kama ifuatavyo:-

Mikutano ya Wakuu wa nchi za Kenya, Rwanda na Uganda bila kuishirikisha Tanzania ilianza ghafla kule Entebbe, Uganda tarehe 24 na 25 Juni mwaka huu, 2013. Burundi pia hawakushiriki.

Mheshimiwa Spika, mikutano wa pili wa viongozi hao ulifanyika mjini Mombasa, tarehe 28 Agosti, 2013, kwa kigezo cha uzinduzi rasmi wa gati namba 19 la bandari ya Mombasa ambalo limepangwa kuwa ni mahsus kushughulikia mizigo ya Rwanda na Uganda.

Mheshimiwa Spika, pamoja na suala hilo la bandari ya Mombasa ilijitokeza kwamba Wakuu hao wa nchi tatu walijadili pia masuala ya uanzishaji wa Himaya Moja ya Forodha Kiingereza (*Single Customs Territory*) uanzishaji wa visa moja ya utalii kwa nchi zao, matumizi ya vitambulisho vya kitaifa kama hati za kusafiria baina ya watu katika nchi hizo tatu na mwisho kuanzisha harakati za kuharakisha Shirikisho la Kisiasa la nchi hizo tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa masuala hayo yapo katika hatua mbalimbali za majadiliano katika ngazi ya Jumuiya ambapo nchi zote tano hushiriki, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mikutano wa 27 wa Baraza la Mawaziri uliofanyika mjini Arusha tarehe 31 Agosti mwaka huu, 2013.

Tulidai ufanuzi na kumtaka Mwenyekiti wa Baraza letu Uganda kutoa taarifa ya kina kuhusu mikutano hiyo ya utatu inayoendeshwa sambamba na mikutano ya kawaida ya kalenda ya Jumuiya. Kikao cha Baraza la Mawaziri wa Jumuiya cha kutathmini hali hii kimepangwa kufanyika mnamo juma la pili la mwezi ujao mjini Arusha.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

### *[WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI]*

Mheshimiwa Spika, wakati tukisubiri taarifa hiyo kutoka kwa wenzetu, msimamo wa Serikali ya Tanzania ni kuwa, masuala yoyote yanayojadiliwa na kuamuliwa nje ya utaratibu wa Jumuiya hatuyatambui kama maamuzi ya Jumuiya. Hivyo, utekelezaji wake utazihusu nchi husika peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote watambue kwamba, tuko makini katika kufuutilia yote yanayotokea katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwamba, wakati wote tutahakikisha maslahi ya Tanzania yanalindwa kwa njia zozote tutakazoona zinafaa. (*Makofi*)

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, bado nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, Tanzania inaendelea kutengwa katika Jumuiya hii ya Afrika Mashariki kwa wenzetu hawa kukutana Marais wa Rwanda, Kenya na Uganda, bila kuishirikisha Tanzania. Je, Serikali haioni kwamba, ushirikiano huu unakwenda kinyume na makubaliano ya Mkataba wa Umoja huu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Tanzania, Mheshimiwa Membe, alikaririwa katika vyombo vya habari akisema kuwa, tunachosubiri Tanzania ni talaka. Je, kwa kutumia Ibara ya 145 ya Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya hii, Serikali iko tayari kuleta pendekezo Bungeni, ili Bunge liridhie na tuweze kujitoa katika umoja huu kabla ya kupewa hii talaka? Kwani jambo la talaka ni baya mno, hata katika dini zetu linapingana nalo; je, Mheshimiwa Waziri unasemaje? (*Makofi/ Kicheko*)

**SPIKA:** Ningetamani sana Waziri ajibu swali linalofuata kwa sababu, majibu yatafanana tu. Swali linalofuata ni la Mheshimiwa Kapteni Komba, linafanana hivyo hivyo, atajibu na yote haya.

Na. 26

**Rwanda na Burundi Kuingia Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Kabla ya Rwanda na Burundi kujinga na Jumuiya ya Afrika Mashariki hali ilikuwa tulivu na yenye maelewano makubwa, lakini mara baada ya nchi hizo kuingia imekuwa tete:-

(a) Je, ni kitu gani kilisababisha nchi hizo kukubaliwa kujinga na Jumuiya hiyo?

(b) Je, kwa nini Tanzania isijitoe kwenye Jumuiya hiyo, kama ilivyofanya kwenye *COMESA*?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, jibu la swali la Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Damiano Komba, Mbunge wa Mbanga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b), ni kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa masharti ya Mkataba wa Jumuiya, nchi za Burundi na Rwanda zilifanyiwa uhakiki kuthibitisha kama zinakidhi vigezo vyta kujinga na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mujibu wa Mkataba wa Jumuiya na nchi hizo zikafuzu. Hivyo, Wakuu wa Nchi Wanachama, yaani Kenya, Tanzania na Uganda, waliridhia na kuruhusu nchi hizo kujinga na Jumuiya ya Afrika Mashariki mnamo 2007.

(b) Mheshimiwa Spika, katika dunia ya sasa ya utandawazi, mtangamano wa Kikanda ni Sera sahihi kwa nchi husika ili kujenga uchumi endelevu. Aidha, nchi za Afrika Mashariki zina historia ndefu ya mtangamano tangu enzi za mkoloni na wakati wote Tanzania imekuwa ni sehemu muhimu ya mtangamano. Changamoto chache za mpito

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI]*

zinazojitokeza ndani ya Jumuiya hivi sasa hazijafikia kiwango cha kuilazimisha nchi yetu kujitoa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kinachohitajika ni kwa nchi wanachama kuzishughulikia changamoto hizo kwa uwazi na weledi ili kuimarisha mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambao wananchi wake wananaufaika nao kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako nadhani sasa nijibu maswali mawili ya nyongeza Mheshimiwa Rukia Ahmed:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni kweli kabisa inakera kuona wabia wetu katika Jumuiya kama vile wanatuzunguka. Lakini nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tufuate ushauri wa Rais wetu Mstaafu, Alhaji Ali Hassan Mwinyi; katika mazingira yanayofanana Rais Mwinyi aliasa kwamba, mwongo mwongoze. Maana yake ni hivi, kama wenzetu hawa wana hila, haitachukua muda tutazibaini tu.

Mheshimiwa Spika, jana wamekutana tena kule Kigali, lakini kwa kuwa sisi tayari tumeshamhoji Mwenyekiti wetu wa Baraza la Mawaziri na baada ya wiki mbili tuna Kikao, basi tusubiri hicho tutakachoambiwa. Kama utaendelea uwongo wa kitoto, Serikali hii ni makini, tutakuja Bungeni na tutaweka mapendekezo ambayo yatakuwa yanakabiliana na hali ya kuchezewachezewa, hatuvezi kukubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili la talaka, kwanza silikubali hili, tusifanye kwamba, Tanzania ndio imeolewa, kwa sababu, Tanzania ni 52% ya eneo zima la Afrika Mashariki, iliyobaki ni 48%. Kwa hiyo, nadhani sisi labda ndio unaweza kusema ndio waoaji. Sasa kwa talaka, sisi hatuisubiri; nadhani walikosea kumnukuu Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Membe, kama ni talaka tutaitoa sisi. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa nini sasa Jumuiya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. J.D. KOMBA]

iliyopo ya Afrika Mashariki isilaani kitendo hiki ambacho kinaunda Jumuiya mpya ndani ya Jumuiya ya zamani?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa nini na sisi tusiunde Jumuiya yetu mpya ya Tanzania Burundi na Kongo, badala ya kuwabembeleza hawa Marais wa ajabu ajabu? (*Makofi/ Kicheko*)

### **WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Mheshimiwa Spika, la kwanza, la kusema kwa nini sisi Tanzania tusilaani kitendo cha hawa wenzetu kuanzisha inayoitwa "Jumuiya ndani ya Jumuiya". Hali halisi ni kwamba, wala hawajaanzisha, wamo katika harakati fulani ambazo mwisho wake hatuuji. Ikitika mahali wanaikubali hiyo Katiba Mpya, ambayo Rasimu yake wanaizungumza, tutajua uamuzi wa kuchukua, lakini ni mapema mno wakati wenzetu bado wapo katika hatua hizo za maandalizi fulani, sisi tuchukue hatua tena kuwalaani, tutakuwa tunazidi kuharibu hali iliyopo.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, tukumbuke kwamba, nchi zetu hizi za Afrika, mara nyingine matatizo yanaletwa na Viongozi tu; mnaelewa ni kwa nini Rwanda inatununia, lakini nchi kama Rwanda au Burundi, Tanzania, zitaendelea kuwepo tu. Kwa hiyo, tusichukue hatua sasa ambazo zinajibu uchokozi fulani, matokeo yake sisi tuwe tumeharibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndio sababu kwa nini hatuchukui hatua ya kulaani hivi sasa, lakini wakati wowote mambo yakidhihirika, basi ninyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge tutawashirikisheni na hatua tutakayoichukua itakuwa ni hatua ya hekima yenze kulinda maslahi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili la Mheshimiwa Komba ni kwamba, kama vile tunachelewa kuchukua hatua. Kwa kweli, kama nilivyojibu kwenye hili la kwanza, mambo mengine ni vizuri uyatazame ukiwa umetulia yafike mahali pake. Ushauri ni ule ule wa Rais wetu wa Awamu ya Pili kwamba, kama kuna uwongo, basi tuufuatilie mpaka tufike

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI]*

mwisho, ili mwongo mwenyewe aumbuke. Kama wanafanya mambo yao kwa hila wataonekana na wakati huo Tanzania itakuwa sio ya kulaumiwa tena.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Haya, Kanuni inasema kama swali limeulizwa, mwingine lisirudiwe. Mheshimiwa Anne Kilango nimemtaja, nikamtaja na Mheshimiwa Hamad. Mheshimiwa Anne Kilango kwanza, swali fupi!

**MHE. ANNE K. MALECEL:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, sasa ni dhahiri kwamba huu Umoja wa Afrika Mashariki unaweza ukavunjika. Je, Serikali haioni kwamba, kuna umuhimu wa kutokuendelea hatua nyingine yoyote ile, kusimamia hapa hapa tulipofikia katika Umoja huu?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, sisi Serikali sio kwamba, tumekaa tu kimya na mambo mengine hayaendelei. Kuna mambo ambayo tayari tumeanza kuyachukulia hatua kuonesha kwamba, hatuvezi kuendelea na kitu kama mchezo wa kuigiza; kwa mfano, tumekubaliana kwamba, ile Mikutano inayohusu masuala ambayo wenzetu wanayazungumza hatutahudhuria. Kwa hiyo, kwa mfano, kuna Mkutano Nairobi wa Mawaziri wa Mambo ya Nje, mamlaka kuu imeamua kwamba, Waziri wetu wa Mambo ya Nje asihudhurie.

Mheshimiwa Spika, hii ni sehemu tu kwa sababu, kama tunazungumza Sera ya Mambo ya Nje na wenzetu wanataka kuunda Shirikisho bila kutushikisha sisi, sasa haina maana kwenda kukaa katika vikao ambavyo hayo yanayozungumzwa wenzetu wanakuwa tayari wana msimamo nayo. Kwa hiyo, baadhi ya hatua tunazochukua, ni kutokelewa kwenye vikao vyote ambavyo wenzetu kwenye masuala hayo tayari wana msimamo kwa sababu, hiyo haina maana tena ya kujadiliana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaitazama hali hii siku hadi siku. Kuna Mkutano kesho Burundi, nimemwagiza Naibu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI]*

Waziri asihudhurie kwa sababu *agenda* zake ni hizo hizo za kuwa na mchezo huu unaendelea mnakutana kwa *agenda* za kawaida, wenzetu wameshazichukulia msimamo, lakini Katibu Mkuu wetu wa Wizara, anaondoka leo anakwenda kuhudhuria. Tumetoa ushauri kwa wenzetu wote Watendaji wanaohudhuria vikao wakati sisi wanasiasa hatupo kwamba, hawana haja ya kutoa msimamo wowote kwa sababu, sio jukumu lao; wasikilize halafu waje watueleze.

Mheshimiwa Spika, haya yote ni sehemu tu ya kuonesha kwamba, Tanzania haifurahishwi na hicho kinachoendelea. Tusubiri, maana tumetafuta ufanuzi kutoka Makao Makuu ya Jumuiya na Mwenyekiti wa Jumuiya, tusubiri bado wiki mbili tupate majibu. Baada ya hapo nchi itachukua hatua. Ahsante.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, sina uhakika kama Waziri anafahamu kwamba, hivi sasa wenzetu wa Kenya, ili kuanza kuona wanaitenga Tanzania wameingia makubaliano na Ethiopia na Sudan, ili kuona kwamba, ni kwa njia gani wanaweza kupanua hilo soko. Katika Jumuiya hii ambayo inaundwa hivi sasa wao wanaendelea na hizo *economic program* zao wakati sisi bado tunangojea ushahidi. Je, Waziri haoni kwamba, sasa ni wakati muafaka sisi kuanza kukaa kujipanga upya *the fallback position* badala ya kungoja ushahidi? (*Makofii*)

### **WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Mheshimiwa Spika, ninaposema ushahidi ni kwamba, mambo mawili yanaendelea hapa. Moja, katika mahusiano ya Serikali, huwezi mwenzio ukamkadiria kutohana na zile dalili ukachukua hatua, lakini hiyo haina maana kwamba, hatujandai. Mazungumzo na Burundi yanaendelea, mazungumzo na *DRC* yanaendelea kwa maana ya kushirikiana.

Mheshimiwa Spika, pengine tufahamu tu kwamba, uchumi mkubwa hapa wa majirani ni *DRC* na sio Burundi wala

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI]

sio Rwanda; Rwanda inatugusa kwa sababu, barabara ya lami tulijojenga kwenda Rusumo inapita Rwanda ili kufika Goma, DRC, kwa hiyo, inakuwa na shida kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini yapo mambo mengi, tumeharakisha sasa hivi kipaumbele cha kujenga reli ya kutoka Uvinza kwenda Msongati ili tuwaokoe Burundi ambao kama wakilazimika kutumia Bandari ya Mombasa, umbali unaongezeka ukilinganisha na Bujumbura – Dar-es-Salaam, Bujumbura kwenda Mombasa, tofauti yake ni kilomita 900. Sasa huyo mfanyakishara atakayekubali kisiasa aingie gharama ya kuzungusha bidhaa kwa kilomita 900 za ziada, ni jambo la ajabu, lakini tuwasaidie Burundi kwa sababu, hata wao kwenye hili wanabaguliwa kama sisi.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa maeleo marefu uliyotoa, lakini naomba tuendelee maana yake nina maswali matatu, niwatendee haki wenye maswali yao. Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Assumpter Mshama, atauliza swali hilo.

Na. 27

### **Hitaji la Minara ya Simu – Kata za Jimbo la Nkenge**

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA** aliuliza:-

Mawasiliano ni muhimu sana hasa katika nyakati tulizonazo za Sayansi na Teknolojia ("Do-Co"):-

(a) Je, ni kwa nini Kata za Buanjai, Bunyango, Ruzinga, Kitobo, Kakunyu, Kilimilile na Minziro hazifungwi minara ya mawasiliano ya simu wakati kuna idadi ya watu?

(b) Je, Serikali, inayo maeleo ya kuwardhisha wananchi wa Missenyi hasa katika Kata zilizotajwa katika swali hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mfumo uliopo wa leseni kwa Makampuni ya Mawasiliano, Makampuni ya Simu yana hiyari ya kupeleka mawasiliano kule yanakoamua. Hata hivyo, kwa kutambua haja ya kupatikana kwa mawasiliano kwa Watanzania wote, Serikali, ilianzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*UCSAF*) ambao unatoa ruzuku kwa Makampuni ya Simu kupeleka mawasiliano kwenye maeneo yasiyo na mvuto wa kibashara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika baadhi ya maeneo, licha ya kutolewa kwa ruzuku hii bado Makampuni ya Simu yamekuwa na uzito wa kupeleka mawasiliano na hili limeleta changamoto kwenye kasi ya kupeleka mawasiliano ikiwemo kwenye maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto hii ya kasi ndogo ya kupeleka mawasiliano, ikiwemo kuongeza ruzuku na kutafuta vyanzo mbadala vya fedha, kwa ajili ya kujenga minara kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote na Shirika la Simu Tanzania (*TTCL*).

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzifanyia tathmini Kata za Kilimilile, Kitobo, Buanjai na Buyango na kuangalia vigezo mbalimbali, ikiwemo idadi ya wakazi, shughuli za uchumi, kiasi cha ruzuku kinachohitajika, Serikali kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote imeziingiza Kata hizo kwenye orodha ya Kata za Zabuni ya awamu ya kwanza (b), ambayo zabuni

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA]

zake zinatangazwa mwezi Disemba mwaka huu. Aidha, Kata za Ruzinga, Minziro na Kakunyu, zitajumuishwa katika miradi ijayo ya Mfuko, kutegemeana na upatikanaji wa ruzuku.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ukiangalia Mikataba ya haya Makampuni utakuta wamesema kwamba, watapeleka masafa nchi nzima, lakini pia, hapo hapo kuna kipengele kinasema kwamba, kwa hiyari yao watapeleka mawasiliano. Je, Serikali haioni kwamba, hapo kuna kiini macho na hamwonni kwamba, hiyo ni haki ya kila Mtanzania kupata mawasiliano mahali popote alipo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nashukuru kwa mkakati unaoendelea katika Kata hizo nyingine za Kitobo, Buanjai na sehemu zingine; lakini Kata ya Luzinga, Kata ya Minziro na Kakunyu ni Kata ambazo zipo mpakani mwa Tanzania na Uganda na walivyomaliza kuongea hapa unaona mambo yanavyoendelea na wale watu wa Kakunyu na Minziro pamoja na Luzinga wanatumia mtandao wa Uganda. Je, Waziri haoni kwamba ni vyema tukatumia labda vigezo vingine vya ulinzi na usalama kuliko vya kiuchumi ili wale wananchi wapate mawasiliano katika nchi ya Tanzania? (Makof!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba makampuni haya yalipokuja kuomba leseni unapewa na masafa aina mbalimbali *megahertz* 900 na 1800 na masafa hayo ni ya nchi nzima, lakini kwa sababu tuliamua kwamba sekta hii iwe ni iendeshwe na sekta binafsi hakukuwa na masharti ya kushurutisha kampuni hizi zipeleke mawasiliano mahali husika. Ndiyo maana Serikali sasa kwa kutambua hilo ikaanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ili kutoa ruzuku kupeleka mawasiliano kule ambako hakuna mvuto wa kibiaresha kwa sababu tuliamua shughuli hii iwe ya sekta binafsi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA]*

Mheshimiwa Spika, sasa ziko namna tatu za kuweza kupeleka mawasiliano katika maeneo. Kwanza, ni kuyashurutisha makampuni yapeleke kama Serikali na hilo halipo na halipo kwenye sheria na hatuwezi.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kutoa ruzuku kama tunavyofanya kwenye Mfuko wa sasa, lakini ya tatu ni sisi wenyewe kama Serikali kujenga minara. Tunafanya yote mawili; kwanza, tunatoa ruzuku kule wanakosema ni gharama zaidi na hakuna watumiaji wengi na hakuna mvuto wa kibiashara, ndio maana upo Mfuko ambao unachangia kwa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini pili tumeamua sasa kwamba, tutafute fedha nyingi zaidi kupitia mkopo kutoka Serikali ya India ili tujenge hili minara wenyewe kupitia Shirika letu la Simu. Katika kufanya hivyo tuko kwenye mazungumzo ya kuamua kuchukua masafa kule ambako makampuni haya hayajapeleka mawasiliano ili masafa hayo tulipe Shirika letu la Simu Tanzania lijenge minara kule ambako makampuni haya hayakuweza kujenga.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mshama, ushauri wake tunauchukua, ni kweli kwamba, yako baadhi ya maeneo ya nchi yetu na kwa kweli tumeanza kufanya kwenye maeneo ya Ziwa Tanganyika mpakani kule na Ziwa Nyasa ambako kwamba inawezekana kabisa hakuna mvuto wa kibiashara lakini kwa sababu ni mpakani na lazima mawasiliano yawepo kwa sababu za kiusalama, basi sisi wenyewe kupitia fedha zetu za Mfuko tutajenga minara katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wabunge katika maeneo hayo ya mipakani, ni mashahidi kwamba tumeanza kufanya hivyo. Maeneo haya aliyoyataja Mheshimiwa Mshama bahati nzuri nayafahamu na yenyewe tutafanya hivyo.

Na. 28

### Dawa Sahihi Inayotibu Malaria

**MHE. MANSOOR S. HIRAN (K.n.y. MHE RICHARD M. NDASSA)** aliuliza:-

Hivi sasa kuna mkanganyiko juu ya dawa gani inayoweza kutibu malaria:-

Je, ni dawa gani sahihi inayotibu malaria?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Jimbo la Sumve na naomba kwanza kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya vimelea vya ugonjwa wa malaria kuanza kuonesha usugu kwene dawa aina ya *SP* yaani kama vile *Fansidar* na *metakelfin* na kufuatia ushahidi wa tafiti mbalimbali za kisayansi zilizofanyika Kimataifa na hapa nchini mwaka 2007, Serikali ili amua kubadili dawa ya safu ya kwanza kwa matibabu ya malaria isiyo kali kutoka *SPkwenda* dawa mseto yenyenye kinyambulisho cha *Artemisinin (ACTs)* hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matibabu ya malaria yamegawanyika katika sehemu au makundi makuu mawili, malaria isiyo kali na malaria kali.

Mheshimiwa Spika, dawa ya kutibu malaria isiyo kali ni mchanganyiko wa dawa mbili moja ikiwa yenyenye kiambata cha *Artemisinin*. *Artemetherna Lumefantrine* au maarufu kwa jina la *ALU* na kama tunavyoita dawa mseto dawa hii hunywewa kwa muda wa siku tatu kulingana na uzito na umri

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

wa mgonjwa. Aidha, dawa zingine za mseto zenye kinyambulisho cha *Artemesinin* ambazo zimasajaliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kwa matumizi ya siku zisizopungua tatu zinaweza kutumika.

Mheshimiwa Spika, kwa matibabu ya malaria kali ambayo dalili zake ni pamoja na homa na dalili za ziada zinazotokana na kutofanya kazi vizuri kwa baadhi ya viungo mwilini, dalili hizo ni pamoja na uchovu mpaka mgonjwa anashindwa kuketi au kusimama mwenyewe, kukosa ufahamu yaani *impaired consciousness* na huweza pia kuleta athari kwenye mapafu na figo.

Mheshimiwa Spika, malaria kali isipotibiwa vizuri na kwa haraka huweza kuleta madhara makubwa kwa mgonjwa na hata kusababisha kifo. Chaguo la dawa ya kutibu malaria kali ni sindano aina ya *quinine* ambayo kipimo cha dawa hutolewa kulingana na uzito wa mgonjwa. Sindano nytingine aina ya *Artesunate* na *Artemether* pia zinaweza kutumika kutibu malaria kali.

Mheshimiwa Spika, jambo la muhimu ni sio kila homa ni malaria, hivyo kwa kupitia Bunge lako, tunahimiza wananchi kuhakikisha wanapima na kuthibitisha kuwepo kwa vimelea vyta malaria ndipo wapatiwe au wapate kutumia dawa.

Na 29

### **Mpango wa Damu Salama**

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT** aliuliza:-

Kitengo cha mpango wa damu salama kimejitahidi sana kukusanya damu na kupeleka hospitalini:-

Je, ni kwa nini baadhi ya wagonjwa wanauziwa damu hiyo wanapohitaji msaada wa damu katika hospitali zetu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mbunge wa Jimbo la Koani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Serikali ni kutoa damu bila malipo kwa wagonjwa wanaohitaji damu katika Hospitali zote za Umma, binafsi na Mashirika ya Dini. Ni kweli Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina taarifa za kuwepo kwa vitendo vya uuzwaji wa damu katika baadhi ya Hospitali, vitendo vinavyofanywa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi za malalamiko tunazipata kupitia mitandao ya kijamii, sanduku la maoni katika Vituo vya Damu Salama, namba ya simu ya ofisi, vyombo vya habari na pale tunapokwenda kuhamasisha wananchi kuchangia damu. Hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali ndugu wa wagonjwa au wagonjwa wenyewe hawatoi taarifa kwa uongozi wa vituo hivyo vya tiba. Hali hii inapelekea kutokuwa na ushahidi wa kutosha kuwadhibiti na kuwachukulia hatua kali watumishi walio na tabia hii. Jambo hili la uuzwaji wa damu katika vituo kwa ujumla wake linawakatisha tamaa hata wanaochangia damu kwa hiari.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa tu mahitaji ya damu Kitaifa ni wastani wa chupa 400,000 hadi 450,000 kwa mwaka. Kwa sasa mpango unakusanya wastani wa chupa 120,000 sawa na 26%. Hii inaonesha kwamba, bado uwezo wa ukusanyaji wa damu mionganoni mwa wanaochangia damu kwa hiari haukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, inawataka Wakuu wa Vituo vya Tiba kudhibiti vitendo hivi vinavyofanywa na baadhi ya watumishi katika hospitali zetu nchini. Hatua mbalimbali zimekuwa zinachukuliwa kwa lengo la kukabiliana na tatizo hili kama ifuatavyo:-

- (i) Kuelimisha wananchi na watumishi wa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]*

Hospitali kuptitia vyombo vya habari kama magazeti na *television* kuwa huduma ya damu inapaswa kutolewa bila malipo.

(ii) Kubandika mabango yenyе ujumbe Damu Haiuzwi kwenye mifuko ya kutunzia damu yaani *blood bags* na katika Hospitali zote nchini na kutoa namba ya simu kwa malalamiko.

(iii) Kuendelea kubuni na kutekeleza mikakati yenyе lengo la kuongeza ukusanyaji wa damu nchini kadiri ya uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwataka wananchi wanaofanya vitendo hivi kuacha mara moja tabia hii, mtumishi atakayebainika kuza damu atachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa kanuni za kudumu za utumishi. Aidha, nitoe rai kwa wananchi wote wanaouziwa damu watoe taarifa kwa Wakuu wa Vituo vya Tiba husika au kituo cha damu salama kilicho karibu.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, Viongozi wa Serikali, Vyama vya Siasa, Dini, Taasisi, Makampuni na wananchi wote kushirikiana na mpango wa damu salama kuhamasisha juu ya kuchangia damu kwa hiari ili nchi iwe na akiba ya damu ya kutosha.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini napenda kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Katika jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri kasema damu inayopatikana ni kidogo na haikidhi mahitaji. Je, Serikali inajipanga vipi ili kuongeza vituo katika Mikoa yote ya Tanzania na kuongeza wafanyakazi, magari ya kufuatilia mpaka vijiji ili damu nyingi ipatikane ya kuweza kukidhi mahitaji? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

wa Jamii naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tuna kanda saba na tuna vituo vya Mikoa katika kuongeza uwezo wetu wa kukusanya damu. Tatizo tunalolizungumzia hapo ni watu kujitolea, kwenda katika vituo au pale magari na wafanyakazi katika mpango wa damu salama wanapofika katika vijiji vyetu na katika maeneo yetu, basi wananchi kujitolea katika kuchangia damu. Hilo ndiyo tatizo ambalo lipo, lakini hivi vituo tukiviongeza gharama za uendeshaji zinakuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika tafsiri hiyo, bado tunaendelea kuwasihhi wananchi wao wajitokeze pale ambako wataalam wetu wa Vituo vya Mpango wa Damu Salama wanapofika katika maeneo yao *either* kazini, mashuleni, kwenye vyuo ili waweze kuchangia damu na kuwa na uwezo mkubwa wa kupata damu ambayo ni salama kwa matumizi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumezidisha muda wa kujibu maswali, lakini tulikuwa na suala kubwa hili la Afrika Mashariki.

Kwanza, niwatambue wageni tulionao; kwanza kabisa, mnafahamu kwamba, wenzetu wa Kenya walishakuwa wamefanya uchaguzi wao. Katika uchaguzi wao wameweza kuwa na nyumba mbili za Bunge; yaani kuna Bunge halafu kuna *Senate*, lakini pia wameweza kuunda kitu kinaitwa *Counties*, *Counties* ziko 47.

Kwa hiyo, leo tumepata bahati ya kutembelewa na *Countymojawapo* na tuna *Countynyingine* itakuja. Kwa hiyo, tuna wageni wetu sita kutoka *County* ya Makueni ya nchi ya Kenya ambao wapo kwa ziara ya mafunzo hapa Bungeni.

Napenda niwatambue Waheshimiwa hawa; yupo Mheshimiwa Francis Mutungi, yeye ni Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani, wenzake akina Tundu Lissu hao.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKAJ]

Pia yupo Mheshimiwa Jonathan Mtuwai, Mwenyekiti wa Kamati ya PAC. Yupo Mheshimiwa Joseph Musya, Makamu Mwenyekiti Kamati ya Fedha. Yupo Mheshimiwa Mtunda Mwangangi, Makamu Mwenyekiti Kamati ya Kilimo. Yupo Mheshimiwa Magdalena Murwa, Mbunge wa kuteuliwa na yupo Mr. Robert Musyoka, Naibu Katibu wa Bunge. Ahsante. (*Makof!*)

Tunaamini kabisa mtapata kuonana na Kamati zinazohusika, mkawea kubadilishana uzoefu na kujifunza ambapo Kamati zetu zitafanya kazi na nyinyi, karibuni sana. Kwa hiyo, tunategemea na *county* nyingine itakuja baada ya hii kuondoka.

Pia tuna Katibu Mtendaji wa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ambaye ameambatana na wataalam wake ndugu Phillipo Isdory Mpango.

Kuna wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo; wako wanafunzi 50 na Walimu saba kutoka shule ya Sekondari ya Balaa Jijini Arusha, wako wapi hawa wanafunzi? Ahsante na karibuni.

Tuna wanamichezo 13 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Arusha wakiongozwa na ndugu Sophia Shoka, Afisa Ushirika wa Wilaya, naomba wasimame wanamichezo hao.

Halafu tuna wanamichezo wengine wanatoka Halmashauri ya Maswa, sijui wako wapi na wenyewe. Ahsanteni sana na karibuni na nawatakia michezo mema huko mnakofanya.

Tuna wanamichezo 25 kutoka Halmashauri ya Wilaya Mbarali, wako wapi hawa wa Mbarali. Ahsanteni sana.

Vile vile tuna wafugaji 60 kutoka maeneo mbalimbali ya wafugaji Tanzania wako wapi na wenyewe. Ahsanteni na karibuni sana.

Tuna wageni watano kutoka Tarime wakiongozwa na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKA]

Mwenyekiti wa CCM, Kata ya Nyasincha, wako wapi hawa? Ahsanteni sana na karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Hassan Mgimwa, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo tarehe 30 saa tano asubuhi, kutakuwa na kikao cha Kamati. Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wa Msekwa B.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba watakuwa na kikao katika ukumbi wa Msekwa C. Wale Msekwa B na hawa Msekwa C.

Halafu nina taarifa pia, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana watakuwa na kikao, ukumbi namba 231, ghorofa ya pili ya utawala.

Halafu nina tangazo la kutoka Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa David Silinde, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA kuwa, leo saa saba mchana watakuwa na mukutano wao katika chumba namba 227.

Halafu na Ofisi kwa niaba ya Katibu wa Bunge inawatangazia kwamba Wabunge waende mapokezi, Jengo la Utawala kwa ajili ya kuchukua fomu zao za maadili za tamko la mali na madeni, maafisa wa Maadili wapo katika eneo hilo kuanzia jana.

Mfanye hivyo, mwaka jana kuna Wabunge kumi na, hawakujaza na kama wengine mtakuwa ni wagonjwa, mnatoa taarifa kwa Spika kwamba nilichelewa kuleta fomu kwa sababu nilikuwa na dharura ya ugonjwa. Utapelekwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKA]

Mahakamani ndugu, maana yake huo ndiyo utaratibu. Nawaomba sana na mkijaza sasa, kabla ya kuondoka itakuwa salama kwenu.

Tunaendelea Katibu! Mheshimiwa Juma Nkumba nini tena!

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nasimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 55(3)(e), nanukuu; "Hoja zifuatazo zinaweza kutolewa bila taarifa; (e) kuahirishwa shughuli za Bunge zinazoendelea ili kujadili jambo la dharura.

Mheshimiwa Spika, ikisomwa pamoja na Kanuni ya 47(1), (2) na (3), kifungu hicho hicho cha 47:-

(1) Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge ye yote anaweza kutoa hoja kuwa, shughuli za Bunge kama zinavyoonesha kwenye orodha ya shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.

(2) Hoja ya namna hiyo itakuwa ni maalum na inaweza kutolewa wakati wowote hata kama majadiliano yatakuwa yanaendelea.

(3) Hoja itatolewa na Mbunge kwa kusimama mahali pake na kuomba idhini ya Spika kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge kwa madhumuni ya kujadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma."

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa; moja, mgogoro kati ya wafugaji na wakulima, wafugaji na hifadhi, wafugaji na wawekezaji, wafugaji na watumiaji ardhi wengine, tatizo limekuwa kubwa na kwa sasa linatishia utulivu na amani ya jamii katika maeneo mengi nchini. (*Makofii*)

Mbili, kufuatia migogoro hii, athari nyingi zimekuwepo za uvunjifu wa amani, uharibifu wa mali na kwa nyakati kadhaa watu wamepoteza maisha.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. J. NKUMBA]

Tatu, migogoro hii imesababisha uhasama mkubwa kati ya wanajamii hasa kati ya wafugaji na wakulima, hususan katika Mikoa ya Morogoro, Pwani, Tanga na Mbeya. (*Makof*)

Nne, kumekuwepo na *operation* mbalimbali nchini zilizosababisha adha na hasara mbalimbali kwa wafugaji na wakulima, zikiwemo za kupoteza mifugo na mazao, kusababishiwa ulemavu, umaskini na mara nyingine kupoteza maisha. (*Makofi*)

Tano, itakumbukwa kwamba mnamo Aprili, 2009, kufuatia malalamiko ya wafugaji pamoja na taarifa za Tume mbalimbali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI alitoa kauli ya Serikali iliyositisha zoezi la kuwaondoa wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini, hadi hapo Serikali itakapokuwa imezifanyia kazi kasoro zilizojitokeza.

Sita, hata hivyo, kasoro zilizojitokeza mwaka 2009, bado nyingi hazikufanyiwa kazi na Serikali na *operation* ya kuwaondoa wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini imeanza tena na inaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizi, naomba Bunge, lako Tukufu sasa likubali kuharisha shughuli za Bunge zilizopangwa kwa siku ya leo, ili Bunge liweze kujadili taarifa hii muhimu kwa maslahi ya umma ili kulinda amani na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lugola! Kaeni, kwani huwa wanaunga mkono hoja hii? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Lugola wewe ultaka kusema nini? Kama unarudia hiyo, basi naomba usitumie muda, sijafanya maamuzi juu ya hoja hiyo. Sema wewe ulisimama mwanzo, ulikuwa unataka kusemaje?

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kutoa hoja.

**SPIKA:** Hiyo hiyo? Kama ni hiyo hiyo naomba ukae kidogo.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Siyo hiyo.

**WABUNGE WENGINE:** Siyo hiyo.

**SPIKA:** Kama siyo hiyo, eleza.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba...

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walicheka kwa kuwa  
Mheshimiwa Mbunge alikuwa amebeba mzigo  
wa vitabu vingi mkononi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge mzigo mwiningine uweke chini kwanza. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie Kanuni ya 47 na 48; ambapo Kanuni ya 47 inasema: "Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge yejote anaweza kutoa hoja kuwa, shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye orodha za shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma." Inaendelea na Kanuni ya 48.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunavyozungumza hapa Bungeni, kuna ng'ombe Kaliua, ambao wameanza kuchambuliwa ng'ombe 12 kwa ajili ya kupigwa risasi ili kuwashinikiza wafugaji waweze kuwalipa fedha, kuanzia 180,000 mpaka 200,000 kwa ng'ombe mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza, makabrasha haya yamejaa picha za ng'ombe ambao wamepigwa risasi juzi, zimejaa picha za ng'ombe ambao wamechinjwa na wanaoendesha *operation* wakafanya vitoweo, zimejaa picha za ng'ombe 151 waliotumbukizwa kwenye Mto Rubama kando kando ya hifadhi ya Serengeti. (*Makofi*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A.K.N. LUGOLA]

Mheshimiwa Spika, tusipojadili jambo hili, utaendeshwa mnada wa uonevu wa kuwafanya ng'ombe hawa 4,000 waliochukuliwa kwa nguvu, kwa mtutu wa bunduki, waweze kuuzwa. Tusipojadili jambo hili kwa sasa, wale ng'ombe waliotumbukizwa kwenye Mto wa Rubama na Kampuni ya mwekezaji ya Gurumeti, kunaweza kukatokea machafuko makubwa kando kando ya mbuga ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo ameelezwa jambo hili na wafugaji kwa muda mrefu, lakini hachukui hatua na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ameelezwa mambo haya kwa muda mrefu, hachukui hatua, ni muda muafaka sasa Bunge hili kujadili kwa upana likiwa na ushahidi na vielelezo ili tuweze kuhakikisha wale ng'ombe hawatauzwa na wananchi hawatanyanyaswa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Hoja hizi huwa haziungwi mkono, naomba mkae, huwa haziungwi mkono hoja za namna hii.

Waheshimiwa Wabunge, hoja zote mbili zilizotolewa ni hoja nzito na huwezi ukadharau. Lakini kama sisi ni Wabunge ambao tunatakiwa kuwa na matokeo ya majadiliano yetu, huu ni upande mmoja. Kwa hiyo, kwa sasa naagiza Serikali ikayafanyie kazi na kabla hatujaondoka hapa watatoa maelezo ndiyo tutakapojadili.

Semeni mnayotaka, nimeshafanya maamuzi. Tunaendelea, Katibu!

(*Hapa Wabunge fulani waliguna kuonesha kutoridhishwa na maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Spika*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, unataka kusemaj?e?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nataka kukuhakikishia maagizo yako tutatekeleza, lakini nataka kutoa tahadhari, pamoja na zoezi hilo linaloendelea kuna utapeli, kuna watu wameingia na utapeli hata hapa Dodoma, watu wanachangisha wafugaji sh. 50,000/= kwa kisingizio kwamba wanakwenda kwenye mkutano wa Waziri Mkuu na ili wamwone Waziri Mkuu, lazima wachangie sh. 50,000/=.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwatangazia wafugaji nchi nzima, hao wanaochangisha fedha wakijifanya ni Asasi za kuwatetea ni matapeli. Watetezi wa wafugaji ni Wabunge waliotoa kauli na taarifa itatolewa Bungeni, itajadiliwa kupitia Kamati na Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kutoa tahadhari hiyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimefanya maamuzi kwamba, hili suala..

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa!

Naomba msiseme aaaaa; hiyo siyo tabia njema! Ninachosema ni kwamba, yule aliyebeba furushi la vitabu na Mheshimiwa Nkumba naye alikuwa na maeleo ya kutosha, wengine wote tunasoma kwenye vyombo vya habari, atajibu nani, nitamwambia tunataka Serikali ijiandae, ilete hapa habari na sisi tujadili.

Nimefanya uamuzi; Katibu, tunaendelea!

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa  
Taifa kwa mwaka 2014/2015**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wale wa Katiba na Sheria, naona ukumbi umebadilika, watakutana katika chumba Na. 219.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKA]

Sasa Waheshimiwa Wabunge, leo tunatumia Kanuni ya 94(1), kwamba katika Mkutano wake wa mwezi Oktoba, ndiyo huu Novemba, kwa kila mwaka, Bunge kwa siku zisizopungua tano, litakaa kama Kamati ya Mpango ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba kwa kujadili na kuishauri Serikali kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata. Naomba utulivu Waheshimiwa Wabunge.

Katika mkutano huo, Bunge pamoja na mambo mengine, itafanya shughuli zifuatazo:-

- (1) Kupokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mwongozo wa kuandaa mpango wa bajeti ya Serikali;
- (2) Kupokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali; na
- (3) Kupokea na kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mapendekezo ya mpango wa Serikali na vipaumbele kuhusu mpango huu.

Kwa hiyo, katika kujadili hii; ndiyo mwanzo wa mzunguko wetu wa bajeti, mwaka huu ndiyo tunaanza vizuri. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba, vile vitabu vimegawiwa, mmesoma vizuri na ni vizuri mkasoma kwa sababu utakapofika wakati wa bajeti kama kutakuwa na *diversions* yoyote, itakuwa ndani ya mpango ambao mtakuwa mmeupitisha hapa. Kwa hiyo, msifanye kama ni kikao cha kawaida tu, hiki ni kikao muhimu sana katika mfumo mzima wa bajeti yetu ya Serikali.

Kwa hiyo, naomba kabisa Waheshimiwa mtoe nafasi ya kutosha, msome, muweze kuona kuwa, mambo gani mnafikiria katika mwaka mwingine wa fedha yapewe kipaumbele zaidi, kuliko tuanze bajeti yenyewe, tunaanza kukimbizana na vipaumbele wakati bajeti imeshatolewa, inakuwa vigumu, kwa hiyo, tunaanza vizuri mwaka huu. Sasa namwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango ili iweze kupokea na kujadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015 ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano, yaani 2011/2012 hadi 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye ndiye Mwenyekiti wa Tume ya Mipango kwa maelekezo yake ambayo yametuwezesha kutekeleza majukumu ya usimamizi na uratibu wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa ya kuwasilisha mapendekezo haya. Vile vile nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti na wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri. Tume ya Mipango itaendelea kuzingatia maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa kwa ushirikiano wake wakati wa maandalizi ya mapendekezo haya. Aidha, nawashukuru Dkt. Philipo Mpango, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango, pamoja na wataalam wake na Dkt. Silvanus Lekwilile, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, pamoja na wataalam wake kwa ushirikiano katika kufanikisha uandaaji wa mapendekezo ninayoyawasilisha.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2014/2015 ni ya nne katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 hadi 2015/2016 na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2026. Hivyo, mapendekezo haya yamezingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano vifuatavyo:-

- (i) Miundombinu;
- (ii) Kilimo;
- (iii) Viwanda vinavyotumia malighafi za ndani na kuongeza thamani;
- (iv) Maendeleo ya Rasilimali watu; na
- (v) Uendelezaji wa huduma za utalii, biashara na fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kwa kifupi utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2012/2013, hususan kwa maeneo ya Kitaifa na ya kimkakati. Kimsingi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2012/2013, mafanikio yamepatikana katika sekta mbalimbali, licha ya kuwepo kwa changamoto kadhaa.

Mheshimiwa Spika, hasa nizungumzie juu ya mwenendo wa uchumi kwa mwaka 2013, taarifa za awali zinaonesha kuwa pato halisi la Taifa lilikuwa kwa kiwango cha asilimia saba katika nusu ya kwanza ya mwaka 2013 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji ni pamoja na usafiri na mawasiliano asilimia 18.4; fedha asilimia 14.6 na ujenzi asilimia 8.7.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi tisa iliyopita, kasi ya mfumko wa bei imekuwa ikiendelea kupungua kutoka asilimia 10.9 Januari, 2013 hadi asilimia 6.1 Septemba, 2013. Kupungua kwa kasi ya upandaji bei, kumetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula, hususan mpunga, mahindi na mtama.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*

Mheshimiwa Spika, hali ya mwenendo wa uchumi wa dunia, siyo ya kuridhisha, kutokana na kupungua kwa mahitaji ya ongezeko dogo la ukuaji la uchumi kwa nchi zinazobukia kwa uchumi. Kudhoofika kwa shughuli za kiuchumi na biashara ya kifedha katika nchi za Ulaya kulikosababishwa na mgogoro wa madeni (*Euro debt crisis*) na kupungua kwa kiwango cha ukuaji kwa nchi ya Marekani. Kulingana na taarifa la Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) ya Julai, 2013, pato la dunia linatarajiwa kukua kwa asilimia 3.1 mwaka 2013 sawa na ilivyokuwa katika mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nchi za Afrika, Kusini mwa janga la Sahara, ukuaji wa pato unaonesha kuanza kuimarika na kufikia ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2012. Ukuaji wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki nao umeonesha kuimarika kwa nchi zote wanachama kwa kuwa na viwango vinavyoongezeka isipokuwa kwa nchi ya Rwanda. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi hizo kwa mwaka 2012 ikilinganishwa na mwaka 2013, inatarajiwa kuongezeka kama ifuatavyo:-

Tanzania kutoka asilimia 6.9 hadi asilimia 7.0; Kenya kutoka asilimia 4.7 hadi 5.9; Uganda kutoka asilimia 2.6 hadi asilimia 4.8 na Burundi kutoka asilimia 4.0 hadi asilimia 4.5. Kwa upande wa Rwanda kasi ya ukuaji inatarajiwa kupungua kidogo, toka asilimia 7.7 mwaka 2012 hadi asilimia 7.6 mwaka huu 2013.

Mheshimiwa Spika, sensa ya watu na makazi iliyofanyika 2012, ilioonesha idadi ya watu Tanzania Bara ilikuwa milioni 43.6 ikilinganishwa na makadirio ya idadi ya watu milioni 43.2 mwaka 2011. Hivyo, pato la wastani la kila mtu liliongezeka kwa asilimia 17.9 na kuwa dola za Kimarekani 647, sawa na sh. 1,025,038 mwaka 2012, ikilinganishwa na dola za Kimarekani 550, sawa na sh. 869,436.3 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, aidha, idadi ya watu Tanzania inatarajiwa kufikia 63 milioni na kulingana na dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, pato la wastani la kila mtu linatakiwa liwe

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]

limefikia dola za Kimarekani 3000, sawa na sh. 4,436,000 ifikapo mwaka 2025. Hivyo, kufikia pato hilo la wastani kwa kila mtu na kufikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati dola za Kimarekani 1,036,000 hadi 4,085, sawa na takriban sh. 1,670,032 hadi sh. 6,536,632 ni dhahiri tunahitaji msukumo mkubwa zaidi katika ukuaji wa sekta zote, hususan sekta ya kilimo yenyeye kuajiri watu wengi.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/2013. Naomba nieleze kwa kifupi, hali ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2012/2013 na robo ya kwanza ya mwaka 2013/2014 kwa baadhi ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la reli, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na; kutandikwa kwa reli yenyeye urefu wa kilomita 42 na kufikisha jumla ya kilomita 136 zilizotandikwa ikilinganishwa na kilomita 197 za reli yenyeye uzito wa ratili 80 kwa *yard* zilizokusudiwa katika reli ya kati; kuendelea kwa ujenzi wa madaraja matatu ya reli; mawili kati ya Kilosa na Gulwe na moja kati ya Bahi na Kintinku; kukamilika kwa matengenezo katika maeneo 13 ya *station* ya Godegode na Gulwe na maeneo 32 yaliyopo kati ya Stesheni ya Kilosa na Gulwe na kufanya malipo ya awali kwa ajili ya ununuzi wa mabehewa 34 ya *break*, mabehewa 22 ya abiria na *engine* mpya 13 kwa ajili ya reli ya kati.

Mheshimiwa Spika, aidha, matayarisho ya kujenga upya reli ya kati yanaendelea ambapo upembusi yakinifu umekamilika. Serikali iko katika hatua za kukamilisha upembusi wa kina na imeanza kumtafuta mwekezaji wa kujenga upya reli hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa reli ya kikanda, hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali – Keza Msongati kilomita 1,464 ni kuendelea na kazi ya kukamilisha taarifa ya mwisho ya upembusi wa kina inayofanywa na Mshauri Mwelekezi Kampuni ya CANARA/L kutoka Canada.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*

Aidha, kuhusu reli ya Tanga – Arusha - Musoma, hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ulipaji wa fidia, kwa wakazi la eneo la Mwambani, Tanga ili kupisha ujenzi wa sehemu ya kupanga mabehewa na kukamilika kwa taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa reli.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha usafiri wa reli Jijini Dar es salaam, kazi zilizofanyika katika mwaka 2012/2013 ni kukarabati, kuimarisha na kupanua tuta la njia, kati ya eneo la Mnyamani na Mwananchi. Kufanya matengenezo ya makutano ya njia ya reli ya barabara pamoja na kuweka alama za usalama. Ujenzi wa sehemu ya kupanda na kushuka abiria, ujenzi wa sehemu ya kupishania treni na kuweka vizuizi vya magari sehemu ambazo treni inakatisha barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ujenzi wa kilomita 558.92 za barabara kuu kwa kiwango cha lami ikilinganishwa na lengo la kilomita 414 na ukarabati wa kilomita 257.53 za barabara kuu kwa kiwango cha lami, umekamilika ikilinganisha na lengo la kukarabati kilomita 135.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madaraja, mafanikio ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa madaraja ya Ruhekei, Mbinga; Nanganga, Tunduru na kuendelea na ujenzi wa madaraja ya Nangoo, Mtwara; Maligisu, Mwanza; Malagarasi, Kigoma na Mbutu, Igunga, ambao uko katika hatua za mwisho kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa daraja la Kigamboni, daraja la muda limekamilika na kazi ya ujenzi wa daraja imeanza ambapo nguzo 150 kati ya 202 zimekamilika na kusafishwa kwa eneo la barabara zinazoingia katika daraja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vivuko, kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilika kwa ukarabati wa kivuko cha MV Chato, Kagera na ununuzi wa kivuko kipyga cha llagala kwa ajili ya Kigoma.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bandari, mafanikio yaliyopatikana, ni pamoja na kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa Ghati namba moja hadi saba katika Bandari ya Dar es Saalam; kukamilika kwa upembuzi yakinifu na kusainiwa kwa makubaliano ya awali kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya watu wa China kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Mbegani, Bagamoyo; kukamilika kwa upembuzi yakinifu na kutangaza mradi wa bandari ya Mwambani, Tanga, ili kupata wawekezaji na kuendeleza Bandari kwa ubia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari kavu ya Kisarawe. Hatua iliyofikia ni kukamilika kwa mchakato wa zabuni kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa awamu ya pili na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe kukamilisha taratibu za kupata kibali kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi cha kutenga eneo la hekari 1,760 badala ya hekari 1,468 za awali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maji safi na maji taka. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kusimikwa kwa mitambo ya umeme na mashine za kusukuma na kusafisha maji katika mradi wa Ruvu Chini na kutandazwa kwa mabomba katika eneo la kilomita 17.1 kati ya kilometa 55 zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa maji Ruvu Juu; ripoti ya usanifu kwa ajili ya kutandaza bomba kuu, kutoka Mtamboni hadi Kibamba na ujenzi wa tanki jipya eneo la Kibamba umekamilika Novemba 2012 na kukamilika kwa taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi Agosti, 2013. Aidha, idadi ya wakazi wa vijijini wanaopata maji safi imeongezeka kutoka watumiaji milioni 20.6 mwaka 2011 hadi milioni 22.29 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Nishati, kazi zilizofanyika katika mradi wa bomba la gesi Mtwara - Dar es Salaam, ni kukamilisha kwa ulipaji wa fidia ya jumla ya shilingi bilioni 6.86 kwa wananchi; kupatikana kwa cheti cha Mazingira tangu mwezi Aprili, 2012; kuwasili kwa mabomba

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*  
ya gesi elfu 20,491 yenye uwezo wa kujenga kilomita 243.86 na kutandazwa kwa mabomba yenye urefu wa kilomita 108 ambapo mabomba yenye urefu wa kilomita 25.8 yameunganishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mradi wa mtambo wa kufua umeme Kinyerezi one, megawatt 150, hatua iliyofikiwa ni kuingia mkataba kati ya Serikali na Mkandarasi kutoka Norway na Mshauri wa mradi kutoka Ujerumani.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuboreshwa kwa miundombinu ya usambazaji wa umeme vijijiini, Jijini Dar es Salaam katika vituo vya Buguruni, katikati ya Jiji, Kariakoo, Kipawa, Mbagala, Mbezi, Oysterbay na Ubungo. Kuungwa kwa *transformer* zenye uwezo wa MVA 15 kwa kila kituo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika miradi ya umeme vijijiini, ni pamoja na kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya za Namtumbo, Nyangh'wale na Nkasi. Kupata Mkandarasi wa kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe na Mbongwe. Kukamilisha tathmini ya zabuni ya kuwapata Wakandarasi kutekeleza awamu ya pili ya mpango kabambe wa usambazaji wa umeme vijijiini.

Mheshimiwa Spika, kukamilisha ujenzi wa kilomita 24.78 kati ya 47.53 za njia ya usambazaji umeme na kufungwa *transformer* saba kati 24 Mkoani Mtwara na kuunganisha umeme kwa wateja 277; kukamilisha ujenzi wa jumla ya kilomita 11.28, kati ya 28.20 za njia za umeme wa Msongo wa KV 33 na KV 11 katika Mkoa wa Lindi. Aidha, ujenzi wa kilomita 59.5, kati ya 72 za njia ya umeme ya msongo wa KV 0.4 Mkoani Lindi umekamilika na *transformer* tano kati ya ishirini tano zimefungwa na wateja 132 wameunganishwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo, mafanikio yaliyopatikana ni kutambua na kuhakiki mashamba yenye ukubwa wa hekta 334,538 kwa ajili ya uwekezaji katika

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]

Mabonde Makuu ya Wami, Ruvu, Rufiji, Kagera, Kilombero na Malagarasi; ambapo hekta 85,000 zimepata hati miliki. Aidha, kazi ya kupima maeneo inaendelea katika Bonde la Rufiji, Mkongo *Block*, ambapo jumla ya hekta 5,551 zimepimwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya ukanda wa *SAGCOT*, hatua iliyofikia ni kukamilika kwa asilimia 40 ya ujenzi wa banio katika mradi wa umwagiliaji Itete, Morogoro, hekta 1,000. Aidha, katika miradi ya umwagiliaji ya Mpanga - Ngalimila, Morogoro hekta 31,500; Sonjo, Kilombero, hekta 1,340 na Lupiro, Morogoro, hekta 4,000. Kazi ya upembuzi yakini imekamilika na kazi ya usanifu na kuandaa michoro ya *scheme* inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi wa maghala ya kuhifadhi chakula; ujenzi wa ghala katika Kanda ya Songea lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000, upo katika hatua za mwisho. Aidha, michoro kwa ajili ya ujenzi wa ghala la Mbozi na ghala lingine Songea imekamilika.

Mheshimiwa Spika, vile vile majadiliano kati ya Serikali na benki ya *Exim* ya China, yameanza kwa ajili ya kupata mkopo wa kujenga vihenge vya kisasa (*silos*) vyenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 160,000 katika Kanda za Kipawa, Makambako, Sumbawanga, Songea, Shinyanga, Arusha na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya viwanda, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilisha uchorongaji wa mashimo 40 yenye jumla ya urefu wa mita 8,000 kwa ajili ya kuhakiki wingi wa chuma katika eneo la Liganga na kukamilisha tathmini ya eneo la Kurasini, hekari 60 lenye thamani ya shilingi bilioni 94.1 Mei, 2013 na kulipa fidia hekari 19.6 kwa kaya 276.

Mheshimiwa Spika, aidha, ulipaji wa fidia wa kiasi cha shilingi bilioni 16.9 kwa eneo la Bagamoyo ulifanyika mwaka 2011/2012 na mwaka 2012/2013 kwa hekta 1,600 kati ya 5,700 zilizofanyiwa tathmini ya shilingi bilioni 58.8 mwaka 2011.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kigoma malipo ya shilingi bilioni 1.5 kwa hekta 3,000, kati ya hekta 20,000, yalifanyika mwaka 2011/2012. Mchakato wa kupata fedha za kumalizia kulipa fidia katika eneo la mradi Bagamoyo na Kigoma unaendelea kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Kiwanda cha Viuadudu Kibaha, hatua iliyofikiwa ni ujenzi wa majengo mawili ya kiwanda, usanifu wa kina na kuanza ufungaji wa mitambo. Kiwanda hiki tayari kimezinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Oktoba, 2013.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa magadi soda, bonde la Engaruka, Arusha; kazi ya kuchoronga mashimo 12 kwa ajili kuhakiki wingi na ubora wa magadi imekamilika; ambapo imebainika kuwa eneo la Engaruka, lina magadi yenye mita za ujazo bilioni 4.68. Kati ya kiasi ambacho ni kikubwa kutosheleza uchimbaji magadi soda kwa zaidi ya miaka 400.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa magadi soda utasaidia katika viwanda, madawa sabuni, nguo, rangi na viwanda vya kuchakata chuma. Kwa sasa Serikali inaendelea na tafiti za kubaini tabia ya ndege aina ya *flamingo* ili kuendana na matakwa ya kimazingira. Ujenzi wa miundombinu na kutafiti teknolojia bora za uchimbaji wa magadi soda.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa rasilimali watu, mafanikio yaliyopatikana hadi Juni, ni pamoja na wataalam wapatao 374 wameendelea kugharamiwa na Serikali katika nyanja maalum za gesi, mafuta, chuma, urani na madini mengine na nyanja nyiningine muhimu kwa ajili ya mendeleo ya Taifa. Kati ya hao, 261 ni wa shahada ya uzamili na 113 shahada ya uzamivu na wanasoma katika Vyuo Vikuu sita vya umma ambavyo ni Dar es Salaam, Sokoine, Muhimbili, Mzumbe, Ardhi na Nelson Mandela.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kugharamia

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*

miradi ya utafiti hapa nchini ikiwa ni pamoja na ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya utafiti na kutengeneza mitambo na vipuri. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilisha ukarabati wa matrekti 11 kati ya 14 umefanywa na CAMARTEC. Kukamilisha matengenezo ya vipuri vya treni, reli na trekta ndogo za mkono *power tiller* yaliyofanywa na taasisi ya *Tanzania Automotive Technology Centre*, iliyopo Kibaha na kuendelea na ubunifu wa uendelezaji wa mashine mbalimbali kwa ajili ya usindikaji mazao.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la huduma za fedha, mafanikio yaliyopatikana ni kuundwa kwa Bodi ya Wakurugenzi na kuanza kuajiri maafisa waandamizi na kuongeza mtaji wa Benki ya Kilimo kufikia shilingi bilioni 90 na kuongeza mtaji wa shilingi bilioni 50 kwa Benki ya Rasilimali Tanzania na kufikia shilingi bilioni 142 na kuongeza mtaji wa shillingi billioni 1.1 kwa Benki ya Wanawake Tanzania na kufikia shilingi bilioni 8.2.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu malengo na hatua za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/2013 na robo ya kwanza kwa mwaka 2013/2014, kwa baadhi ya maeneo yakijumuisha mafanikio yaliyopatikana wa upande wa sekta binafsi yako katika kitabu cha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2014/2015, Sura ya Pili.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2012/2013, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kumekuwepo na changamoto kadhaa pamoja na ufinyu wa rasilimali fedha hususan upatikanaji wa mikopo na kugharamia miradi. Taratibu ya tathmini ya fidia na ulipaji wa fidia kwa wakati, upatikanaji wa ardhi iliyopimwa kwa ajili ya uwekezaji, upatikanaji wa huduma wezeshi hususan barabara, maji na umeme katika maeneo ya miradi na madeni ya miaka iliyopita kwa baadhi ya miradi.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa kukabiliana na changamoto hizo ni pamoja na kuendelea kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato, kuandaa mwongozo wa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*  
andiko la miradi kwa ajili ya kuwezesha Wizara kuandaa  
miradi inayokidhi vigezo vya mikopo. Kuimarisha mfumo wa  
ufuatilaji na tathmini ya miradi chini ya *President's Delivery  
Bureau* na kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na  
uwekezaji ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika  
utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie maeneo  
muhimu ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa  
mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali  
itaendelea kuelekeza fedha za maendeleo kwenye miradi  
michache ya Kitaifa, ya kimkakati na yenye kuleta matokeo  
makubwa ili kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi na hivyo  
kuongeza ajira; uzalishaji hususan katika sekta ya kilimo kwa  
lengo la kuendelea kudhibiti mfumko wa bei; kuimarisha  
ushindani wa kiuchumi; kuongeza mauzo nje ya nchi na  
kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia fursa za kikanda  
na dunia, jitihada za ziada zinahitajika ili kuhakikisha kuwa  
zinaleta matokeo chanya na kwa haraka. Hivyo,  
inapendekezwa kuwa, masuala muhimu yafuatayo  
yazingatiwe katika kuandaa Mpango wa Maendeleo wa  
Taifa kwa mwaka unaokuja:-

(1) Kudumisha amani na utawala bora kama  
msingi muhimu wa kuwezesha uzalishaji mali, uwekezaji, ukuaji  
wa uchumi na maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(2) Ukuaji uchumi unakuwa shirikishi ili kuondoa  
tofauti za kipato na kupunguza umaskini;

(3) Kuongeza tija katika kilimo hususan mazao  
yenye thamani kubwa (*high value crops*);

(4) Ubunifu wa maendeleo na teknolojia,  
kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*

(5) Masoko kwa bidhaa za ndani na vyanzo vipyta vya uwekezaji katika uchumi wa kikanda na dunia vinatumika vizuri;

(6) Kujenga uwezo wa kuhimili changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi;

(7) Kujenga uwezo wa kutumia vizuri mapato yanayotokana na gesi asilia na madini mengine yanayoendelea kugunduliwa;

(8) Kutumia fursa ya ongezeko la watu nchini, kuleta manufaa ya kiuchumi kwa kupunguza kiwango cha utegemezi, yaani uwiano kati ya watoto amba ni tegemezi na idadi ya watu wanaofanya kazi; na

(9) Kutumia fursa ya ongezeko kubwa la watu mijini kwa kuifanya miji kuwa vituo endelevu vya ubunifu na ukuaji uchumi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2014/2015. Kwa kuzingatia masuala muhimu niliyoyaanisha, sasa naomba nieleze kwa ufupi maeneo ya Kitaifa ya kimkakati, ya kipaumbele katika Mpango wa Taifa wa mwaka 2014/2015. Maeneo ya kipaumbele yanajumuisha miradi iliyoibuliwa katika *program* ya matokeo makubwa sasa na maeneo ya Kitaifa ya kimkakati ya *program* ya matokeo makubwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miundombinu, maeneo yanayopewa kipaumbele ni nishati. Kuendelea kutekeleza miradi iliyoibuliwa chini ya matokeo makubwa sasa, ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam na kuendelea kuboresha miundombinu ya ufuaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme mijini na vijijini. Aidha, Serikali itaendelea na uwekezaji katika vyanzo vingine vya nishati mbadala, jadifu na makaa ya mawe na kuweka mazingira wezeshi ili Taifa liweze kunufaika na rasilimali ya gesi asilia.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

Mheshimiwa Spika, barabara; kutengeneza miradi ya barabara ilioibuliwa katika *program* ya matokeo makubwa sasa, hususan ujenzi na ukarabati wa barabara zinazofungua maeneo yenye fursa ya kiuchumi na kuboresha na kusimamia viwango vya usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, reli; Serikali itaendelea kuimarisha reli ya Kati, hususan miradi ilioibuliwa katika *program* ya matokeo makubwa sasa ikiwa ni pamoja na ukarabati wa miundombinu ya reli, ikijumuisha majengo ya *station* na madaraja. Kuanzisha mpango wa biashara (*business plan*) na mfumo madhubuti wa ufuutiliaji wa mizigo na ukarabati wa ununuzi wa injini na mabehewa ya treni kwa ajili ya reli ya kati.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ni kuendelea kukamillisha upembuzi wa kina na kumpata mwekezaji wa kujenga upya reli ya kati kwa kiwango cha geji ya kisasa; Kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kutafuta wawekezaji katika miradi mipya ya reli.

Mheshimiwa Spika, kuboresha usafiri wa reli Jijini Dar es salaam na kuendelea kuvutia sekta binafsi, kuwekeza katika ujenzi wa reli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari; kujenga na kuboresha miundombinu ya bandari ilioainishwa katika *program* ya matokeo makubwa sasa hususan, kuboresha mfumo wa mawasiliano katika bandari ya Dar es salaam na kuboresha miundombinu ya reli iliyopo bandarani.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa bandari.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa anga; kuendelea kuboresha miundombinu ya usafiri wa anga ili kuongeza ufanisi na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege katika maeneo ya kimkakati.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*

Mheshimiwa Spika, maji safi na maji taka; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika program ya matokeo makubwa sasa, hususani kuimarisha na kuongeza miundombinu ya maji vijijini kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji safi na maji taka katika Jiji la Dar es Salaam na miji mingine nchini na kuboresha ukarabati na kuongeza miundombinu ya vyanzo vipyta.

Mheshimiwa Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, kuanzisha maeneo maalum ya TEHAMA, utekelezaji wa mradi wa Anwani za Makazi na Mishimbo ya Posta na kuhamasisha na kukuza tafiti za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Kilimo, maeneo yatakayopewa kipaumbele, ni kuendeleza miradi ya kilimo katika programu ya matokeo makubwa sasa, ikiwa ni pamoja na kuendeleza kilimo cha kisasa kwenye *schemes* za wakulima wadogo wa mpunga; kutafuta mashamba kwa ajili ya Wawekezaji wakubwa, na kuanzisha mfumo wa maghala ya masoko ya mazao (*collective warehouse based marketing system*)

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ni utekelezaji wa miradi ya miwa na mpunga katika maeneo ya Bonde la Wami, Ruvu, Kagera, Kilombero na Malagarasi. Utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji katika ukanda, *SAGCOT*; kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji; kuimarisha Vituo vya Tafiti za Kilimo, kuwezesha na kuimarisha ushirika nchini, na kuendelea na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia chakula.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Mifugo, maeneo yatakayopewa kipaumbele, ni kuendeleza na kuboresha miundombinu ya mifugo kama vile malisho, majosho na malambo; kujenga na kuimarisha vituo vya uhamilishaji, kuongeza thamani ya mazao ya mifugo na kuimarisha Vituo vya Tafiti za Mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uvuvi, maeneo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU])*  
ya kipaumbele, ni kuimarisha usimamizi katika eneo la Bahari Kuu ili kuongeza mapato; kuimarisha zana za ukaguzi na uvunaji wa samaki; kukuza huduma, miundombinu na uzalishaji wa samaki na kuimarisha vituo vya tafiti na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Viwanda, maeneo ya kipaumbele ni kuendelea kutambua na kutenga maeneo ya ardhi ya uwekezaji hususan katika maeneo maalum ya uwekezaji yaani EPZ na SEZ; ujenzi wa Kituo cha Biashara na Huduma, Kurasini; kuongeza kasi ya kuvutia Wawekezaji na kujenga mazingira wezeshi katika Sekta ya Viwanda; kujenga miundombinu muhimu katika kuendeleza mradi wa Chuma cha Liganga na mradi wa Magadi soda katika Bonde la Engaruka.

Mheshimiwa Spika, pia kuendeleza miradi ya kukuza ajira kwa vijana kwa kuimarisha Viwanda vidogo vidogo chini ya S/IDO; kukuza maendeleo ya Wajasiriamali wadogo na wakati na kuanzisha maeneo maalum ya Viwanda na uhaulishaji wa teknolojia ya uzalishaji wa matrekta na zana za kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika maendeleo ya Rasilimali watu maeneo ya kipaumbele, ni kuendelea na utekelezaji wa miradi ya elimu katika programu ya matokeo makubwa sasa, hususan mpango wa kuwezesha wanafunzi na Walimu kujifunza kwa Shule za Msingi na Sekondari; kuimarisha mfumo wa ruzuku na kuendesha shule na ujenzi wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine, ni kuendelea kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali hususan katika gesi na mafuta, chuma, urani, madini, umwagiliaji na maji na kuendeleza elimu ya ufundi stadi kwa kuongeza na kuboresha miundombinu na Mitaala katika Vyuo vya Ufundi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi; upanuzi wa Vyuo vya Ualimu hasa katika masomo ya Sayansi na Vituo vya Utafiti na kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi na kuwekeza katika maendeleo ya rasilimali watu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

### *[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya huduma ya fedha, maeneo ya kupaumbele ni kuongeza mitaji na matawi katika Benki ya Kilimo, Benki ya Rasilimali na Benki ya Wanawake; kujenga uwezo na utoaji huduma wa mikopo na mafunzo ya Wajasilramali. Aidha, Serikali itaendelea kupanga na kutangaza utalii na kushirikisha sekta binafsi kuwekeza zaidi katika maeneo ya vivutio nya utalii.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi. Pamoja na kuwepo kwa maeneo ya Kitaifa ya kimkakati na programu ya matokeo makubwa sasa, kutahitajika uwekezaji katika maeneo mengine ambayo yana uhusiano na maendelo ya kipaumbele ya Kitaifa. Miradi katika maeneo haya itaibuliwa na Sekta, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi na kutekelezwa katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, maeneo yatakayozingatiwa ni Elimu, Mafunzo ya Ufundi, Madini, Mifugo na Uvubi, Misitu na Wanyamapori, Afya na Ustawi wa Jamii na Ardhi, Nyumba na Makazi. Maeneo mengine ni Usafiri wa Anga, Hali ya Hewa, Biashara na Masoko, Utawala Bora, Ushirikiano wa Kikanda, Utambulisho wa Taifa, Sensa ya watu na makazi, Katiba mpya, Ajira na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya kina kuhusu maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2014/2015 yako katika kitabu cha mapendekezo ya mpango wa Taifa wa maendeleo 2014/2015, Sura ya Tatu.

Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka ujao. Makadirio ya mahitaji ya rasilimali fedha ya kugharimia bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/2015 ni shilingi Triliioni 19, bilioni 909.7. Kati ya hizo shilingi triliioni 11, bilioni 713.6 zitatokana na mapato ya ndani na shilingi triliioni moja, milioni 148 ni mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara. Shilingi triliioni mbili, bilioni 898.2 ni mikopo ya ndani na shilingi triliioni tatu, bilioni 772.0 ni misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho cha fedha kitagharamia matumizi ya kawaida na shilingi triliioni 14, bilioni 642.4 na miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi triliioni tano, bilioni 267.3, sawa na asilimia 26.45 ya bajeti ya Serikali. Katika bajeti ya maendeleo, fedha za ndani zitakuwa kiasi cha shilingi triliioni mbili, bilioni 643.3 na kiasi cha shilingi triliioni mbili, bilioni 624.0 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, izingatiwe kwamba, kiwango cha bajeti ya maendeleo kilichotajwa hapo juu hakikujumuisha fedha kwa ajili ya Mfuko wa Barabara na maendeleo ya rasilimali watu, ambazo kwa mfumo huu wa sasa wa bajeti zinapangwa kama sehemu ya matumizi ya kawaida, japokuwa kiuhalisia, ni matumizi ya maendeleo. Kama vipengele hivyo vikijumuishwa, bajeti ya maendeleo itafikia takribani asilimia 31 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujikita katika kuwezesha sekta binafsi kuchangia katika kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kipaumbele itakuwa ni kutumia rasilimali chache, kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi, pamoja na kuendelea kuboresha mazingira ya kibiasara na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji katika maeneo ya kipaumbele na yenye kuleta matokeo makubwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuboresha mfumo wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeelo hususan miradi ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya utekelezaji; mara baada ya mapendekezo haya kuridhiwa na Bunge, Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, zitatakiwa kuandaa na kuwasilisha Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha miradi itakayotekelzwa katika sekta zao kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, wiki ya nne ya Januari, 2014, Tume ya Mipango itafanya uchambuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Wizara za Kisikta na miradi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU]*

itakayopitishwa itajumuishwa katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015, na kitabu cha bajeti ya maendeleo kwa 2014/2015 *Volume iv.*

Mheshimiwa Spika, aidha Mamlaka za Serikali za Mitaa, zitatakiwa kuainisha miradi ya maendeleo na kuwasilisha mapendekozo ya miradi hiyo Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Wizara ya Fedha, kwa ajili ya kujumuisha katika kitabu cha bajeti ya maendeleo, yaani *volume iv.*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu, likae kama Kamati ya Mipango na kujadili mapendekozo niliyowasilisha ili Serikali iweze kunufaika na ushauri na maoni ya Waheshimiwa Wabunge. Baada ya kupata maoni ya Wabunge, Mpango wa Maendeelo wa Taifa 2014/2015, utaandaliwa na kuwasilishwa rasmi Bungeni Mwezi Juni, 2014. Serikali itazingatia maoni na ushauri wa Kamati ya Mipango ya Bunge Zima na kuyafanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono. Sasa utaratibu tutakaotumia, kwanza kwa kutumia Kanuni zangu hapa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti atakayetoea maoni ya Kamati ya Bajeti kwa muda wa saa moja, halafu na Kambi ya Upinzani nao watatoa kwa muda wa saa moja.

Nafikiri Kambi ya Upinzani itakuja baadaye mchana kwa sababu muda uliopo hautoshi, lakini baada ya hapo, itabidi niondoke na nguo ziondoke na ile Sime itoke kusudi tukae kama Kamati tujadili, lakini kwanza tupate maoni rasmi haya kwa pande hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti!

**MHE. ANDREW J. CHENGE-MWENYEKITI WA KAMATI YA**

**BAJETI:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 94(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, inalitaka Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango kwa siku zisizopungua tano katika Mkutano wake wa Mwezi Oktoba-Novemba kwa kila mwaka, ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba kwa kujadili na kushauri Serikali kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilikutana na Tume ya Mipango na kupata fursa ya kupokea na kuchambua mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015 kwa mujibu wa kanuni ya 94(4).

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kwa mujibu wa kanuni ya 94(5)(a) niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu maoni na ushauri wa Kamati kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015 uliowasilishwa na Serikali hivi punde.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba mnamo mwezi Juni, 2011, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; alitoa tamko la Kisera kwa Taifa kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuanzia Mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016.

Maelezo aliyyoatoa Mheshimiwa Rais kuhusu Mpango yameeleweka vizuri, hasa baada ya kuzingatia kuwa lengo la utaratibu wa awali wa nchi kupanga mipango yake kwa muda mfupi lilikuwa ni kujandaa na utengamavu wa uchumi mkuu ili kuweza kuanza na Mpango wa Maendeleo wa muda mrefu kwa kuanzia na Mpango wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012-2015/2016) ni

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI KAMATI YA BAJETI]*

awamu ya kwanza ya Mpango Elekezi (*Roadmap*) wa kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025 kwa kipindi cha miaka 15 iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudini kubwa zilizochukuliwa na Serikali katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, nchi yetu haikuweza kufikia baadhi ya malengo ya Dira yaliyowekwa kwa asilimia 100. Hivyo, mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa yaliyowasilishwa na Serikali mbele ya Bunge lako Tukufu ni maandalizi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji makini na kwa wakati wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kila mwaka, utafungua fursa za ukuaji wa uchumi na hivyo kuelekeza nguvu za Kitaifa katika maeneo ambayo yatakuza viwango vya jumla na vya kisekta, kiuchumi na hatimaye kuendelea kupambana na changamoto kubwa za kupunguza umaskini wa mahitaji muhimu na ule wa kipato.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuwasilishwa kwa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo mbele ya Bunge lako Tukufu, ni kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kutoa maoni na ushauri utakaosaidia kuboresha mapendekezo hayo kabla ya kuandaa Mpango wenywewe wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Waheshimiwa Wabunge yanatarajiwani kuboresha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kabla ya kufanyiwa kazi na kuletwani tena Bungeni kuitia Kamati ya Bajeti mwezi Machi/Aprili na hatimaye kuwasilishwa Bungeni rasmi asubuhi ya siku ya Bajeti. Hivyo, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wabunge wayatafakari mapendekezo haya na kisha wayatolee maoni na ushauri kwa jinsi watakavyoona inafaa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI KAMATI YA BAJETI]*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2013/2014; Kamati ilipata fursa ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali pamoja na baadhi ya miradi ya maendeleo kwa robo ya kwanza ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kifupi niainishe tathmini ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Bajeti, Mapato ya Serikali; lengo la makusanyo ya fedha kutoka vyanzo mbalimbali halikufikiwa kwa kiasi cha asilimia 14.3. Kamati ilijulishwa kwamba, katika robo ya kwanza ya mwaka 2013/2014, jumla ya mapato yote yalifika shilingi bilioni 3,082.2, sawa na asilimia 85.7 ya makadirio (*ceiling*) ya shilingi bilioni 3,598.5. Mapato yatokanayo na kodi yalikuwa shilingi bilioni 2,082.5 ikilinganishwa na makisio ya shilingi bilioni 2,492.3 sawa na upungufu wa asilimia 14.6.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa misaada na mikopo, Serikali imepokea misaada ya jumla ya shilingi bilioni 94.1 sawa na asilimia 32.4 ya makadirio ya shilingi bilioni 291 yaliyotarajiwa katika robo ya kwanza. Kati ya misaada hiyo, shilingi bilioni 43.4 zimepokelewa kama misaada ya kibajeti na shilingi bilioni 50.7 ni za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya masharti ya kibiashara katika kipindi hiki ilifika shilingi bilioni 118.6 kutoka benki na taasisi za kifedha kati ya ukomo (*ceiling*) wa dola ya Kimarekani milioni 700 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu hizi, ni wazi kwamba, katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2013/2014, malengo ya makusanyo ya mapato kutoka vyanzo vyote hayakuweza kufikiwa kikamilifu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI KAMATI YA BAJETI]*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; jumla ya fedha zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo katika kipindi hiki kwa miradi inayosimamiwa na Serikali Kuu ilifikia kiasi cha sh. 581,611,667,769, sawa na asilimia 11 ya fedha zote za maendeleo katika mwaka huo. Kwa upande wa fedha za mikoa, kiasi cha sh. 115,196,413,727, sawa na asilimia 17 tu ndio zilitolewa.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa upatikanaji wa fedha katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2013/2014, unaonesha kuwa ipo changamoto kubwa katika utekelezaji wa malengo tuliojiwekea katika bajeti, hususan kwa miradi ya maendeleo.

Hivyo basi, hatua za makusudi zinahitajika katika kubuni, kukusanya na kusimamia vyanzo vипya vya mapato. Vinginevyo, juhudzi za Serikali na wote wanaoitakia mema nchi hii katika maendeleo, hazitazaa matunda yanayotazamiwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto za kibajeti katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo; ili kutekeleza Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano, ilikadirisha kwamba kiasi cha shilingi triliioni 44.4 zitahitajika kugharamia mpango huo.

Mheshimiwa Spika, gharama hizi ni wastani wa shilingi triliioni 8.9 kwa kila mwaka, ambapo kati ya fedha hizo shilingi triliioni 2.9 zitatokana na fedha za ndani katika bajeti ya Serikali na shilingi triliioni 6.0 zitatokana na uwekezaji wa sekta binafsi na washirika wa maendeleo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kwamba, kwa miaka miwili ya kwanza ya kutekeleza wa Mpango huo, kiasi cha fedha za maendeleo kilichotengwa ni chini ya kiwango kilichowekwa na Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, fedha zilizotengwa kwa ajili ya Maendeleo zilikuwa shilingi trillioni 4.9 wakati katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 kiasi kilichotengwa zilikuwa shilingi trillioni 4.5. Kama hali hii itaendelea, matarajio ya kutekeleza malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ifikapo mwaka 2015/2016 hayatafikiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, moja ya sababu kubwa inayosababisha kutotolewa kikamilifu kwa fedha za maendeleo ni mfumo wetu wa Bajeti ya Serikali, unaotegemea makusanyo (*Cash Budget*). Katika mfumo huu, fedha za bajeti hugawiwa kwa jinsi zinavyopatikana. Hivyo, pindi makusanyo yasipofikia malengo ama ahadi za wafadhili zinapochelewa au kupungua, hali hii huathiri mapato ya bajeti na hivyo kusababisha kutotekelawa kikamilifu kwa shughuli husika katika kipindi hicho. Aidha, sehemu kubwa ya fedha za maendeleo katika Bajeti ya Serikali hutegemea fedha za nje. Kwa miaka kadhaa sasa tumeshuhudia miradi mbingi ya maendeleo ikishindwa kukamilika kwa wakati uliopangwa kutokana na sababu za kibajeti kiasi cha kuongezeza gharama Serikali kutokana na kuongezeka kwa gharama za miradi kunakosababishwa na ucheleweshwaji wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mbali na mfumo wa bajeti unaozingatia makusanyo ya siku hadi siku, kuongezeka kwa kasi ya matumizi ya kawaida ya Serikali imekuwa ni changamoto kubwa katika utekelezaji wa bajeti kwa upande wa miradi ya maendeleo. Kama ilivyoelezwa awali, fedha za makusanyo hukusanya kulingana na matumizi ya wakati husika, lakini mgawanyo huu hufanyika kwa kuzingatia vipaumbele. Katika utaratibu wa sasa, hakuna uwiano sawia kati ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kwa mfano, katika robo ya kwanza ya mwaka

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

huu wa fedha, jumla ya matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 3,806.5, sawa na asilimia 98.8 ya ukomo (*ceiling*) ya shilingi bilioni 3,854.2.

Mheshimiwa Spika, Mpango Elekezi wa Maendeleo ya Taifa letu unaelekeza kwamba, mgawanyo wa Bajeti ya Serikali ufanyike kwa uwiano wa asilimia 65 kwa matumizi ya kawaida na asilimia 35 kwa matumizi ya maendeleo. Hata hivyo, kwa mujibu wa bajeti iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka huu, bajeti ya matumizi ya kawaida inapaswa kuwa asilimia 68.07 ya matumizi yote na ile ya maendeleo inapaswa kuwa asilimia 30.93 ya matumizi yote. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha, matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 747.9, sawa asilimia 19.6, ambayo ni pungufu ya asilimia 30.93 ya kiasi hicho ambacho kingepaswa kutengwa kwa shughuli za maendeleo. Kama bajeti ya matumizi ya maendeleo ingetengwa kwa uwiano halisi, kiasi cha fedha kilichopaswa kutolewa kingekuwa shilingi bilioni 1,177.4. Huu ni upungufu wa shilingi bilioni 429.5, sawa na asilimia 11.33. Kwa upande wa matumizi ya kawaida kama fedha ingetolewa kwa uwiano halisi, kiasi hiki kingekuwa shilingi bilioni 2,629.14 tofauti na shilingi bilioni 3,068.04 zilizotolewa na Serikali. Hili ni ongezeko la asilimia 6.55 ya kiasi kilichostahili kutolewa kwa matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili la kasi ya matumizi ya kawaida linatisha na linapaswa kufanyiwa kazi (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa matumizi ya Serikali mwaka hadi mwaka huilazimu Serikali kuongeza bajeti yake hivyo hivyo mwaka hadi mwaka. Kwa kuwa wigo wetu wa kodi bado haujaweza kupanuliwa na kutumika kwa kiasi kikubwa, hatua ambayo imekuwa ya kawaida katika kila bajeti ni kuongeza viwango vya kodi ili kuweza kugharlamia matumizi yaliyoongezeka. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 bajeti ilikuwa trillioni 15, mwaka 2013/2014 trillioni 18. Mwaka ujao wa fedha mahitaji ya rasilimali fedha yanakadiriba takribani 19.9, tuseme trillioni 20. Kamati haipingi ongezeko la bajeti, ila ina

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

maoni kwamba, kila mara Serikali inapopanga kuongeza bajeti, ije na vyanzo vipyta vya uhakika vya mapato vinavyoendana na ongezeko la matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kuhusu ukomo wa ukopaji mikopo ya nje yenye masharti ya kibashara ambayo Serikali imejivekeea. Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo bado hazijaweza kutumia kikamilifu fursa ya kukopa mikopo mikubwa ya kibashara (*non-concessional loans*) kutohana na masharti kati ya Serikali na Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*). Kwa sasa kiwango cha mikopo ya nje kinachoruhusisha kwa mwaka ni kiasi kisichozidi Dola za Marekani milioni 700 kutumia *exchange rate* ya Dola moja kwa Shilingi 1,600 ni kama shilingi bilioni 1,120. Ni Maoni ya Kamati kwamba, masharti haya ni moja ya vikwazo vinavyokwamisha kutekelezeka kwa Miradi mikubwa ya Kitaifa ya Kimkakati kama vile ujenzi wa reli, bandari na kadhalika. Hata hivyo, pamoja na ukomo huo mdogo, Kamati inashangazwa na uamuzi wa Serikali wa kusita kukopa ndani ya ukomo huu kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya masharti ya kibashara iliyochuliwa na Serikali katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha ni kiasi cha shilingi bilioni 118.6 na hii ni pungufu kwa shilingi bilioni 161.4 kama Serikali ingekopa robo ya fedha yote katika kipindi hiki ambazo ni shilingi bilioni 280.

Mheshimiwa Spika, eneo hili ni vyema Bunge lako ikaliangalia na kutoa ushauri kwa makini. Kwa upande wa usimamizi na ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo, Kamati imebaini changamoto kadhaa ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi. Tume ya Mipango ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Kitaifa nchi nzima. Nchi yetu ni kubwa na miradi mingi hutekelezwa kwa wakati mmoja. Kamati inasita kuamini kwamba Tume ya Mipango katika hali yake ya sasa inao uwezo wa kutekeleza majukumu hayo. Aidha, Maafisa Mipango wa Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri, hutakiwa kuandaa maandiko ya Miradi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

na kuwasilisha Tume ya Mipango, TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu, kabla ya kuidhinishwa na kupangiwa fedha. Hata hivyo, Kamati imearifiwa kuwa wengi wa Maafisa hawa wana uwezo na uzoefu mdogo wa kuandaa maandiko ya Miradi hiyo. Miradi hii inahitaji utaalam na uzoefu wa hali ya juu. Kamati inaendelea kushauri kuwa, ipo haja ya kujengea uwezo Tume ya Mipango pamoja na Maafisa wa Mipango katika Wizara, Idara na Halmashauri zetu ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Manunuzi bado ni changamoto katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Kama nilivyowahi kulielezea Bunge lako Tukufu wakati nikiwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Bajeti ya Serikali ya mwaka 2013/2014, Sheria ya Manunuzi huiongezea Serikali gharama kubwa ya manunuzi ikilinganishwa na hali halisi ya soko. Kwa kuwa sehemu kubwa ya fedha za Bajeti huelekezwa katika manunuzi, ni dhahiri kuwa sehemu kubwa ya Bajeti inayopitishwa na Bunge haipati thamani halisi kwa bidhaa na huduma zinazonunuliwa na Serikali. Aidha, Sheria hii imekuwa kikwazo kikubwa cha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa vile mchakato wake una mlolongo mrefu. Sheria hiyo, pia hutoa mianya ya udanganyifu. Kamati inashauri eneo hili liangaliwe haraka.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2014/2015 na kuyafanya uchambuzi wa kina. Kuna maeneo ambayo Serikali imejitahidi kufanya vizuri kwa kusimamia na kutekeleza kwa ufasaha mipango ya maendeleo. Baadhi ya maeneo haya ni Miradi ya Barabara; kudhibiti mfumuko wa bei; kukuza kiwango cha ukuaji wa uchumi; na kuimarisha hifadhi ya chakula nchini.

Pamoja na mafanikio hayo kuna maeneo ambayo Serikali haijafanya vizuri, ikiwa ni pamoja na kuendelea kuongezeka kwa Deni la Taifa; madeni ya wazabuni wa ndani kutolipwa kwa wakati; kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya maji na umeme hasa vijijini; kutopatikana kwa wakati pembejeo za kilimo hasa mbolea; malimbikizo ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

mishahara ya walimu na watumishi wengine; na kukosekana kwa utekelezaji wa mpango wa masoko kwa mazao ya wakulima mfano kurundikana kwa zao la mpunga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mtiririko wa Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati, haujaweza kutoa picha kamili ya mwelekeo wa kukamilika kwa Mipango ya Maendeleo kwa muda uliopangwa. Uchambuzi wa kina unaonesha ukurasa wa 1 – 47, yaani Sura ya Kwanza na ya Pili, umebeba maelezo mengi ya nadharia kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo uliopita. Ukurasa wa 48 – 56, yaani Sura ya III imeelezea vipaumbele vitakavyozingatiwa katika maandalizi ya Mpango wenyewe na ukurasa wa 57 – 58, yaani Sura IV zinalezea ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo na ukurasa wa 59 – 62, yaani Sura ya V imeelezea utekelezaji, ufuatilaji na tathmini ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri yaliyoandikwa, Miradi mingi ya Maendeleo haijaaelezewa hatua iliyofikiwa na gharama zilizotumika na kiasi cha fedha kilichobakia kukamilisha Miradi hiyo. Aidha, Miradi mingi haijulikani utekelezaji wake utachukua muda gani na fedha zipi zitakamilisha utekelezaji wake. Kamati ya Bajeti ilitegemea kuwa Serikali ingewasilisha taarifa ambayo ingebeba maelezo ya kina kuelezea hatua iliyofikiwa katika kutekeleza Miradi hiyo, muda wa kukamilika Miradi, kiasi cha fedha kilichotumika, kiasi cha fedha kilichobakia kukamilisha Miradi na vyanzo vya fedha vitakavyotumika kugharamia utekelezaji wa Miradi husika.

Mheshimiwa Spika, Mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo yameelezea njia zitakazotumika kugharimia Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2014/2015. Kamati inashauri kuwa msisitizo uwekwe kwenye kuimarisha vyanzo vya sasa vya mapato; kuibua vyanzo vipyta ikiwemo kuingiza Sekta isiyo rasmi kwenye Mfumo wa Kodi; kutumia mfumo wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP); pamoja na misaada na mikopo yenye masharti nafuu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

ikiwemo ile ya masharti ya kibashara; pamoja na Serikali kupunguza matumizi ya kawaida na kuimarisha matumizi ya maendeleo ili kuhakikisha Miradi ya Maendeleo inakamilika.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo yameendelea kuelekeza utaratibu utakaotumiwa na Wizara, Mikoa na Serikali wa jinsi ya kufuatilia, kutathmini na kutoa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na hatimaye kuelezea wajibu na kazi za Taasisi mbalimbali katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2014/2015. Aidha, ieleweke kwamba awamu ya kwanza ya Mipango hii ya Maendeleo itafikia ukomo mwaka 2015/2016. Hivyo, juhudhi kubwa na maarifa ya kuleta mabadiliko zinahitajika ili Miradi ikamilike kwa muda uliopangwa. Serikali haina budi kuhakikisha kwamba, kila mdau anayehusika katika milango hii kwa nafasi yake ya kiutendaji anitimiza wajibu wake ili Serikali iweze kutekeleza vipaumbele vichache vitakavyoharakisha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini, pamoja na kuboresha na kuendeleza huduma za jamii.

Kamati inaona kwamba, pamoja na kauli za Serikali kwamba vipaumbele vinavyotekelawa ni vichache (Miundombinu; Viwanda; Maji; Kilimo, Ufugaji na Uvuvi; na Maendeleo ya Rasilimali Watu), tatizo kubwa Mheshimiwa Spika lipo kwenye idadi kubwa ya miradi ya tunayotazamia kuitekeleza kwa kutegemea fedha zetu za ndani na wahisani. Idadi hii kubwa ya Miradi haiendani na kiasi cha fedha kinachohitajika kugharamia Miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), Mheshimiwa Stephen Wassira, inaonesha kwamba, mwenendo wa uchumi Duniani siyo wa kuridhisha kutokana na kupungua kwa mahitaji na ongezeko dogo la ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoibukia na zile zinazoendelea. Pato la Dunia linatarajiwa kukua kwa asilimia 3.1 mwaka 2013 sawa na ilivyokuwa mwaka 2012. Kwa upande wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa Pato unaonesha kuanza

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

kuimarika na kufikia ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2013 baada ya kushuka kutoka asilimia 5.4 mwaka 2011 hadi asilimia 4.9 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2013, Pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 7.5 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Hii imetokana na ukuaji wa shughuli za kilimo asilimia 1.4, uzalishaji viwandani asilimia 8.6, umeme na maji asilimia 6.3, ujenzi asilimia 5.3 na uvuvi asilimia 2. Kamati inaipongeza Serikali katika juhudzi zake za kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya juhudzi kubwa katika kupunguza mfumuko wa bei. Takwimu zinaonesha kuwa, mfumuko wa bei umepungua kutoka kiwango cha asilimia 10.9 Januari, 2013 hadi asilimia 6.1, Septemba, 2013. Hii imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula hususan mahindi, mpunga na mtama.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015, takwimu zinaonesha kuwa, mwenendo wa viwango vya riba vinavyotozwa katika huduma za Kibenki siyo wa kuridhisha hasa kwa upande wa riba za kukopa ambazo zimeongezeka hadi asilimia 14.23 mwezi Juni, 2013 kutoka asilimia 13.92 mwezi Juni mwaka 2012 kwa riba za mwaka mmoja. Riba za kuweka kwa wastani zimepungua kutoka asilimia 12.12 mwezi Juni, 2012 hadi asilimia 8.65 mwezi Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha ajira imekua kwa asilimia 6.7, uwiano ukiwa mkubwa katika Sekta Binafsi ikilinganishwa na Sekta ya Umma. Hii ni changamoto kwa Serikali kuititia mipango yake ya kuimarisha soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa Deni la Taifa siyo wa kuridhisha; takwimu zinaonesha deni la umma na sekta binafsi limeongezeka hadi Dola za Kimarekani milioni 16.523 Juni, 2013 likilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

12,686.8 Juni, 2012. Hii imetokana na kuongezeka kwa mikopo ya masharti ya kibiashara na malimbikizo ya riba. Kamati haijapata taarifa ya kina kuhusu matumizi ya ongezeko la Deni la Taifa kwa mikopo iliyochukuliwa na Serikali. Aidha, Kamati ina wasiwasi kuhusu takwimu zinazotolewa na Serikali juu ya Deni la Taifa na nija zinazotumika kukokotoa Deni hili.

Mheshimiwa Spika, Mahusiano Kati ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mifumo Mingine ya Kimaendeleo; Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now (BRN)*), kuna wengine mitaani wanauita *better resign now*, sisi tunauita *Big Results Now (BRN)*, ni mfumo mpya ambao umeanzishwa na Serikali chini ya Ofisi ya Rais (*President's Delivery Bureau - PDB*) ili utumike katika kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango ya maendeleo hususan Miradi ya Kipaumbele ya Kitaifa iliyopo katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012) – 2015/2016). Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo katika maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2014/2015 yamehusisha mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa (*BRN*). Pamoja na nia njema ya Serikali ya kuanzisha mfumo huu, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

- Msukumo mkubwa unahitajika ili kuhakikisha Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati inatekelezwa kwa malengo na muda tuliojiwekea.

- Kuna dalili kubwa za kushindwa kukamilisha malengo ya *BRN* kwa kuzingatia ukosefu wa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo na kuhakikisha kwamba inakamilika ndani ya muda uliowekwa. (*Makofii*)

- Malengo na utekelezaji wa mfumo wa *BRN* hayajaeleweka vizuri kwa Watendaji wa Serikali na Wananchi wote kwa ujumla.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

- Madeni makubwa kwa baadhi ya Miradi ya Maendeleo na hivyo kuathiri muda wa kukamilisha Miradi hiyo.

- Ucheleweshaji wa maamuzi pamoja na mfumo wa manunuzi kuathiri utekelezaji wa haraka wa Miradi ya Maendeleo.

- Idadi ndogo ya walipa kodi na vyanzo vya kodi bado ni vichache na hivyo kuathiri mapato ya kutosha kuweza kugharamia mfumo huu na miradi ya maendeleo; na

- Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015 kutoainisha kwa kina Miradi iliyoibuliwa na mfumo wa *BRN* pamoja na namna ya utekelezaji wake kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mapendekezo ya Mipango wa Maendeleo unaozingatia utekelezaji wa Malengo Makuu yaliyoainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo – 2025 ambayo ilianza kutekelezwa mwaka 2000 ili kuongeza maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla na hivyo kuiwezesha nchi ya Tanzania kufikia hadhi ya nchi zenyе kipato cha katи. Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuweza kutekeleza baadhi ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia hasa kwa upande wa elimu ya msingi, afya, utawala bora, hali ya usalama, amani na umoja nchini. Hata hivyo, eneo la kuondoa umaskini wa kipato kwa kutumia rasilimali zetu zilizopo bado halijapatiwa ufumbuzi wa kutosha. Utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele na ya kitaifa ya kimkakati iliyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) na ile ya kila mwaka, bado haujaweza kutoa fursa ya kuwawezesha Wananchi wa kawaida kujikwamua kimaendeleo. Mipango hii imeendelea kuwa kwenye maandiko zaidi kuliko utekelezaji, kwani fedha nyngi zinazotengwa kwenye miradi husika hazitolewi kwa wakati kulingana na mahitaji ya miradi na ahadi za wafadhili zinazochelewa kutolewa kwa wakati.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa hapo awali, Kamati inatoa ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo unaokusudiwa kutekelezwa mwaka 2014/2015 ni lazima yaoneshe kuwa yanazingatia utekelezaji na uchambuzi wa changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo unaotekeliza hivi sasa, yaani mwaka (2013/014). Aidha, shabaha na misingi iliyowekwa katika kutekeleza Mpango ujao lazima zishabihiane na hatua iliyofikiwa mwaka huu. Kamati inapenda kutoa ushauri kuwa:-

- Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa yanatakiwa yaainishe malengo mahususi (*defined specific targets*) ya kila mwaka katika maeneo yote ya vipaumbele. Kwa maana nyingine, mapendekezo yaainishe Mpango wenye matokeo yanayopimika (*measurable*);
- Mpango wa Maendeleo utakaotokana na mapendekezo haya ulenge kujibu tatizo la umaskini wa kipato, mfumuko wa bei, kushuka kwa thamani ya shilingi na ukosefu wa ajira kwa vijana;
- Eneo lingine vyombo vinavyohusika kwenye utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo lazima vihakikishe vinasimamia ipasavyo utekelezaji wa Malengo ya Mipango inayowekwa kila mwaka;
- Sera za Fedha na Kodi zinatakiwa kujibu changamoto za ukosefu wa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo;
- Serikali iendelee kudhibiti matumizi ya fedha za umma;
- Serikali iendelee kutekeleza mipango thabitii ya kuendeleza rasilimali watu nchini; na

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

- Ushiriki wa Sekta Binafsi katika masuala ya kukuza elimu na ujuzi uwe wazi na wa kueleweka.

Mheshimiwa Spika, Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali kuwa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo lazima yawe dira ya kuagiza na kujenga nidhamu kwa vyombo vikuu vya kupanga, kufuatilia, kutathimini na kutekeleza Mipango ya Nchi. Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2014/2015 pamoja na kuelekezea msingi na shabaha ya utayarishaji wake ni lazima vilevile uoneshe jinsi Mpango unavyotarajiwu kujibu changamoto na vikwazo vya kimfumo (*Institutional*), vilivyojitokeza katika kuendesha na kusimamia Uchumi katika Mpango wa Maendeleo kwa Taifa wa Mwaka 2013/2014. Bado kuna tatizo la utekelezaji wa Miradi kwa wakati (*timeliness*); urasimu katika utoaji wa maamuzi kwa Miradi ya Maendeleo na upungufu wa rasilimali fedha katika kugharamia Miradi ya Maendeleo. Aidha, Mpango wa Maendeleo usisitize udhibiti na upangaji wa matumizi ya Serikali kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Isisitize kudhibiti matumizi bila ya idhini ya Bunge. Kwa hali hiyo sasa, inaonesha kuwa kuna kiasi kikubwa cha fedha kinatumika nje ya utaratibu na idhini ya Bunge lako Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo kubwa la kupashana habari (*flow of information*), utaratibu wa ufanyaji kazi, ushirikiano na maingiliano katika vyombo vinavyosimamia Mipango ya Maendeleo na Rasilimali Fedha (Bajeti). Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zimekuwa zikitoa taarifa, takwimu au kuandaa programu zinazokinzana kuhusiana na Miradi ya Maendeleo. Aidha, maeneo ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo umekuwa siyo wa kuridhisha kutohana na bajeti yake kutolindwa (*ringfenced*) na kutoa mwanya fedha hizo kuhamishwa ili kugharamia mambo mengine nje ya bajeti. Rasimali chache za Serikali zimekuwa zikitawanya katika miradi mingi, hali ambayo imeleta matokeo hafifu ya utekelezaji wa Miradi. Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2014/2015 hauna budi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

kurekebisha upungufu huu ikiwemo kuimarisha menejimenti na uendelezaji wa Uchumi wa Nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, idadi ya watu wa Tanzania imefikia milioni 44.9, kati ya hao, wanaolipa kodi ni kiasi cha watu milioni 1.7 kwa wafanyabiashara na watu milioni 5 kwa wafanyakazi. Idadi ya watu nchini inakua kwa kasi kuliko uwezo wa kiuchumi unaohitajika kuwapatia maendeleo endelevu, ikiwa ni pamoja na huduma muhimu za jamii kama vile elimu na afya, maji na kadhalika. Fedha zinazotengwa kwenye Miradi ya Maendeleo ni tegemezi na bado ni tegemezi na haziwiani na ongezeko la watu; hali hii inatishia uwezekano wa kupunguzwa umaskini, uwezekano wa kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (*MDGs*). Hali kadhalika, rasilimali hii ya watu haitumiki ipasavyo katika kukuza uchumi wetu. Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo 2014/2015 hayajafafanua namna Serikali itakavyoweza kutatua tatizo hili na hivyo kuweza kutumia rasilimali watu kuleta maendeleo ya nchi kuitia shughuli za uzalishaji na ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, wakati Bunge lako Tukufu linapitisha Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2013/2014, Kamati ya Bajeti ilielezea kuwa msingi wa kuainisha vipaumbele vya Taifa kwenye Miradi ya Maendeleo, ulilenga katika kufahamu kiasi cha fedha zitakazotumika pamoja muda wa utekelezaji wa Miradi. Hali ilivyo sasa ni kwamba, pamoja Bunge kuidhinisha fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, bado Miradi mingi haikuweza kupewa fedha hizo na pia hajaweka muda maalum wa kukamilisha Miradi hiyo. Hali hii inasababisha utekelezaji wa Miradi hiyo kusuasua na hivyo kupelekea kuongezeka kwa gharama za ulipaji wa fidia kwa baadhi ya Miradi.

Maelezo yanayotolewa na Serikali mara kwa mara, mathalani Mradi upo kwenye hatua ya upembizi yakinifu au majadiliano yanaendelea ya kumpata mhandisi mshauri au mkandarasi, hayasadii kukamilika kwa Miradi kama

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

hauna muda wa ukomo (*time frame*). Mfano mzuri ni Mradi wa Reli ya Kati, Reli ya Tanga – Arusha – Musoma, Gati Namba 13 - 14 Bandari ya Dar es Salaam. Bandari ya Mwambani – Tanga, Bandari ya Mtwara na Kituo cha Bandari Kavu cha Kisaraawe. Ninaweza nikasema mengi ambayo mtayasoma kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa ni vyema sasa ikazingatia kutoa muda maalum (*time frame*) katika kutekeleza Miradi hiyo na pia ilipe fidia haraka maeneo ya Wananchi yaliyochukuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi hiyo. Aidha, Watendaji wataokwamisha utekelezaji wa haraka wa Miradi hyo wachukuliwe hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa suala la ajira bado halijafanyiwa kazi kikamilifu. Hivyo, Kamati inapendekeza kuwa, Mpango uielekeze Serikali iandae na kutekeleza programu za namna suala la ajira litakavyotekelawa kwa kila sekta na rasilimali fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo katika kila sekta husika. Kufanya hivyo kutasaidia ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa programu za ajira nchini. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi iwekeze katika sekta zinazozalisha zaidi kama kilimo na viwanda vinavyosindika malighafi zinazopatikana nchini ili kujenga ajira zaidi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Serikali katika kuanzisha mfumo mpya wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa (*BRN*), ambao Serikali imeamua utumike katika kusimamia, kufualitia na kutathmini utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Utaratibu huu ni mzuri kama utatekelezwa ipasavyo kwa kuzingatia malengo yaliyopo. Hapo awali Kamati ilitoa ushauri katika baadhi ya maeneo ya msingi yatakayosaidia kutekeleza mfumo huu, ikiwa ni pamoja na watu kubadili mitazamo ya kifikra kwa kuwa tayari kuwajibika na kuwajibishwa pale wanapokosea. Nidhamu ya kuheshimu sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa isimamiwe ili kuhakikisha tunafikia malengo tuliojiwekea katika utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudzi za Serikali katika kuboresha huduma za fedha hapa nchini. Hivi sasa tunayo mabenki mengi yanayofanya kazi hapa nchini. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa kuboreka huko kwa Sekta ya Fedha kuendane na kuboresha mazingira ya wafanyabiashara wadogo na wa kati kuweza kupata huduma za kifedha kwa urahisi na kwa masharti nafuu. Aidha, masharti kuhusu mikopo yaliyowekwa na Benki Kuu kwa ujumla wake ni vyema yakapitiwa upya ili kupanua wigo wa ukopaji hapa nchini. Sasa hivi masharti hayo ni kero. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali ifanye ufatiti wa kupata taarifa zitakazowezesha yafuatayo:-

- Kuweka utaratibu kwa Mabenki kutenga sehemu ya faida (angalau asilimia 15 ya faida ya Benki husika) kwa ajili ya maeneo mahususi yatakayokuza uchumi na kuungeza ajira vijijini. Nchi nyingi zinafanya hivyo duniani. (*Makofii*)

- Kufahamu mantiki ya utaratibu wa Serikali kufungua akaunti zake kwenye Mabenki ya Biashara na baadaye kupatiwa mikopo kutohuna na fedha zake yenewewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kukabiliana na tatizo la kuchelewa kutolewa kwa fedha za bajeti kikamilifu katika kila robo mwaka. Kamati inapendekeza utaratibu wa sasa wa *cash budget* uangaliwe upya. Kamati inashauri Serikali irejee utaratibu wake uliotumika huko kabla ya mwaka 1995/1966 ili twende kwenye utaratibu wa *Capital Budget*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaanmini kwamba, ili nchi iweze kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati kama vile ujenzi wa reli mpya ya kati kwa *standard gauge*, bandari na kadhalika, ni lazima nchi iweze kufanya maamuzi sahihi. Kamati inashauri Serikali ikope kutoka katika vyanzo mbalimbali hususan mikopo ya nje yenye masharti nafuu ili kuweza kukamilisha Miradi husika pindi ikishindikana. Serikali

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

ichukue mikopo yenyenye masharti ya kibiashara baada ya kushauriana na Bunge. Aidha, Kamati pia inaishauri Serikali na kuitaka Wizara ya Fedha, kukamilisha mapema taratibu za nchi kutathminiwa kukopesheka katika soko la fedha la kimataifa (*sovereign rating*) ili kuweza kuipa Tanzania kiwango kinachotumika, kuthibitisha uwezo wake wa kukopa katika vyanzo vya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango inalo jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Kitaifa nchi nzima. Kazi hii ni ngumu na inahitaji uwezo wa kifedha na rasilimali watu. Kamati inashauri Serikali iwezeshe kifedha Tume hii ili iweze kujii marisha. Aidha, Tume iruhusiwe kuajiri wataalamu zaidi ili kuweza kufika maeneo yote ya Miradi ya Kitaifa. Sambamba na hili, Kamati inashauri ifanyike programu kabambe ya kuwajengea uwezo Maafisa wa Tume ya Mipango pamoja na wale wa Idara za Mipango katika Wizara, Idara za Serikali, Wakala na Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa ili kuwawezesha kumudu vyema majukumu yao katika uchambuzi na usimamizi wa Miradi. Kufanya hivi kutaboresha ufanisi katika Sekta ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaelewa kwamba, mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa mwaka 2014/2015 ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano ambao Bunge lako Tukufu liliuridhia pamoja na vipaumbele vyake. Pamoja na ukweli huo, katika utekelezaji imeonekana kuna changamoto nyingi zinazotokana na aidha uwingi wa vipaumbele ama uwingi wa Miradi ya vipaumbele na vipaumbele ndani ya vipaumbele. Kamati inapendekeza, ili tuweze kuona matokeo makubwa katika utekelezaji wa Miradi, tupunguze idadi ya Miradi katika kila kipaumbele ili Miradi itakayoteuliwa itekelezwe kikamilifu ndani ya muda mfupi. Tumalize biashara, kisha Miradi iliyobaki itekelezwe katika awamu zingine. Kufanya hivi kutasaidia kukamilisha Miradi mingi zaidi ifikapo mwaka 2015/2016. (*Makofi*)

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa la kulimbikiza madeni katika Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri. Madeni haya huathiri utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Sehemu kubwa ya Bajeti ya Serikali inayopitishwa na Bunge lako Tukufu hutumika kulipia madeni ya miaka ya nyuma na hivyo kuathiri utekelezaji wa bajeti iliyopangwa na kuidhinishwa na Bunge katika mwaka husika. Kamati inarejea pendekezo kwamba, kama madeni haya hayaepukiki, Serikali itoe Waraka kwa Taasisi zake zote kwamba, pindi wanapoandaa bajeti waweke pia bajeti ya kulipia madeni. Hata hivyo, madeni haya ni lazima yawe yametokana na shughuli zilizopangwa na kwamba yalishindwa kulipika katika mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwiano wa mgawanyo wa fedha za bajeti, Kamati inapendekeza Serikali iangalie uwezekano wa kuweka utaratibu maalum kwa fedha za maendeleo (*ringfencing*) hasa kwa miradi ya kipaumbele. Kufanya hivi kutasaidia sana katika kufanikisha utekelezaji wa miradi ya kimkakati iliyopangwa. Aidha, Kamati inashauri kwamba, utaratibu ulioainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa kutoa fedha za bajeti kwa uwiano wa asilimia 65 kwa matumizi ya kawaida na asilimia 35 kwa matumizi ya maendeleo, uzingatiwe na kusimamiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inarudia kuishauri Serikali kuendelea kutengeneza mazingira wezeshi kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kufanya hivi kutachochea uwekezaji hasa uwekezaji katika Miradi ya Maendeleo na hivyo kuisaidia Serikali katika azma yake ya kuileta nchi katika maendeleo kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza mwanzoni kupitia taarifa hii, kilichowasilishwa na Serikali ni mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015. Lengo ni kutuwezesha sisi Wabunge kuchambua mapendekezo haya na kisha kuishauri Serikali namna bora ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa mwaka utakaopitishwa na Bunge hili. Hivyo ni wasaa mzuri kwa Bunge lako Tukufu kuishauri Serikali kuhusu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]

masuala mbalimbali yaliyomo katika mapendekezo ya Mpango huu, kwa nia ya kuuboresha.

Mheshimwia Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa mara nyine, kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), Mheshimiwa Stephen Wasira, kwa kushirikiana vyema na Kamati wakati wa kujadili taarifa hizi. Namshukuru pia Waziri wa Fedha – Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, kwa ushirikiano anaoipatia Kamati hii. Ninawashukuru pia wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango, ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili na kuchambua Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka ujao wa 2014/2015. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Andrew J. Chenge – Mwenyekiti, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami, Mheshimiwa Mansoor S. Hiran, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa Christina M. Lissu, Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa Assumper N. Mshama, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Joseph R. Selasini, Mheshimiwa Salehe Pamba, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa John M. Cheyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru pia Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake katika mazingira

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI]*

magumu. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati kama ilivyoongozwa na Ndugu Elisa D. Mbise na Makatibu wa Kamati; Ndugu Lina Kitosi, Ndugu Michael Chikokoto, Ndugu Elihaika Mtui na Ndugu Michael Kadebe, kwa kuihudumia vyema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha rasmi taarifa hii na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema mwanzoni, Kamati ya Bajeti tunaipa saa nzima. Sasa mkiangalia muda tulionao, tumesalia na dakika kumi na tano, ambazo haziwezi kutosha kwa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mpango huu. Kwa hiyo, ninasitisha shughuli za Bunge kwa kipindi hiki mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.42 mchana Bunge lilitfungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu?

Mheshimiwa vipi mbona hatujaanza, ngoja kwanza tumwite Katibu!

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa  
kwa Mwaka 2014/2015**

*(Majadiliano yanaendelea)*

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), kuhusu jambo ambalo limetokea mapema.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Samahani; Kanuni gani?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, 68(7).

**SPIKA:** *Okay.*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kuhusu jambo ambalo limetokea mapema leo. Wakati Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, anazungumzia suala la wafugaji hapa Bungeni, alieleza na kuwatahadharisha wafugaji kote nchini juu ya matapeli, aliowaita matapeli, ambao alisema wajihadhari nao waliowachangisha kwa ajili ya masuala ya kuwatetea juu ya haki zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutolewa kauli ile, binafsi kama Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, ambayo tumekuwa tukipokea malalamiko ya wafugaji kutokana na *operation* inayoendelea juu ya majangili, nimepewa taarifa na wafugaji kwamba, walikuwa na umoja wao ambao kimsingi walifanya Mkutano rasmi kabisa uliofunguliwa na Serikali, uliofanyika hapa Dodoma katika Ukumbi wa *African Dream* tarehe 26 na 27 na kufunguliwa na Viongozi wa Serikali, ukiwa na wafugaji zaidi ya 250 kutoka maeneo mbalimbali nchini, ambapo walipitisha maamuzi juu ya masuala ambayo hapa yameitwa kuwa ni mambo ya kitapeli na mambo ambayo Viongozi wa Kiserikali wamekuwa wakishiriki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako ili Mheshimiwa Waziri wa Nchi aweze kuifuta ile kauli yake aliyoitoa, kuwaita hawa watu wa Chama cha Wafugaji na Viongozi wao ambao wengine mpaka hivi ninavyozungumza wako hapa katika eneo la Bunge kwamba ni matapeli na badala yake Serikali ijielekeze katika kutatua tatizo la msingi la Wafugaji ambalo Serikali yenyewe ndiyo imelisababisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

**SPIKA:** Naomba umalizie kuisoma hiyo Kanuni uliyonisomea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68 (7): *"Halikadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba "Mwongozo wa Spika" kuhusu jambo lolote ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papohapo au baadaye, kadiri atakavyoona inafaa."*

**SPIKA:** Basi natumia hii hatua ya pili; nitatoa baadaye kadiri nitakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Gekul!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nami naomba Mwongozo wako kupitia Kanuni ya 68 (7), kuhusu suala ambalo limejitokeza mapema hapa Bungeni asubuhi. Suala zima la operesheni na matatizo ambayo wafugaji wamekuwa wakikumbana nayo.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea, maeneo mengi nchini sasa mifugo ya wafugaji inapigwa bei, lakini pia hili liliombewa Mwongozo asubuhi ukasema Serikali itatoa Kauli baadaye. Ninaomba Mwongozo wako kwa nini shughuli za Bunge zisitishwe, Serikali ikatoa Kauli yake sasa hivi tukajadili kwa sababu tunapoongea wafugaji huko waliko wameji-*organise* wanataka kupambana na hao maaskari ambao wanaendesa *operation*. Hali hii ni tete, sasa ipo maeneo mengi kwenye Mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako, kuna sababu gani ya kusubiri wakati hali ni tete, amani inataka kuvunjika, lakini wale wafugaji wako kwenye hali mbaya, mifugo yao inauwawa na wao pia wanapata madhara hayo?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. P. P. GEKUL]

Naomba mwongozo wako ni kwa nini tusijadili hili suala hivi sasa?

**SPIKA:** Mimi ningekwambia usome Kifungu cha 53 (8), lakini nakuachia kwa sababu nataka nitoe maelezo. Kifungu cha 53 (8) kinasema hivi: *"Kitu mlichoamua Mkutano uliopita au Mkutano unaoendelea hakibadilishwi."* Kwa hiyo, tulichoamua asubuhi, naomba tuwe tunasikilizana, ni kwamba, tunataka Serikali izichukue zile hoja ikazifanyie kazi.

*Infact* sasa sisi tumeshaamua kwamba, kesho baada ya Kipindi cha Maswali, Kamati ya Uongozi itakaa tuweze kujaribu kuona ni namna gani tunai-*direct* Serikali ili tupate haya tunayoomba, lakini yakiwa yametengenezwa vizuri. Kwa sababu ningewaruhusu ndugu zangu ninyi tuzungumze tungekuwa ni kama *open cheque*, mnazungumza mwisho ng'ombe wanazidi kufa. Ndio maana nikasema tutumie utaratibu mzuri tupate haya yote na *ma-book* ya akina Mheshimiwa Lugola nayo yaende kwenye Kamati yangu ile ya Kilimo na wengine wanaoweza waende, lakini Kamati yangu ya Uongozi itakaa asubuhi iweze ku-*direct* ni namna gani tunachokitaka sisi.

Tusifanye vitu hivihivi maana ni jambo kubwa. Jambo kubwa huwezi kulifanya kama ni mradi tu Sheria namna hii, haiwezekani ndugu zangu; *Management* haitakiwi, tuzungumze halafu iweje? Kwa sababu Bunge linazungumza kwa hoja moja; hoja ipo so *open-handed*, hata hoja aliyoitoa Bwana Nkumba, anasema tuahirishe Bunge, ndiyo hoja, halafu tuzungumze kuhusu nini? Jambo hili kubwa.

Kwa hiyo, asubuhi Kamati yangu ya Uongozi itakaa. Serikali nayo kama inatoka wajue wenyewe ndiyo wanaojua zaidi na vyombo wanavyo, watumie hatua inayostahili, lakini na sisi tutakaa tui-*direct* Kamati yetu ije humu ndani kwa mjadala kabla hatujaondoka. Ndicho hicho tulichoamua; ndio maana sikutaka utumie Kanuni ya 53 (8) kwa sababu ni kitu ambacho kinaweza kuelezwu.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[SPIKA]

Tunaendelea, Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Asubuhi tulimsikia Msemaji wa Kamati, lakini sasa ni nafasi ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani na muda ni saa moja. (*Makofii*)

Samahani kidogo, Mheshimiwa Lukuvi, nakutaka kesho asubuhi utoe majibu haya aliyosema Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y. MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5)(a), napenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa Maoni hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, inapenda Watanzania wafahamu kwamba, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 ni kwamba; Bunge katika Mkutano wake wa mwezi Oktoba – Novemba kila mwaka, linatakiwa kukaa kama Kamati ya Mpango kwa siku zisizopungua tano, kwa madhumuni ya kujadili na kuishauri Serikali kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata. Aidha, ni katika mkutano huo huo, ambapo Bunge hujadili, kutoa maoni na ushauri kuhusu mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali, ikiwa ni pamoja na kujadili na kuishauri Serikali juu ya vyanzo vya mapato ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, inapenda vilevile Wananchi wafahamu kwamba, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ya 2014/2015 yaliyoletwa na Serikali ili yajadiliwe na Bunge hili ni ya nne katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016). Kwa maneno

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

mengine ni kwamba, imebaki miaka miwili tu kukamilisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016).

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, inapenda pia kuwalishwa Wananchi kwamba, wakati imebaki miaka miwili tu kwa Serikali kukamilisha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, umebaki mwaka mmoja tu kwa upande wa Chama cha Mapinduzi kukamilisha utekelezaji wa Mpango huo. Hii ni kwa mujibu wa Sura ya Tisa, Ibara ya 212 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 ambayo inasema kwamba: “*Chama cha Mapinduzi katika miaka mitano ijayo (2010 - 2015) kinanelekeza nguvu kubwa katika kutimiza lengo la msingi la Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 kwa kuendeleza jitihada za ujenzi wa uchumi wa kisasa na Taifa linalojitegemea. Katika kuzingatia jukumu hilo, Ilani hii ya CCM ya 2010 hadi 2015 inatangaza nia ya mordenisation ya uchumi. Mordenisation ya uchumi ndiyo njia ya uhakika itakayobadili na kuleta mapinduzi katika uchumi wa nchi, kujenga msingi wa uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda, kuondoa umaskini wa Wananchi wetu kwa kiwango kikubwa na hivyo kuwezesha nchi yetu kujitegemea...*”

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inataka Wananchi wapime na kufanya tathmini wenyewe juu ya mambo yafuatayo:-

- (i) Miaka mitatu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa Upande wa Serikali na miaka minne ya utekelezaji wa Mpango huo huo kwa upande wa CCM imeleta mabadiliko katika maisha yao yaliyokusudiwa na mpango huo?
  
- (ii) Je, ni kweli kwamba mkakati wa CCM wa kufanya Mapinduzi ya Uchumi (*Mordenisation ya Uchumi*) uliotangazwa na

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 umefanikiwa?

- (iii) Je, ni kweli kwamba msingi wa uchumi wa Tanzania unaongozwa na viwanda kama CCM ilivyoahidi kwenye Ilani yake ya Uchaguzi ya 2010?
- (iv) Je ni kweli kwamba umaskini wa wananchi umepungua zaidi kuliko miaka mitatu au minne iliyopita kama CCM ilivyoahidi kupunguza umaskini kwa Wananchi na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania?
- (v) Je, ni kweli kwamba sasa hivi Tanzania ina uwezo zaidi wa kujitegemea kuliko miaka mitatu au minne iliyopita kama ambavyo CCM iliahidi kwamba kabla ya 2015 Tanzania itakuwa na uchumi imara na hivyo kujitegemea?
- (vi) Je, ni kweli kwamba hali ya ajira hasa kwa vijana ni bora zaidi kuliko miaka mitatu au minne iliyopita kama ambavyo Serikali ya CCM ilivyoahidi kutoa ajira ili kupunguza umaskini wa kipato?
- (vii) Je, ni kweli kwamba elimu yetu ni bora zaidi kuliko miaka mitatu au minne iliyopita kama Mpango wa Maendeleo ulivyokuwa umekusudia? Ikumbukwe kwamba katika kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ndipo Taifa limeshuhudia kuperomoka kwa elimu kwa kiwango kikubwa kuliko vyote katika historia ya Tanzania. Ni kipindi ambacho tumeshuhudia zaidi ya asilimia 65 ya wanafunzi wa Kidato cha Nne wakipata alama sifuri katika mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2012. Ni kipindi ambacho

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

tumeshuhudia wanafunzi wanahitim darasa la saba na kufaulu bila kujua kusoma, kuandika na kadhalika.

(viii) Je, ni kweli kwamba Sekta ya Wanyamapor na Utalii vimeimarika zaidi kuliko miaka mitatu au minne iliyopita? Ikumbukwe kwamba, katika kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ndipo tumeshuhudia ujangili wa Tembo wa kutisha kuliko ilivyokuwa hapo kabla.

Mheshimiwa Spika, yapo maswali mengi ya kujuliza ili kujua kama Mpango umefanikiwa au la, lakini bila shaka majibu ya maswali haya yako wazi kwa kuwa kila kukicha malalamiko ya Wananchi kwamba hali ya maisha inazidi kuwa ngumu yanaongezeka.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2014/2015 ni sehemu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao nao ni sehemu ya kwanza kati ya sehemu tatu za mipango ya nchi ili kufikia Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Lengo la ujumla la sehemu ya kwanza ya Dira ya 2025 ni kutoa fursa ili hazina ya rasilimali za nchi zitumike ipasavyo ili kuweka mazingira wezeshi na kutanua wigo wa ukuaji wa uchumi ili watu maskini waweze kukua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, katika hotuba za mpango wa uchumi zilizopita, imejitahidi sana kuishauri Serikali namna mbalimbali za kusimamia utekelezaji wa Mpango, lakini mara zote Serikali imekuwa ikipuuza ushauri na matokeo yake ni kwamba, mipango hiyo imekuwa haitekelezeki kwa ufanisi, jambo ambalo limesababisha Wananchi kuzidi kuwa maskini na rushwa kuzidi kuongezeka. Tunaendelea bila kuchoka kuishauri Serikali hii ya CCM inayojitaa sikuvi lakini isiyosikia mapendekezo muhimu na kuyazingatia katika

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

uandaaji wa Mpango unaoweza kutekelezeka na ambao unaakisi hali halisi ya uchumi na Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zinaonesha kuwa, Serikali kwa ushauri wa Tume ya Mpango, iliweka vipaumbele kwa miaka mitano (2011/2012 - 2015/2016), ambavyo katika utekelezaji wake vitaleta matokeo ya haraka katika kuchochaea maendeleo ya maeneo mengine ya uchumi (*multiplier effect*); uwezo wa mradi husika kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi na hivyo kuongeza ajira. Vipaumbele vilivyochanguliwa ni kama ifuatavyo:-

- (i) Miundombinu;
- (ii) Kilimo;
- (iii) Viwanda;
- (iv) Maji; na
- (v) Rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tathmini ya utekelezaji wa Miradi iliyotajwa hapo juu sambamba na taarifa ya matumizi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji wa Miradi hiyo ili tuweze kupima malengo tuliojiwekea katika Mpango wa Miaka Mitano 2011/2012 – 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, kuna tofauti kubwa sana kati ya maendeleo yaliyoandikwa kwenye Mpango na Maendeleo halisi kwa Wananchi. Sababu za tofauti hii ni kama ifuatavyo:-

- (i) Tunapanga maendeleo yetu kwa kutegemea misaada au uvezeshaji toka kwa wahisani (Misaada na mikopo 30% +).
- (ii) Tunapanga mipango ambayo hatuwezi kuitekeleza. Miradi mingi inachukua muda zaidi ya muda uliopangwa na hivyo kuongeza gharama.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

- (iii) Miradi mingi ya maendeleo haina uhalisia wa malengo au mahitaji ya jamii inayolengwa (Miradi inakuwa siyo shirkishi na hivyo utekelezaji wake hauhusishi Wananchi).
- (iv) Serikali haijatekeleza vipaumbele ilivyoviweka (kupanga bajeti yake kulingana na maazimio iliyordhia).
- (v) Serikali imeshindwa kutoa fedha za maendeleo hata zile zilizopangwa kwenye bajeti yake kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango.
- (vi) Miradi mingi inayokamilika haikidhi viwango, jambo linalosababisha ukarabati wa mara kwa mara kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kuna usemi mmoja wa Wajapani unaosema kuwa; "*Planning without action is a daydream but action without planning is a nightmare.*" Hapa *action* ina maana ya bajeti itakayowezesha utekelezaji. Jambo la ajabu ni kwamba, Serikali ya CCM huwa inapanga bila kuwa na bajeti ya utekelezaji na ndiyo maana Mawaziri wanapoulizwa maswali na Wabunge juu ya utekelezaji wa Miradi fulani, hukimbilia kujitetea kwamba, kuna ufinyu wa bajeti ndiyo maana utekelezaji umekwama. Kupanga bila bajeti ndiyo tunaambiwa na Wajapani kuwa ni kuota ndoto za mchana. Je, Watanzania wataendelea kusubiri Serikali iote ndoto za mchana hadi lini?

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo yanaonesha kwamba, utendaji wa Serikali katika kuimarisha uchumi kwa kpindi cha 2013/2014 - 2015/2016 umefikia malengo katika baadhi ya maeneo na pia umevuka malengo katika baadhi ya maeneo.

Uchunguzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni unaonesha kwamba, Serikali katika kupanga, ilijiwekea malengo madogo ambayo ni rahisi kuyafikia na

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

kwa matumizi ya fedha nyingi na inapoyafikia inajigamba kuwa imevuka lengo. Kwa mfano, katika utekelezaji wa Mpango tunaambiwa kuwa, makusanyo ya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kwa mwaka 2013/2014 ni asilimia 20.2 ya Pato la Taifa na shabaha ilikuwa ni asilimia 19.1 ya Pato la Taifa. Hivyo basi, Serikali inajipongeza kwa kuvuka malengo. Hoja hapa ni kwamba, lengo hilo katika shabaha ni halisia katika uendelezaji wa mipango tuliojiwekea?

Je, makusanyo hayo yanaweza kutekeleza hata robo ya Miradi iliyo katika mpango wa mwaka huu? Kambi Rasmi ya Upinzani inasema shabaha na misingi hii haiakisi hali halisi ya rasilimali zetu na watu wake na hivyo ni mkakati wa kifisadi wa kuifanya nchi yetu iendelee kuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, ni katika utekelezaji wa Mpango huu wa Miaka Mitano ambapo kumekuwepo na ukwepaji mkubwa wa kodi na utoroshaji wa fedha za umma kwenye mabenki nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani ilitoa hoja binafsi hapa Bungeni na Bunge likaazimia kwamba, Serikali ifanye uchunguzi ili wahuksika wawajibishwe kwa mujibu wa sheria na kuinusuru nchi yetu na janga la uhujumu uchumi. Hadi nasoma Hotuba hii, Serikali haijaleta taarifa Bungeni kuhusu utekelezaji wa Azimio hilo la Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji; kwa mtindo huu Serikali itawezaji kutekeleza Mpango wa Maendeleo wakati fedha zinazotoroshwa zingeweza kuongeza Bajeti ya Serikali na hivyo kuepuka kuendelea kuwa tegemezi kwa nchi wahisani?

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kwamba, kati ya mwaka 2001 na 2011, Uchumi wa Tanzania ulikuwa kwa wastani wa asilimia saba kwa mwaka lakini umaskini ulipungua kwa asilimia mbili tu. Ukuaji mkubwa wa uchumi ilitokea kwenye Sekta ya Madini na Sekta ya Huduma. Kwa bahati mbaya ni kwamba, ukuaji huo haumlengi Mwananchi maskini. Kwa maana rahisi ni kwamba, jamii maskini za Watanzania zimeendelea kuwa maskini hadi sasa. Tafiti zinadhahirisha kuwa mapato ya kodi kutokana na uwekezaji yamekuwa kidogo sana na ajira zimezidi kupungua sana

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

hasa wachimbaji wadogo wamezidi kuhangaika kwa kukosa kazi wakati makampuni makubwa yamezidi kupata faida kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa misingi ya Mpango kwa mwaka 2014/2015 kifungu cha (c) kinasomeka kuwa ni kuimarisha utekelezaji wa Miradi iliyoibuliwa mwaka 2012/2013 ya Programu ya Matokeo Makubwa sasa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona hapa hakuna umakini katika kuhakikisha Mpango wa Miaka Mitano.

Miradi hii haikuibuliwa mwaka 2012/2013, bali Miradi hiyo ilitakiwa iwemo ndani ya Mpango wa Miaka Mitano na siyo kweli kwamba Matokeo Makubwa Sasa ni Mpango! Kiuhalisi ni kwamba, Matokeo Makubwa sasa ni *Monitoring Tool* ya Mpango wa Miaka Mitano ili kuhakikisha malengo ya Mpango yanapatikana kama illyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa ni kwamba, wasifu wa mtu na *record* yake ya nyuma ndiyo inatoa imani kwa watu; hivyo basi, bado Watanzania wana makovu ya Kampuni yao ya Simu na ile kampuni yao ya *Celnet*. Jinsi ambavyo uhujumu ulivyofanywa na kuiua na *Celtel* ya MO Ibrahim ikaingizwa nchini rasmi na kuchukua mali zote za iliyokuwa Kampuni ya Simu. *Celtel* ilikiwa chini ya uratibu wa Mratibu wa sasa wa Matokeo Makubwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mpango huu ambao umeletwa kwa ajili ya Bunge kuupitia na kutoa ushauri ni sehemu ya nne ya Mpango wa Miaka Mitano, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tathmini ya sehemu ya kwanza, pili na tatu, kama malengo ambayo yalikusudiwa yamefikiwa kwa kiasi gani na kama tumeshindwa tumeshindwa wapi.

Mheshimiwa Spika, kuna usemi unaosema kuwa, *if we can not measure, we can not manage* (kama hatuwezi kupima, basi hatuwezi kudhibiti). Hivyo basi, ni jukumu letu kama Bunge kwa niaba ya Wananchi kabla ya kukubaliana

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

na Serikali, kwanza, tupime yale yote tuliyokubaliana kuwa yatatekelezwa katika awamu zilizopita za Mpango wa Miaka Mitano ndipo twende mbele. Kinyume cha hapo ni ukweli usiopingika kuwa, tunawalaghai Watanzania na hata wale wote wanaochangia fedha zao kwa ajili ya kutusaidia kujikwamua katika umaskini.

Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba linakwamisha utekelezaji wa Mpango ni kutoshirikishwa kikamilifu kwa Wananchi katika hatua zote za uandaaji na utekelezaji wa Mpango. Kwa mfano, ni kwa kiasi gani Mpango wa Miaka Mitano unaeleweka kwa Wananchi? Hii ni muhimu kwani kuna maeneo ambayo jamii inawajibika kuwa washiriki katika utekelezaji wake. Mfano, sehemu ya nguvu kazi, badala ya kuleta nguvu kazi toka Uchina au maeneo mengine, vijana wa maeneo husika wanaweza kufanya kazi.

Je, ni mkakati gani umefanyika wa utekelezaji wa Mpango katika ngazi zote za Serikali za Mitaa kwa kuanzia ngazi ya Halmashauri, Kata hadi Vijiji unaweza kupimika?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasilitiza matumizi ya Mfumo wa Uwajibikaji kwa Jamii (*Social Accountability Monitoring – SAM*), ambao ni utaratibu unaojali na kuimarisha uwajibikaji kimfumo huku ukijenga uwezo kwa jamii, wadau na waajiri wa Serikali kuhoji na kupata ufanuzi toka kwa waliopewa mamlaka ya utekelezaji kwa maamuzi, matendo na taarifa zao za uwajibikaji wao katika shughuli za umma.

Mheshimiwa Spika, Mfumo huu unawarejesha Wananchi kwenye nafasi yao ya asili ya ukuu wa kuiwjibisha Serikali na vyombo vyke na watendaji wake. Unawakumbusha viongozi na watendaji katika huduma za umma juu ya uwajibikaji wao kwa matumizi ya rasilimali za umma, mipango ya matumizi, mgawanyo wa rasilimali; matokeo na ufanisi wa matumizi ya rasilimali hizo; mifumo iliyopo ya uwajibikaji na vyombo vya usimamizi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa mfumo huu unarejesha hadhi ya dola kuwajibika kwa wapiga kura wake, huku ikiwarejeshea hadhi yao kwa kupata taarifa, uwazi, kujadili mipango ya maendeleo, kujishirikisha kwenye utekelezaji mipango, kuchambua ufanisi na kuhoji maamuzi na utendaji.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama haya yasiyokuwa na uwajibikaji, je, tunaweza kutimiza malengo yetu ya Mipango?

Mheshimiwa Spika, katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/2014, kifungu cha 5.3 kinachohusu uratibu wa kusimamia fedha za maendeleo, kinaonesha kwamba, Wizara, Idara na Wakala au Taasisi za Serikali kujaza Fomu *TFN 358* kwa Miradi iliyopata idhini ya Tume ya Mipango na kuwasilisha Wizara ya Fedha kwa ajili ya ufuatiliaji wa tathmini na pia Taasisi hizo za Serikali zitatakiwa kuwasilisha Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha taarifa ya kila robo mwaka si zaidi ya wiki mbili baada ya robo mwaka unaotolewa taarifa husika kwa uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, hoja hapa ni taarifa ya fedha inayokwenda na hali halisi ya Miradi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona ni bora Bunge lipewe taarifa ya hali halisi ya maendeleo ya Mradi kwa fedha zilizotarajiwa kutolewa na zilizotolewa, Mradi umetekelezwa kwa kiwango kipi na unatarajia kukamilika lini. Hii inawapa hata Wananchi uwezo wa kupima utendaji kazi wa Serikali yao na siyo wangoje kuambiwa na washauri waelekezi kuwa mambo ni mazuri kama inavyofanyika sasa.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kuwa miongozo hiyo ya ufuatiliaji na kufanya tathmini ipo katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, lakini tatizo ni kwamba, mkakati wa utekelezaji wake ni tatizo kubwa kwani nyaraka zote na wanaoelewa ni wataalam washauri tu (*consultants*), nao wako Serikali Kuu lakini kwenye ngazi zingine za Serikali hakuna uelewa wa hilo. Kama Wananchi na watekelezaji

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

wengine hawashirikishwi kuelewa, ni vigumu sana kufanikisha Mpango yetu. Mpango ya TASAF ililetu matunda kwa sababu kubwa ya kuwa shirkishi na hivyo hata tathmini yake ilikuwa shirkishi na matokeo yake wazi.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mpango huu imeainisha maeneo ya Kitaifa ya kimkakati kwa mwaka wa 2014/2015 ambayo ni miundombinu, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu, huduma za fedha na utalii huku maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi yakiwa ni elimu au mafunzo ya ufundi, afya na ustawi wa jamii, mifugo na uvuvi, misitu na wanyamapori, madini, ardhi, nyumba na makazi, usafiri wa anga, hali ya hewa, biashara na masoko, Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, Utawala Bora, Vitambulisho vya Taifa, Sensa ya Watu na Makazi, kazi na ajira na mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inachambua maeneo hayo ya kimkakati kwa kuweka kipaumbele katika maeneo yafuatayo, ambayo kimsingi ni lazima Serikali iyatolee ufanuzi ili Bunge linapokaa kujadili Mpango wa mwaka 2014/2015, yatolewe ufanuzi na Serikali.

Moja ni Miundombinu; pamoja na kuwa ndiyo kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na kwa kuangalia fursa ya nchi yetu kijiografia ili kuhudumia Mataifa ambayo hayana fursa hasa ya bandari, Serikali imeshindwa kutekeleza matakwa ya mpango ya kuifufua Reli ya Kati na kuifanya kuwa katika kiwango cha usafirishaji wa abiria na mizigo kwa nchi jirani. Aidha, kwa kuwa miundombinu imegawanyika katika aina mbili (*hard and soft infrastructure*), *soft* inayohusisha umeme na mawasiliano mengine, miradi ya umeme imekuwa kitendawili, mgawo wa komyakimya umeendelea na hivyo uchumi wetu umezidi kuwa ghali na kufanya Watanzania kuzidi kutegemea bidhaa kutoka nje. Kwa tathmini rahisi ni kwamba, kwa upande wa nishati tumeshindwa. (*Makof!*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa, Serikali imeshindwa kuboresha elimu nchini na ni jambo la kushangaza kuwa, Serikali inaendelea kupiga danadana mustakabali wa elimu hapa nchini kana kwamba ni jambo la mzaha. Inatamka kuwa elimu ni kipaumbele katika nyaraka zake lakini katika ugawaji wa rasilimali fedha haioneshi kama ni kipaumbele, kwani inajisifu kwa suala zima la kuongeza madarasa na walimu huku kukiwa na madai ya malimbikizo ya mishahara ya walimu. Mishahara ya walimu ikiwa katika kiwango ambacho si tu kinawaumiza walimu, bali kinachangia pia kushuka kwa kiwango cha ufaulu, hali duni ya mazingira ya ufundishaji, kukosekana kwa nyumba za walimu, ubovu na kushindwa kwa Baraza la Mitihani la Taifa (*NECTA*) kusimamia majukumu yake. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa tunajadili Mpango wa Maendeleo wa Taifa utakaoleta mapendekozo ya uboreshaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitaka Bunge hili kupitia Kiti chako, kuitaka Serikali kuleta Ripoti ya Tume ya Kuchunguza Matokeo ya Kidato cha Nne iliyoundwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, iwasilishwe rasmi Bungeni na kujadiliwa ili kwa pamoja tuazimie hatua zitakazoweza kunyanya Sekta ya Elimu kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa migogoro ya ardhi nchini imeendelea kuongezeka huku Serikali ikionekana kukwepa moja kwa moja uwajibikaji ambao umesababisha upotevu wa maisha pamoja na uharibifu wa mali uliotokana na migogoro mingi sehemu mbalimbali. Pamoja na Serikali mara kadhaa kuahidi kutatua migogoro hiyo ikiwemo kuwalipa fidia Wananchi, kuyarudisha mashamba na maeneo ambayo wawekezaji wameshindwa kuyaendeleza na pia Serikali iliahidi kufanya ukaguzi wa mashamba kila mara ambapo Kambi Rasmi ya Upinzani imekua ikihoji.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza migogoro ambayo ipo na inaendelea ni kwa Serikali kupima na kutoa umiliki

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

wa ardhi kwa Wananchi. Katika kadhia hiyo ni dhahiri Serikali itanufaika kukusanya kodi (*land rent*). Faida kubwa zaidi ni kuwezesha ardhi yenyewe kutumika kwa manufaa na kupunguza ardhi kubaki bure bila matumizi kwa muda mrefu, matumizi yasiyo na faida au kuiweka ardhi kusubiri soko. Wenye ardhi watalazimika kuitumia kwa manufaa ili iweze kulipa kodi tajwa. Hii ni njia nyingine ya kuiongezea mapato Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kuujadili Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2014/2015, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, kupitia Wizara ya Ardhi yenyeye jukumu pana la kusimamia Sekta ya Ardhi kuhakikisha kwamba, Mpango unajumuisha pia kusimamia maeneo yote ambayo hayajaendelezwa na wawekezaji yarejeshwe Serikalini bure bila fidia kwani wahusika wamekiuka masharti ya mikataba ya wao kupatiwa ardhi husika. Aidha, Kambi inahitaji mrejesho wa usitishwaji, ugawaji na umilkishaji wa ardhi kwa wawekezaji wa nje kama Maazimio ya Wabunge yalivyo hitaji, baada ya Mheshimiwa Halima Mdee kuwasilisha hoja yake Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo ndiyo Sekta Mama katika utoaji wa ajira hapa nchini na inayoweza kuibadilisha hali nzima ya uchumi wa nchi kutoka uchumi tegemezi kwenda uchumi uliosimama bila utegemezi. Utafiti uliofanywa na shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha na kilimo la “PELUM ASSOCIATION” unaonesha kwamba, kwa kipindi cha kati ya mwaka 2000/2001 hadi 2008 fedha zilizotengwa na Serikali na zile zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya kilimo zilikuwa na upungufu wa kati ya asilimia 6 hadi 49. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, fedha za ASDP, Hazina ilitoa shilingi bilioni 107.1 kwa Wizara zinazojihusisha moja kwa moja na programu hiyo, lakini zilizotumika ni shilingi bilioni 77.9 tu, sawa na asilimia 72.8 zilizobaki, asilimia 27.2 hazijulikani zilitumika vipi.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Maendeleo, Serikali ilikusudia kuimarisha uwezo wa kitaasisi na mifumo kwa ajili ya usimamizi wa majanga katika maendeleo ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

Sekta ya Mifugo. Badala ya kutekeleza Mpango huo, Serikali ndiyo imekuwa chanzo cha majanga kwa wafugaji kwa kuuza ama kuua mifugo yao katika operesheni mbalimbali zinazoendelea nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la hifadhi ya jamii ni jambo ambalo Serikali haiwezi kuliepuka. Dhana ya hifadhi ya jamii ni chombo kimojawapo cha kupambana na kupunguza umasikini katika jamii. Hivyo basi ni jukumu la nchi kuhakikisha hifadhi ya jamii inahusisha Wananchi katika sekta rasmi na isiyo rasmi. Kwa hivi sasa Watanzania wanaonufaika na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni asilimia sita tu ya Watanzania wote. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza Mpango huu wa 2014/2015 ujumuisho yafuatayo:-

- Upanuzi wa wigo wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa sekta isiyo rasmi hasa wakulima wadogo ambao ni takribani asilimia 80 ya Watanzania.
- Uimarishaji wa Hifadhi ya Jamii kwa wakulima kwa kupitia vyama vyao vya ushirika ili waweze kujumuishwa katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii.
- Kuipitia upya na kuiboresha Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali ya CCM kutimiza ahadi yake ya kutoa pensheni kwa wazee kama ambavyo Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, katika kilele cha Siku ya Wazee Duniani, tarehe 1 Oktoba, 2010 alipowaahidi wazee kupata pensheni yao. Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA, inaikumbusha Serikali ya CCM kuwa, ni takribani miaka kumi imepita toka Sera ya Wazee itungwe mwaka 2003; hata hivyo, utekelezaji wake chini ya Serikali inayoongozwa na CCM umekuwa ni wa kusuasua. Kwa kuwa Mpango huu ni wa mwaka 2014/2015, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Pensheni ya Wazee inaingia katika maeneo ya kipaumbele.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

Mheshimiwa Spika, ugharamiaji wa Mpango. Mpango wa Maendeleo ya Serikali wa mwaka 2014/2015 ni dira ya kuakisi mpango wa kibajeti kwa mwaka 2014/2015 na ili kuweza kutekeleza mpango kwa ufanisi, ni dhahiri kuwepo kwa umuhimu wa kubainisha vyanzo vya mapato vya uhakika ambavyo vitawezesha kugharimia Miradi ya Maendeleo inayokusudiwa. Kuna haja ya Serikali sasa kutafakari kwa kina na kuona kazi kubwa inayofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuishauri Serikali juu ya uongezaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa kibajeti kila mwaka.

Hii inaweza kuijengea heshima nchi yetu na pia kuboresha huduma kwa Wananchi wake na si kwa kutegemea mapato ya nje ambayo yameendelea kuidhoofisha nchi yetu mbele ya uso wa dunia kwa kuwa Taifa tegemezi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inapendekeza kukusanya mapato ya ndani hadi asilimia 25 ya *GDP* ili kuweza kuendesha miradi yetu wenyewe. Uwezo wa makusanyo hadi kufikia hapo tunao, kwanza ni kupambana na makampuni makubwa ya kimataifa ili yalipe kodi stahiki na kuacha ujanja wa kukwepa kodi, kuondoa misamaha ya kodi na kuzuia upoteaji wa mapato ya ndani. Ni dhahiri kuwa mapato ya ndani yanaweza kutekeleza vipaumbele vyetu, ambavyo ni vifuatavyo ili kukabiliana na matatizo tuliyoyaainisha:-

Moja; utafutaji na ukusanyaji wa rasilimali ikiwemo za wakwepaji kodi na watoroshaji wa fedha.

Mbili, ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa kuwekeza kwa wakulima wadogo kwenye mashamba ya pamoja (*integrated production schemes*).

Tatu, kuwekeza katika Barabara, Maji na Umeme vijijini

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

Mheshimiwa Spika, katika miaka kadhaa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa nia njema ya kuijenga nchi yetu, ilipendekeza mambo kadhaa ili kuweza kuongeza mapato ya Serikali na moja ya mambo yaliyopendekezwa ni kuhakikisha kwamba, Serikali inakusanya kodi kwa kiwango cha asilimia thelathini kama ongezeko la mtaji (*capital gains*) kutokana na mauziano ya Kampuni yoyote ambayo mali zake zipo Tanzania. Je, utekelezaji wa ushauri huo umefika wapi?

Mheshimiwa Spika, lakini pia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza kupunguza misamaha ya kodi hadi kufikia asilimia moja ya Pato la Taifa kama wenzetu wa Uganda na Kenya. Serikali ilikubaliana na pendekezo hili kwa maneno lakini imeshindwa kulitekeleza licha ya kutoa ahadi za kufanya hivyo kila mwaka. Hivi sasa misamaha ya kodi imefikia asilimia 4.3 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani pia ilipendekeza kuifanya marekebisho Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kwa kufuta sehemu ya Kodi ya Mapato inayotoa fursa kwa kampuni za madini kutumia Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973 iliyofutwa (*grand fathering*). Pendekezo letu lilikuwa na lengo la kutaka kuweka mfumo wa *straightline method of depreciation* ya asilimia 20 badala ya sasa ambapo Kampuni za Madini hufanya *100 percent depreciation* kwenye mitambo yao mwaka wa kwanza na hivyo kuchelewesha kulipa *Corporate Tax*. Pendekezo hili ambalo lingi eipatia Serikali mapato mengi kwa sasa bado halijatekelezwa kwa kampuni za madini zenyewe mikataba.

Mheshimiwa Spika, kupuuuzwa kwa mapendekezo haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kunatafsiriwa kuwa wana vyanzo vingi vya mapato vya kuweza kutekeleza matakwa ya mpango wake. Ukweli ni kuwa, Serikali iko hoi bin taaban katika kukusanya mapato na hili ni wazi kwani fedha za maendeleo zinategemea misaada na mikopo toka nje.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wabunge kupinga hatua ya Serikali kutoza kodi ya matumizi ya simu za mkononi kwa Wananchi na Serikali kukaidi kuiondoa kwa sababu zake binafsi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuna haja ya Serikali kuwajibika kutoa huduma kwa raia wake na siyo kuendelea kumnyonya Mwananchi kwa kuweka kuwa ndiyo chanzo cha mapato ya Serikali, hivyo kuacha mianya katika vyanzo vya uhakika hususani vile tunavyovipendekeza kwa masilahi ya Wananchi na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango umezungumzia suala la kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi. Kuna tafsiri mbalimbali za sekta binafsi; kwanza, inayozungumzwa katika Mpango na nyine inayozungumzwa na Viongozi wa Serikali. Kumekuwepo na mjadala katika kukuza Uchumi wa Taifa katika nyanja ya uwekezaji, Viongozi wa Serikali bila aibu wameendelea kuidhalilisha nchi na watu wake na kunadi wawekezaji wa nje. Lazima sasa tujifunze kwa historia kama si ya nchi yetu juu ya kushindwa kwetu basi twende nje tuone walifanikiwa vipi. Tumrukkuu Mwanauchumi mmoja aliyefanya kazi Benki Kuu ya Dunia, *Joseph Stiglitz* aliwahi kusema; “*On average, resource-rich countries have done even more poorly than countries without resources.*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu kubwa kwa nchi zenye rasilimali asili kutonufaika nazo ni pamoja na uongozi mbovu na rushwa. Tunaanza kupata shaka sasa juu ya mabishano ya sisi kwa sisi kama Serikali na Wananchi yana tija gani kwa taifa? Kuna nini kwa wawekezaji wa nje hadi tuwapuuze wawekezaji wa ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali tunapoelekea kutoa mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali ni vyema kama nchi kuona umuhimu wa kukaa chini na kujadili kwa pamoja kama nchi na siyo kuishi kwa imla kwa minajili ya kwamba, nchi hii ni ya Serikali na siyo Wananchi. Kuna haja ya kuhitaji teknolojia kutoka nje lakini wawekezaji wa ndani wakilindwa na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

kupewa fursa ndiyo watajenga uwezo kiuwekezaji bali kupuuzwa ni dalili za kuanza kushindwa kwa Serikali na kufikia kutonufaika na rasilimali zetu kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutaka majibu ya kina juu ya masuala yote tuliyoyahoji kwenye Hotuba hii kuhusu utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2012/2013, 2013/2014 na mapendekezo ya 2014/2015; Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA, inataka maelezo mahususi kuhusu masuala yafuatayo:-

- Sababu za kutokuwasilisha Bungeni mpaka sasa Muswada wa Sheria mpya wala kufanya marekebisho ya kisheria kuwezesha uwajibikaji katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine, inaboresha usimamizi wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini na ufanisi wa Tume ya Mipango. Serikali itekeleze ahadi zake ilizotoa Bungeni mwaka 2011 na 2012.
- Sababu za kuanzisha Kitengo kingine cha Utekelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini (*Presidential Delivery Unit -PDU/PDB*) na kukiweka chini ya Ofisi ya Rais kama ilivyo pia kwa Tume ya Mipango, badala ya kuwa na sheria iliyotungwa na Bunge ya kuwezesha Taifa kuwa na mfumo thabiti wa uwajibikaji katika kushughulikia udhaifu wa upangaji, utekelezaji na ufuatiliaji. Sababu za kukwepo kuwasilisha Bungeni mikataba inayoelezwa kuingiwa chini ya Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Result Now*) wa Mawaziri husika kuwajibika pale wanaposhindwa kufikia malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia hali halisi ya utekelezwaji wa Mipango ya miaka miwili iyopita ni dhahiri kwamba, kama nchi inatubidi kuanza kupanga upya “*drawing board*.” Hii inatokana na hali halisi kuwa rasilimali tunazotarajia kutekeleza Mpango wetu tunatarajia zitoke

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

kwa wahisani na pia kile tulichonacho tunashindwa kukitumia kwa mahitaji ya Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa lengo kuu la sehemu ya kwanza ya Dira ya Taifa ya mwaka 2025 hatujaweza na hatutaweza kuitimiza kutokana na hali halisi ya jinsi tunavyopanga na kutekeleza yale yaliyomo kwenye Mpango wa Miaka Mitano ambayo ni sehemu ya kwanza ya Dira ya Taifa ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango umeonesha kila lengo na kiashiria chake cha mafanikio pamoja na bajeti ya jinsi ya kufikia lengo tajwa. Kwa bahati mbaya ni kwamba, mambo hayo yamebaki katika maandishi na vitabu tu. Kambi Rasmi ya Upinzani inashawishika kuamini kwamba, utekelezaji duni wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo hautokani na ukosefu wa rasilimali kama ambavyo Serikali imekuwa ikijitetea kila mara, bali ni ukosefu wa uongozi madhubuti katika kusimamia rasilimali za nchi na kuzigawa ipasavyo katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo. Hivyo, dawa ya kutibu tatizo hili ni mabadiliko ya Mfumo wa Utawala tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunatoa wito kwa Wananchi kuchagua Serikali itakayoongozwa na CHADEMA kumaliza malalamiko ya Serikali ya CCM yasiyo na msingi kwamba, Miradi inashindwa kutekelezwa kwa kuwa bajeti haitoshi. Wakati Serikali ya CCM inalalamika kuwa bajeti ni finyu, mafisadi wanatorosha fedha kwenda Uswisi na kwingineko hawashughulikiwi. Wakati ardhi yetu inaporwa na wageni, Serikali inapuuzia Azimio la Bunge la kufanya tathmini ya ardhi, wakati tembo wa nchi hii wanakwisha kutokana na ujangili uliokithiri, Serikali inawakumbatia majangili hata wale ambao tayari wametajwa na kadhalika. Kwa jinsi hii tutaendeleaje? Kwa vyovoyote vile, tunahitaji utawala mwingine unaojali masilahi ya Taifa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. E. SILINDE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante. Katibu hatua inayofuata!

### **KAMATI YA MIPANGO**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi ninakwenda kutoa mavazi haya na Siwa hii itawekwa ili tuweze kuongea kutokana na maamuzi haya.

Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mnashangaa kwa nini sikukaa hapa; hakuna vifungu tunaongea tu.

Waheshimiwa Wabunge, tuna muda mpaka saa mbili kasorobo na tunaweza kuwapata wachangiaji kama kumi na mbili. Nitaanza na Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema. Ninawataja lakini nitawapanga wakati wa kuzungumza, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa, atafuatiwa na Mheshimiwa David Kafulila, atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany na Mheshimiwa Amina Abdallah Amour; hawa tutaanza nao na tutaendelea baadaye.

Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale!

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii niwe mchangiaji wa kwanza. Nina mambo machache ambayo ninataka niyachangie katika hotuba hii.

**MWENYEKITI:** Tunafuata Kanuni za Fedha, ni dakika kumi.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwa kuishukuru Serikali, hasa kwa mipango mingi na kwa barabara kubwa ambazo zimejengwa kila sehemu ya nchi yetu. Imekuwa ni ukombozi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MCH. L. N. MWANJALE]

kwa sababu ninasafiri kutoka Sumbawanga, Mwanza, kila mahali ni barabara za lami; hilo ninaishukuru Serikali kwa Mpango yake mizuri.

Kitu ambacho ninataka nikiseme hapa ni kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Umeme, Maji na Barabara hasa za vijiji. Mwaka jana tulipewa ahadi ya kutekelezwa kwa umeme katika vijiji vingi hapa nchini, lakini kwa bahati mbaya inaelekea kuwa Mpango huo haukuweza kukamilika sawasawa, vijiji vingi havikupata umeme.

Mwaka huu tena au mwaka 2013/2014, tumepewa orodha ya vijiji vingi ambavyo vinatakiwa vitekelezwe kwa kuwekewa umeme, lakini nina mashaka kama ahadi hiyo au Miradi hiyo itatekelezwa. Kuna ahadi ya kutekeleza vijiji vingi sana, kwangu viro vingi na karibu kila Mbunge alipewa orodha ya vijiji hivi. Vilevile kuna mpango wa kutekeleza Miradi ya Maji vijiji, ambapo ndani ya Bunge lako hapa tulipiga kelele na kutengewa shilingi bilioni 184.5 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maji, ambayo kwa miaka mingi ilikwama. Nina wasiwasi kama Miradi hiyo itatekelezwa kwa sababu sisi ambao tunatoka huko Halmashauri tukiuliza fedha kwa ajili ya Miradi ya Maji zimefika wanakwambia bado!

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi kuwa mpaka kufikia mwaka kesho mwezi wa saba, Miradi hii yote itakuwa imetekelezwa. Pia nina wasiwasi kama Miradi hii ya Umeme na Barabara kama itakuwa imetekelezwa. Ninaomba zipatikane fedha za kutekeleza Miradi hii ambayo tulainishiwa vizuri sana katika Bunge lako na kama hazitapatikana kwa kweli tutakuwa tumeingia katika mtego mbaya sana. Naiomba Serikali ihakikishe kuwa Miradi hii yote ambayo illainishwa inatekelezwa kwa mwaka 2013/2014. Huu mpango ni mzuri lakini usipokuwa na utekelezaji inakuwa haina maana tena. Tunaweza tukawa tunasomewa hii Mpango lakini ni Mpango ambayo mwisho wake haitekelezwi na hailetii faida.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MCH. L. N. MWANJALE]

Ninaomba Miradi hii ambayo tuliambiwa kuwa tunatafuta fedha za kuhakikisha umeme vijiji na mijini, maji vijiji na mijini inatekelezwa, Serikali ihakikishe kuwa fedha hizo zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni la kutathmini, kama nilivyosema mwaka jana, tuliambiwa Miradi kadhaa itatekelezwa lakini haikutekelezwa na hatuambiwi tulishindwa kwa sababu moja, mbili, tatu. Ninafikiria kuwa, kitu cha kwanza ambacho tungekuwa tunaelezwa ingekuwa ni tulifika wapi katika utekelezaji ambao tulikuwa tume pangiwia. Tukiambiwa na Serikali kuwa vijiji kadhaa vitatekelezewa umeme na tunapokwenda kwa Wananchi tunawaambia jamani mwaka huu tumetengewa kiasi hiki, vijiji ishirini au thelathini vitapewa umeme. Visipopewa mwisho wa siku sisi tutaambiwa ni waongo.

Miradi mingi ya Maji ni hivyo hivyo na kila Wizara hapa ilikuja na Mpango wake mzuri sana. Wizara ya Maji imekuja na Mpango wa vijiji vingi kutekelezewa Miradi ya Maji, lakini mwaka umepita hatujaona kijiji hata kimoja ambacho kimetekelezewa Mradi wa Maji; ilikuwa ni hatari kubwa sana kwetu. Mwaka jana tuliambiwa Miradi hii yote ambayo tumeainishiwa itatekelezwa na tukipeleka mbele hawa watu watafikiri kwa vyovyote vile tumeona uchaguzi umefika ndiyo maana tunataka kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Miradi yote hasa ya Umeme, Maji na Barabara, Serikali ihakikishe inatafuta fedha kwa udi na uvumba, zipatikane fedha hizo ili Miradi hii itekelezwe, ifikapo mwaka kesho mwezi wa saba angalau Wananchi wajue kuwa sasa Serikali inafanya kazi. Kinyume na hapo, Serikali tunajiu wenywewe. Ninaomba Mpango huu wa Maendeleo wa mwaka 2014/2015 ulete matunda, tuisome kwenye karatasi na mwisho tusipate matokeo yake.

Ninaombwa Serikali ijitahidi kwa sababu ninachokumbuka ni kwamba, fedha kwa ajili ya kutekeleza

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MCH. L. N. MWANJALE]

Miradi ya Umeme haikupatikana na tukaiomba Serikali itafute kwa namna yoyote ile; na kwa kweli Kamati ya Bajeti ninaishukuru, ikakaa, ikaja na Mpango kamili na kutueleza kuwa billioni 184.5 zimepatikana kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maji. Mpaka sasa Miradi hii ya Maji haieleweki kama kweli itapata fedha ya kukamilishwa na kwenye umeme hivyo. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iliangalile suala hili, la sivo tutakuwa tunajua wenyewe, tunawaambia uongo Wananchi ambao wanatusikia tukisema.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Miradi ya Maji na Miradi ya Umeme itekelezwa, ifikapo mwezi wa saba mwakani kama ilivyo katika mikataba. Miradi hiyo iwe imekwishatekelezwa, tukinyimwa hapa itakuwa CCM tunajua wenyewe. Nina imani kuwa kwa kero hii iliyopo, bila shaka Serikali inasikia na itafanya yale ambayo imetuahidi. Nasi tunaenda kifua mbele kwa Wananchi kuwaambia jamani Serikali ni sikuvi imesikia na fedha zitapatika kwa vyovypole vile kuhakikisha kuwa Miradi hii ambayo iliainishwa mapema itatekelezwa.

Mimi sina mengi zaidi ya hayo, lakini ninaiomba Serikali ihakikishe inatuondoa katika matatizo hayo na Wananchi, la sivo tutaambiwa Wabunge ni waongo na Serikali ni waongo. Ninaomba hizo shilingi billioni 184 kwa ajili ya maji zipatikane, maana mpaka sasa inaelekea fedha hizo bado hazijapatikana. Shilingi billioni zaidi ya mia mbili kwa ajili ya umeme nazo zipatikane ili Miradi hii yote ambayo tumeainishiwa hapa na kila Wizara imeleta, iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kamani, atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. T. M. KAMANI]

ujao. Nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kazi inayofanya, inajibidiisha sana kutimiza Mpango huu.

Kwa siku tisa nilipata nafasi ya kufuatana na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Ziara ya kikazi kule China. Niliona kazi kubwa ambayo Serikali inafanya katika kuingia utaratibu wa mikataba ya kufanya kazi na nchi marafiki na iliingia mikataba mingi na hasa ya Miradi ambayo tunasema ya kimkakati; kwa mfano, ujenzi wa Reli ya Kat, Mikataba ya Nishati ya Uzalishaji, Bomba la Gesi, Usafirishaji, Miradi ya Makaa ya Mawe kule Liganga na Mchuchuma, Bandari ya Bagamoyo na maeneo mbalimbali ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, niliona kazi kubwa, mtoto wa mkulima alikuwa anafanya kazi usiku na mchana; ninampongeza sana kwa kazi nzuri aliyofanya. Nakushukuru nawe kwa kunipatia ruhusa ya kusafiri.

Katika Mpango huu uliowasilishwa, nimeona eneo moja ambalo ninaona kama Serikali hailiangalii kwa kina ni eneo la kimkakati lakini sijui kwa nini Serikali hailipatii uzito ni eneo la Uwekezaji la Kurasini. Katika kipindi cha bajeti tulilizungumzia sana, lakini fedha linayopewa ni ndogo sana, eneo linahitaji fidia ya shilingi bilioni tisini na nne. Eneo hili lingeweza kufungua Miradi mikubwa na kuifanya Tanzania kuwa ndiyo kituo kikuu cha bidhaa kutoka China kwa nchi za Maziwa Makuu, ambapo ingetengeneza ajira nyingi, tungepata kodi nyingi, usafirishaji na mambo mengine kadha wa kadha na hivyo Serikali kupata mapato. Sijui kwa nini Serikali hailioni hili?

Ninafikiri ni muhimu sana katika Mpango ujao ulipaji fidia ufanyike katika eneo hili ili kazi ianze kutekelezwa.

Eneo lingine limezungumzwa na mzungumzaji aliyepita, kuhusu ugharamiaji wa Miradi hii. Tulipitisha bajeti kwa ajili ya mwaka huu na utaratibu mpya wa kupitisha bajeti, lakini fedha mpaka hivi sasa hazifiki kwenye Miradi iliyokusudiwa kwenye Halmashauri zetu na sehemu mbalimbali za Miradi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. T.M. KAMANI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa hivi tunakaribia katikati ya mwaka na miradi hiyo haijaanza kutekelezwa, maana ya kubadilisha ule mfumo wa bajeti ili kuwa ni nini? Matokeo hayapo, naiomba Serikali, kama kweli ile nia njema ya kutengeneza bajeti kwa utaratibu ule mzuri iweze kuleta matokeo chanya, ni muhimu fedha iwasilishwe katika maeneo yaliyokusudiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo muhimu sana katika kuondoa umaskini wa Watanzania, ni kuwekeza katika kilimo. Katika mpango wote huu, eneo la kilimo limezungumzwa kwa uchache sana na kwa miradi midogo midogo sana na hivyo asilimia themanini ya Watanzania wanaoishi kwa kutegemea kilimo, hawawezi kuondokana na umaskini. Nashauri Serikali ili angalie eneo la kilimo kwa karibu kabisa kwa sababu bila kuleta mapinduzi ya kilimo katika nchi yetu, tusitegemee madini, utalii, sekta nyingine yoyote ambayo itaondoa umaskini kwa haraka kwa wananchi bila kuwekeza katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa kwa mfano katika Ukanda wetu ambao tunategemea zao la pamba, zao la pamba linategemewa na wananchi karibu milioni kumi na nne, karibu theluthi ya Watanzania wote lakini bado watu wanatumia mbegu za kizamani, Serikali ni kama imeenda likizo katika usimamizi wa zao la pamba. Zao la pamba lina sheria, lina kanuni zake kumi, linaachiwa watu wanajipangia wanavyotaka walime. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unategemea wananchi hawa watabadilika namna gani? Wanatumia mbegu za kizamani ambayo unasema ndiyo babu zetu walikuwa wanatumia mbegu za namna hii. Maana ya kuwa na sayansi ni nini? Maana ya kuwa na vituo vya utafiti ni nini kama sayansi ile haiwezi kuingizwa katika kilimo. Mwenye wajibu wa kusimamia sayansi iingie ni Serikali. Kwa hiyo, naomba Serikali ichukue jukumu kubwa katika usimamizi wa mazao yote makuu, kwa sababu bila kuwekeza katika kilimo hatuwezi kubadilika hata kidogo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. T.M. KAMANI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za karibuni nimeona au tumeshuhudia katika nchi yetu kitu cha ajabu sana. Mtu mwenye akili timamu, una gari lako linapata pacha, unakasirika mpaka unalichoma moto? Haiingii akilini. Tanzania ina rasilimali ya mifugo, ni nchi ya tatu katika Bara la Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusingekuwa na mifugo hii, Serikali ingepaswa kuagiza mazao ya mifugo ya *protein* kutoka nje. Sasa kuna *import substitution*, hatuagizi mazao kwa sababu mifugo ipo pale, hatuoni umuhimu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaeleza katika Bunge hili kwa hesabu rahisi, kunapokuwa na kundi la ng'ombe elfu tatu ni shilingi bilioni moja kwa bei ya chini. Tunaenda nje kutafuta uwekezaji wa bilioni, wakati tuna bilioni zinachezacheza hapa. Eti tu kwa sababu ng'ombe hawakusimamiwa vizuri, wameingia sijui kwenye eneo la msitu, wameingia kwenye shamba, watu wanaenda kupiga risasi ng'ombe sijawahi kuona katika maisha yangu. Hatuwezi kuwa na Serikali yenye unyama wa namna hii, haikubaliki! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli binadamu yeoyote mwenye akili timamu, anayesimama kumpiga ng'ombe risasi na ng'ombe hajajipeleka mwenyewe kwenye eneo, ng'ombe anapelekwa na mtu, mtu huyo alaaniwe.

**MBUNGE FULANI:** Ni kweli!

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mungu achukue hatua kabisa. Haiwezekani mnyama ana haki ya kuishi kama binadamu mwingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshindwa kusimamia maendeleo ya mifugo ambayo yangeweza kuleta thamani kubwa kwa nchi hii. Mazao ya ngozi, ungewawekea miundombinu mizuri wafugaji hawa ungeona. Usifikiri watu hawa hawana akili. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. T.M. KAMANI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kitabu hiki cha Mipango, ukurasa wa 37, naangalia miundombinu kwa ajili ya mifugo imejengwa sijui Kondoaa, sijui Bahi lakini maeneo yenye ng'ombe wengi, hakuna mradi hata mmoja wa maji. Halafu mnasema mifugo inahama kutoka Shinyanga, kutoka Mwanza, kutoka Simiyu, iende wapi wakati huweki hata muundombinu huko? Sasa tunategemea tutayapatajeye mazao bora? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sekta ya kilimo katika maana yake halisi ni pamoja na mifugo kwa sababu wananchi wetu ni wakulima na wafugaji. Kwa kweli unyama huu ni hatari. Mungu atatulaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naendelea kuiomba Serikali, kwanza hatua zinazoendelea sasa hivi zisimamishwe mara moja ili wananchi wapate amani. Ng'ombe wanakamatwa, wanafungiwa kwenye mazizi kwa siku tano wanakufa. Katika Mkoa wangu karibu elfu tatu...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba Serikali ijielekeze kwenye suala hili katika mipango yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Godbless Lema, atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Aliko Kibona na Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nilipokuwa nikisoma hiki Kitabu cha Mpango na nilipokuwa nasikiliza majibu ya Mheshimiwa Waziri Sitta asubuhi wakati anajibu suala la *East Africa*, nilipata mashaka ya utawala bora na nilijuliza maswali mengi sana. Kama Waziri mwenye dhamana ya kutafuta *reconciliation* na kuleta watu pamoja anaweza kuwa *source* ya kuvunja mshikamano na *community* ya Afrika Mashariki wakati huu

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. G.J. LEMA]

ambapo dunia inakabiliwa na changamoto kubwa ya ugaidi ambapo mshikamano na ushirika ni kitu muhimu sana. Nilipokuwa natafakari, sikumwona Sitta peke yake, nikaiona Serikali nzima ya Chama cha Mapinduzi kuhusu utawala bora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango yote hii mnayoisema, hata kama mtaleta watu kutoka mataifa yaliyoendelea kuwafanya *research*, haitakaa ifanikiwe kwa sababu miyo ya wataawaala wa Chama cha Mapinduzi imepoteza *dignity*. Huwezi kumsaidia mtu unayemchukia kufanikiwa kwa sababu tu wewe ni Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanatembea na uchungu sana. Mheshimiwa Dokta Kamani ametoka kuongea sasa hivi, anasema anaumia na ameomba Mungu aingilie kati kwa sababu anajua Serikali yake haiwezi tena, nami nikukaribishe huku, kwamba imefika mahali binadamu anapiga ng'ombe risasi. Mimi nikushangae kwamba unashangaa ng'ombe kupigwa risasi, binadamu wanapigwa risasi kila siku na kuuawa na hakuna hatua zimechukuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapowaona mnashangaa ng'ombe wanapigwa risasi na hamuumi binadamu wanapopigwa risasi na wanavyopewa kesi za kizushi na kuwekwa magerezani, nami ninawashangaa. Nimwombe tu Mungu kwamba kila uchungu anaopitia binadamu ambaye hana *influence*, upite pia katika familia zenu ili wote tuimbe wimbo unaofanana wa kutaka haki katika Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taifa hili, utawala bora ni *issue crucial* sana. Hapa Bungeni kumekuwa na mijadala mingi sana kuhusu maisha ya watu huku nje, kuhusu unyama unaotendeka, kuhusu watu wanavyoumizwa lakini Serikali imekuwa ikichukulia kawaida. Kwa sababu ya wingi wenu, mtaendelea kushinda lakini kwa sababu mnaoshinda ni dhambi, mshahara wa dhambi ni mauti na hayo mauti yatawakuta tu siku moja. (Makofi/Kicheko)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. G.J. LEMA]

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema, jadili hoja tafadhali. Naomba jadili hoja. (*Kicheko*)

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea utawala bora.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa  
Wakiongea kwa sauti za juu)*

**MWENYEKITI:** Namwomba Mheshimiwa Lema ajadili hoja, kelele za nini. Naomba uendelee kujadili hoja.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora naendelea nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema hapa, ninaomba nieleweke kwamba ninaongelea utawala bora, kwa sababu mambo yote yanayosemwa hapa, yatafanikiwa kwa sababu ya kuwa na msingi bora wa utawala bora. Ndio nikasema unapokuwa na watawala ambao hawana *dignity*, watawala ambao wanafikiri Polisi wanaweza wakawa chanzo cha kuleta amani na sio haki na ukweli, nchi hii mtaaingiza mahali pagumu sana. Kwa hiyo, niishauri Serikali na hasa Chama Tawala ambacho kimepewa dhamana ya kuongoza, ushauri wetu kuhusu haki na ukweli msiupuuze na muelewe kwamba lengo letu sisi sio tu kuwanyang'anya dola 2015 lakini pia tukiona kwamba mnazingatia ushauri wetu, mnafanya kazi inavyotakiwa, mnawenza kujenga Taifa letu katika utu, pengine hata 2015 mkajikuta mnapewa ridhaa, ridhaa ambayo kwa sasa katika mioyo ya watu mmeshanyang'anya. Hali ni mbaya sana kuhusu utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mazingira. Nimeangalia katika mipango huku, ukiangalia tishio lingine katika ulimwengu baada ya ugaidi, ni mazingira. Leo Naibu Waziri wa Maji wakati ananijibu swali langu la nyongeza kuhusu tatizo la maji Arusha, Waziri alisema chanzo kinachosababisha kuwepo na tatizo la maji katika Jimbo la

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. G.J. LEMA]

Arusha mjini ni pamoja na vyanzo vya maji vimekauka kwa sababu ya ubovu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira ni *sensitive* sana. Hivi tunavyoongea sasa Ziwa Manyara miaka kumi iliyopita kina chake kilikuwa kati ya mita kumi na kumi na mbili lakini sasa ni mita moja mpaka mita moja nusu na wataalam wanasema kwamba pengine miaka mitano ama miaka kumi inayokuja Ziwa Manyara linaweza likakauka na likikauka maana yake ni kwamba ndege wanaopatikana maeneo yale ambao wanavutia utalii, hawatakuwepo, wataondoka na eneo lile litakuwa *dormant* hasa katika biashara ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inapoandaa mipango, kipaumbele cha kwanza sana na cha msingi sasa hivi ambacho sijui nishauri Serikali ifanye kitu gani kwamba mazingira iwe jambo muhimu sana. Hali ikiendelea kama ilivyo, ukataji wa miti ukiendelea kama ulivyo na sioni *alternative* ya Serikali, kwa sababu mnavyowaambia watu wasiuze mikaa, wasikate miti wakati huohuo bei ya gesi inazidi kupanda, huwezi kuwaambia watu wale chakula kibichi wakati wanaweza kukata miti wakapata mkaa wakapikia chakula. Serikali yetu isipoweka mkakati maalumu kuhusu mazingira, Taifa letu katika miaka michache inayokuja linaweza kuwa jangwa na watoto watakaokuja kuishi miaka ijayo, watasema wazazi wetu hawakufanya kitu cha maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Serikali ilichukulie suala la mazingira kwa kipaumbele sana. Kipaumbele kikubwa kama ambavyo huwa mnajipanga kuzuia maandamano yetu ya kudai haki, nguvu hizohizo pelekeni kwenye suala la mazingira kwa sababu hali ya mazingira katika Taifa letu ni mbaya sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la maji na umeme. Maji ni biashara, umeme ni biashara. Arusha Mjini ni Jiji, kuna Kata ambayo iko kilometa tano kutoka Jiji la Arusha Mjini haina umeme miaka zaidi ya 50 ya uhuru. Umeme huu ni biashara kwamba mtu akifungiwa umeme anafungiwa na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. G.J. LEMA]

Luku na huyo mtu analipa bili ya umeme. Ni biashara ambayo ingeweza kufanyika kwenye umeme na maji peke yake, kama mngekuwa *sensitive* na mka-*plan* vizuri ingeweza kusaidia ku *boost* uchumi wa nchi hii kwa kiwango kikubwa sana. Mnaacha pesa kwenye umeme, mnaacha pesa kwenye maji, mnakwenda kutafuta pesa kwenye pembe za ndovu na kwenye vitalu ambavyo siku ya mwisho vinakuja kuangamiza kabisa uchumi wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme tu kwamba Serikali yetu ukiitazama mipango yake, unaona watu walioandika vizuri lakini huoni weledi, huoni *positive thinking*. Kama hawa wangekuwa wana-*commitment* ya kweli kuhusu Taifa hili, Taifa hili lingeweza kubadilishwa katika vitu vichache sana. Ndiyo maana Kagame wakati fulani akasema kwamba akipewa bandari ya Tanzania peke yake ya Dar-es-salaam anaweza akalisha Tanzania na Rwanda. Ilionekana kama ni tusi lakini alionyesha *commitment* ya *leadership* na *positivity* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi na nyumba. Arusha inaenda kuwa *squatters...*

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, nimesema nitamwita Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Aliko Kibona na badala ya Mheshimiwa Mchungaji Msigwa atakuwa Mheshimiwa Wenje.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo ya Taifa ambao ni muhimu sana. Tunajua kwamba Mpango wa Maendeleo ni elekezi kwa ajili ya kutengeneza bajeti ya mwaka unaokuja. Bahati nzuri kwenye Mpango huu katika kusoma kwangu, naweza nikasema ni mpango ambao unaelekeza tunatoka wapi, tunaenda wapi. Katika mpango huu Serikali, kwanza naipongeza imeweza kuelekeza imefanya nini kwa mwaka

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. M.L. KIGOLA]

2012/2013. Kwa hiyo, Serikali imetoa picha imefanya nini. Kweli ukiangalia kila Wilaya, kila Mkoa na kila Majimbo ambapo sisi tupo kule, kwa kweli Serikali imejitalihidi sana, napenda kuipongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano mdogo tu kwenye miundombinu, ukiangalia barabara zimejengwa, kwa mfano barabara ya kutoka Iringa kwenda Mafinga imeisha na imejengwa kwa kiwango cha lami kizuri, kwa hiyo, tunaipongeza Serikali. Vilevile Serikali kwenye miundombinu hiyo hiyo, mwaka jana nilikuwa naiomba Serikali iweze kufanya upembuzi yakinifu katika Jimbo langu la Mufindi Kusini barabara inayotoka Nyororo kwenda Igohole mpaka Mgololo, bahati nzuri wale wapembuzi yakanifu walifika pale na walianza kazi. Kwa hiyo, lazima tuangalie tunafanya nini huku nyuma. Bahati nzuri sasa hivi tunajadili Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2014/2015. Nliombe Serikali kwamba vitu ambayo havijafanyika kwa mwaka 2013, tunaomba tukiingia kwenye bajeti ya mwaka 2014 ambayo tunafuata Mpango wa leo, yale ambayo tutayapendekeza sisi Wabunge lazima yaingie kwenya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nipendekeze kwa Serikali, tukija mfano kwenye kilimo, Watanzania wengi sana wanategemea kilimo lakini bado katika utawanyaji wa mbolea katika Wilaya na vijiji bado inasuasua. Hii mbolea ambayo inatawanywa kwa mfano kwenye Jimbo langu mimi kuna sehemu nyingine kwa mfano hii mbolea ya Minjingu wananchi wanalamika wanasema haisaidii. Mimi naiomba Serikali ifanye utafiti wa kutosha kuangalia hii mbolea kama inasaidia wakulima. Kwa mfano, mimi vijiji vyta Nyigo na Idunda nimekuwa nafanya mikutano kule wanasema hii mbolea bado haijawasaidia sana, inawezekana katika utowaji wa elimu na matumizi yake wananchi wale bado hawajapewa vizuri, sasa naiomba Serikali ifanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, Serikali iliahidi na ahadi hiyo ipo na kwenye bajeti ilionesha kwamba mimi nimepwa shilingi 1.9 bilioni kwa ajili ya kueneza umeme kutoka Makambako ambaao utakuja Nyigo, Mbalamaziwa mpaka

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M.L. KIGOLA]

kule Malangali na Ihoanza lakini ile kazi bado haijaanza. Namwomba Waziri mhusika kwenye mipango hii ambayo tunaiweka maana tunategemea mwaka 2014 umeme utakuwa umeshawaka, kwenye muongoza wa mipango yetu, naomba hivi tunavyoviongea sasa hivi tunasema kuna *Big Result Now* na hii *Big Result Now* inaonyesha matokeo halisi na katika matokeo halisi yanataka vitendo, vitendo ndio hivi, sasa hivi tunakimbizana na muda, naomba Waziri husika na Nishati, kama alivyoahidi na wananchi wameshafanya *wiring* na yeche aliashajibu akawaambia wafanye *wiring* kwenye nyumba zao, namwomba Waziri aweze kutekeleza ile kazi mapema sana kwa mwaka huu 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwenye kilimo cha umwagiliaji, nadhani tulipitisha sheria hapa na ile sheria lazima tujikite kwenye mipango yetu, kwa mfano umwagiliaji. Mimi kwenye bonde langu la Mgololo, wananchi walilitikia sana na wamelima kwa sehemu kubwa lakini sasa hivi vitendea kazi ni duni. Wale wananchi wanalima kwa kutumia matrekta ya kukodi ambayo ni bei kubwa sana yaani *cost* ya kulimia inakuwa kubwa kuliko kipato atakachopata. Kwa hiyo, naiomba Serikali, nadhani uwezekano upo katika sehemu ambazo tumesema tutafanya kilimo cha umwagiliaji, Serikali ipeleke matrekta kwa wananchi wale, hata yakiwa matrekta ya mkopo kwa bei nafuu na kwa riba nafuu ili waweze kulima kwa urahisi. Kuna sehemu nyingi sana ambazo tulisema kwamba kilimo cha umwagiliaji kinawenza kikafaa kwa mfano kule kwangu ukienda Idete, niliongea hata mwaka jana, nilisema wananchi wa Idete wanataka trekta ili waweze kulima vizuri. Kuna bonde lingine la Idumlavano, kuna wakulima wanawenza kulima kilimo cha umwagiliaji kikasaidia sana nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ni muhimu ni kwenye vituo vya afya, ingawa Serikali imefanya vizuri lakini kwenye mpango ni lazima tuoneshe, hapa nilikuwa nasoma naona bado haijaonesha vizuri. Vile vituo vya afya vinasaidia sana wananchi kule. Bahati nzuri Waziri wa Afya nadhani yupo hapa ameahidi kunipatia *ambulance* kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Mgololo. Kwa hiyo, namwomba sana

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M.L. KIGOLA]

kabla hatujamaliza mwaka huu, kwa sababu alisema nimepewa shilingi milioni 150 kwa ajili ya *ambulance* kule, wananchi wale bahati nzuri walikusikia na walikupongeza, kwa hiyo wanaisubiri, nadhani ndani ya mwaka huu kufikia Disemba tunaomba tuwe tumeshaipata kwa sababu kule mvua zinanyesha sana wananchi wanashindwa kusafiri kwenda hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vituo vya afya ambavyo bado havijaisha. Naomba viingizwe kwenye mpango, kwa mfano kituo cha Mninga pale bado hakijaisha, kituo cha Mtwango hakijaisha, kuna kituo kingine kiko pale Bumilainga. Naomba vyote hivyo viingie kwenye mpango ili tunapoingia kwenye bajeti tusiwe tunaulizana tena maswali tunasema vitu vingine havipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa mchango wangu kwenye eneo la viwanda. Serikali inategemea mapato makubwa kutoka kwenye viwanda. Kama viwanda vitakuwa havifanyi kazi kama inavyotakiwa, hiyo inatuletea hasara kubwa sana kwa Taifa letu. Kwa mfano, sasa hivi kile kiwanda cha Mgololo ni kikubwa sana katika *East Africa* au naweza nikasema Afrika nzima. Kile kiwanda pamoja na kwamba tumempa mwekezaji mpaka sasa hivi ninapoongea kile kiwanda kimefungwa. Kufungwa kwa kiwanda kile kunaleta hasara kubwa sana kwenye pato letu la Taifa. Naiomba Serikali na Waziri wa Viwanda na Biashara akae na Waziri wa Maliasili na Waziri wa Uwekezaji waangalie jinsi ya kukiendesha kile kiwanda kwa sababu sasa hivi kinaendesha kwa *style* ambayo siyo ya uwekezaji. Sasa hivi kimefungwa na kuna wafanyakazi zaidi ya 1300, mwezi uliopita hata mshahara wao wamechelewa kuupata, wamepata juzi ambayo ilikuwa tarehe 21, kwa hiyo, mtu anafanya kazi miezi miwili anapata mshahara wa mwezi mmoja, hii ni hatari sana kwa wananchi wale wanaofanya kazi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, kile kiwanda kwa sababu ni kikubwa, pia naipongeza Serikali kwa kujenga kiwanda kikubwa kama vile, lakini bado, kwa mfano sasa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M.L. KIGOLA]

hivi kuna ugomvi kati ya Maliasili na mwekezaji kwamba bei ya magogo imepanda, sasa ile kupanda kwa bei ya magogo, naomba Mawaziri hawa wawili wakae, waangalie jinsi ya kuendesha kile kiwanda, la sivyo kama mwekezaji ataona ameshindwa kuingia kwenye *competition* ya bei ya magogo, basi wafanye utaratibu hata wa kuirudishia Serikali ili wafanyakazi wetu wale wasipate shida sana. Nakumbuka miaka ya nyuma kiwanda kiliwahi kufungwa kikakaa muda mrefu sana kwa sababu ya Serikali kushindwa kuendesha kile kiwanda, lakini isije ikatokea tena kiwanda kile kikafungwa kikaa kwa muda mrefu bila kufanya kazi. Kwa hiyo, naomba Serikali hii ilichukulie hili suala kwa umakini sana ili wafanyakazi wale waendelee kufanyakazi pale.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kumbukeni huu ni Mpango, mkianza maji kijiji cha wapi na wapi na wapi, unaondoka kuwa Mpango wa Taifa inakuwa tena maneno yaleyale. (*Makofii*)

Kama mmesoma vizuri kile kitabu cha Mpango, hakijataja kijiji cha mtu. Kwa hiyo, mtu hapa atakayekuwa anataja vijiji vyake, kwa kweli tutakuwa hatuelewani hapa. Naomba tujadili Mpango ili kusudi tuiongoze Serikali katika mambo yale ambayo tunafikiria ni ya *priority* na siyo kuanza kuongelea vijiji vyetu. Kwa hiyo, tunaendelea kwa msingi huo ili kusudi watu watuelewe, maana hawatatuetelea tukianza kusema vijiji vyetu leo, vijiji vyetu tutavisema baadaye, kwa sasa muendelee kujadili Mpango.

Sasa ni zamu Mheshimiwa Kibona atafuatiwa na Mheshimiwa Wenje, Mheshimiwa Mohamed Mgimwa, Mheshimiwa Deusderius Mipata, Mheshimiwa Barwany,

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MWENYEKITU]*

Mheshimiwa Kafulila na wa mwisho nadhani ni Mheshimiwa Anna Abdallah. Mheshimiwa Kibona!

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii niwe mionganini mwa wanaochangia mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulikuwa na utaratibu kama huu, tuliletewa mpango mzuri. Wenzangu wamesema, yapo maeneo mbalimbali ambayo Serikali kwa kweli imejitalihidi, imefanya kazi kubwa, Wilaya mbalimbali tumeona barabara zinajengwa, barabara zinapanuliwa, madaraja yanajengwa, lami zinajengwa na kadhalika. Katika eneo hilo, napenda kuipongeza Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya pongezi hizo, napenda niseme upungufu ambao binafsi nimeuona. Tunaona mpango mzuri, kama mwaka jana kwa mfano tumeletewa mpango kwamba Serikali italeta minara kwenye Wilaya zetu Kitaifa. Mpango ule nina wasiwasi labda nitaambiwa vinginevyo kwenye bajeti ijayo, kwamba tutaingia mwaka wa fedha ujao ile mipango ambayo tuliwapelekea wananchi, tukarukaruka, tukawaonesha kwenye makabrasha kwamba Serikali imejipanga hivi, hatutafika huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutafika huko kwa sababu nina ushahidi, maeneo mengi, Wilaya nyingi ikiwemo ya kwangu ile mipango ambayo tulisema kwamba Serikali imojiandaa, haijakamilika. Nina wasiwasi kwenye eneo hilo. Naomba Serikali ijpange vizuri, kama wenzangu walivyoshauri kwamba tunaingia kwenye mwaka mpya wa fedha, tusijetukadhalili, amesema Mchungaji pale kwa uchungu kwamba ni hatari mtu mzima kuwaambia watu kwamba kitu fulani kitafanyika halafu kitu hicho kisifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa harakaharaka, mwaka jana pia tuliambiwa juu ya mpango wa Serikali kuhusu kufufua na kuendeleza miradi ya makaa ya mawe hapa nchini.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A.N. KIBONA]

Nataka nijielekeze kwenye mgodi wa makaa ya mawe Kiwira. Mwaka jana niliambiwa kwenye mpango, Serikali inaendelea na mazungumzo kutafuta mwekezaji, leo ukurasa wa 19 katika kitabu hiki cha mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa, naambiwa tena bado mchakato unaendelea. Sasa hii *Big Result Now* inatia wasiwasi. Tumeambiwa kwamba *Big Result Now* (Matokeo Makubwa Sasa), mwaka jana ninacho kitabu kama hiki, Serikali ilikuwa inazungumzia mchakato wa kurudisha mgodi wa makaa ya mawe Serikalini kutoka kwa wawekezaji feki leo naambiwa Serikali inaendelea na mchakato. Naomba Waziri wa Nishati na Madini tutakapoingia kwenye bajeti, ninaamini Wabunge wenzangu hawatamuelewa tutakapokwuwa tunazungumza kitu ambacho tulizungumza mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu kilimo, nadhani kilimo kuna matatizo. Kwa nini ninasema kuna matatizo? Ajabu ni kwamba mpaka sasa hivi tunaelekea kwenye msimu wa kilimo lakini huwezi kuamini mgawo wa mbolea baadhi ya vijiji vinapata mifuko 20 kijiji kimoja. Hapa sijui hii tunaiita Kilimo Kwanza, Mjumbe mmoja aliwahi kusema kwa kweli hii ni kiini macho, tunaweza kusema ni Kilimo Mwisho siyo Kilimo Kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea ya Minjingu. Nimepita maeneo mbalimbali Nyanda za Juu Kusini, mbolea hii ya Minjingu haina ladha kwa walaji, walaji hawaitaki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana watalaan wameitengeneza vizuri kweli lakini kama mlaji unamwambia hii nguo ni nzuri halafu yeye mwenyewe haitaki, hivi utamlazimisha? Nadhani kuna tatizo. Wale wakulima wamelima miaka mingi, wanafahamu kila kitu siyo wajinga, tatizo lipo kwenye ile mbolea. Mimi nadhani Serikali ije na mpango mahsusituambie, hatuwezi tukawa tunapiga kelele watu wazima na wakulima wetu kuhusu mbolea hii. Mwaka jana tulipewa zoezi la kuwashawishi wananchi kuwaambia kwamba mbolea hii imefanyiwa utafiti upya, ni mbolea nzuri, ina virutubisho, imechanganywa vizuri lakini matokeo yake

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. A.N. KIBONA]

wakulima wanalia. Naomba wakulima watendewe haki, wapewe kile wanachotaka kula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu elimu. Tuna watoto wengi hasa elimu ya juu kwenye kipengele cha mikopo. Mheshimiwa Rais alishasema kwamba zipo kozi ambazo mtu akichagua kusoma atapewa mkopo. Mimi nashangaa, vijana wengi hapa nchini, maelfu hawajapewa mikopo kwenye masomo ya vipaumbele ambayo Mheshimiwa Rais alilitangazia Taifa kwamba wazazi mtoto wako akichagua ualimu, afya, kilimo na kadhalika, namhakikishia mkopo na ajira. Leo vijana wengi wanahangaika hawajapata mikopo kwa sababu ambazo henzieleweki. Naomba Serikali jie na majibu mazuri itusaidie kwa kutusaidia kwa watoto wale kwa kweli kupata mikopo yao, hapo ndipo tutasema mpango huu tunaoujadili kila tunapoelekea kwenye bajeti una mantiki, una manufaa kwa wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme. Mheshimiwa Mwenyekiti tusizungumzie maeneo yetu, lakini watu wanasimama hapa wanasma jambo la dharura linalolihusu Taifa, mimi ningeweza kusema leo jambo la dharura. Kule lleje kuna Hospitali Teule ya Wilaya (DDH) inaitwa Isoko ilikuwa inategemea umeme wa kutoka kwenye maporomoko ya mto lakini mto umekauka, hospitali toka jana wamesitisha huduma za operesheni, kupima vipimo vya *ultrasounds* na kadhalika. Hospitali hiyo ipo kilomita tano kutoka Kiwira ipelekewe umeme.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya kengele ya pili.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Wenje, Mheshimiwa Mgimwa na Mheshimiwa Mipata wajilanda.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kupata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwamba mpango huu tunaoujadili leo, unaoenda mpaka mwaka 2015, halafu mpango mpana tulionao kama Taifa ambao ni wa *Milleniam Development Goals* unaisha mwaka 2025. Mimi naamini kwamba katika mataifa yote yaliyoendelea duniani angalau wamekuwa na mpango wa muda mrefu zaidi hata miaka mia moja. Ndiyo maana hata Mzee Warioba katika ile Rasimu ya Kwanza walioitoa, walitoa mapendekezo kwamba tuweke katika Katiba ijayo malengo ya muda mrefu ya Taifa ambayo Chama chenu pia kilipinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka kusema ni kwamba, kwa mambo kama haya, ndiyo maana tumejikuta leo katika Taifa tunaongoza Taifa kwa Kauli Mbiu. Nchi hii mara unasikia MKUKUTA, mara MKURABITA, mara KILIMO KWANZA, mara leo mna kitu kinaitwa *Big Results Now*, hatujui ni *Big Results to where!* Sasa kama mnaongoza nchi kwa Kauli Mbiu, mnabadilisha Kauli Mbiu kila wakati, hii nchi haiongozwi kwa Kauli Mbiu, hii nchi inaongozwa kwa mikakati, maono, *seriousness, accountability and commitment.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana katika hili kabrasha, katika vipaumbele vilivyowekwa na Serikali vya mwaka 2014/2015, kwa mfano, katika kipengele namba moja wanasema kwamba Serikali itakuwa na mikakati ya kuboresha viwanda nchini vinavyotumia *raw materials* zinazopatikana hapa nchini na wakatoa mfano wa ngozi. Sasa nauliza, hivi viwanda mnavyoenda kuviendeleza viko wapi au ni porojo? Kwa sababu ukija Mwanza kwa mfano kulikuwa na Kiwanda kinaitwa *Tanner/eskilikuwa kina-process* ngozi, kiwanda kimekufa ninyi mnaenda kuendeleza kipi? Hii ndiyo Serikali peke yake duniani inayofanya kazi *vise versa*. Viwanda vya pamba vilivyokuwa vinachukua pamba kama

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. E. D. WENJE]

*MWATEX* mliua, sasa hii mliyoweka hapa mnaenda kuendeleza, ni vipi sasa, ni vya watu binafsi au ni vya kwenu? Ni vya akina nani hivi mnavyoenda kuendeleza kwa sababu vile vya Serikali mliua! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuua hivi viwanda, ndiyo leo imetokea kuna kundi la watu barabarani wanaitwa wamachinga na mama ntilie. Viwanda vilivyokuwa vinaajiri watu hata wale *non skilled* vyote mliua, leo tuna wamachinga wako barabarani, mnarudi tena kwa *gear zilezile* za kuwalaghai wakati ninyi ndiyo mlifanya wameenda barabarani, leo ndiyo mnaenda tena kwenye harambee eti mnawapa pesa wakati *for the first time* ninyi ndiyo mmewafanya wapo barabarani leo! Hii mnatudanganya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kujua hivi viwanda mnavyoenda kutengeneza viko wapi? Mimi nilitegemea kwa hali kama hii, kwenye huu mpango nilitegemea kwenye ile sekta ya ajira kuona *heavy investment* ya *youth fund*, muweke *commitment* ya *heavy investment* kwa *youth fund*, isaidie wamachinga, isaidie bodaboda, isaidie vijana wanaotoka vyuo vikuu ambao hawana ajira, kuwe na *heavy investment* kwenye *youth fund* lakini sijaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zingine kama Kenya walikuja na *project* inaitwa Kazi kwa Vijana *Project*, ambayo ilikuwa inasaidia vijana kama hawa ili tusiwe na watu wengi wanaoendesha pikipiki wanakufa kila siku. Hawa wanaoendesha pikipiki, ninyi ndiyo mmesababisha leo Watanzania wanaendesha pikipiki kwa sababu viwanda mliua, kwa hiyo hawana ajira wanaendesha pikipiki. Halafu mnakuja hapa mnatudanganya tena eti mmeondoa ushuru kwenye pikipiki, hii ni kamba, mnatupiga kamba! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nilitegemea kuona, mimi Mwanza watu wanani pigia kelele kila siku, *TANESCO* wanachukua pesa za wananchi wanaotaka kuvutiwa umeme, wanakaa nazo hata miezi sita, wanafanya nazo biashara, wanakopa pesa kutoka kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E. D. WENJE]

wananchi hawapeleki umeme. Mtu anakaa mpaka miezi sita! Nilitegemea kuona *heavy investment* kwa TANESCO inayoenda ku-reform TANESCO, ili kama Mtanzania ameomba umeme apewe hata *within two weeks*. Sasa kuna mtu anachukua mkopo ili avute umeme, aanze biashara aliye na ule mkopo, kwa hiyo mnafilisi hata Watanzania mnawakopa pesa kupitia TANESCO, hizi pesa sijui mnapeleka wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine katika shabaha, hizi shabaha zimeandikwa kwenye ukurasa wa 11, kipengele cha (b) kinasema Serikali itaendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei. Mimi ninawaambieni kwamba hauwezi ukadhibiti mfumuko wa bei kama unaongeza kodi kwenye mafuta kila mwaka. Kila mwaka unaongeza kodi kwenye mafuta, ukishaongeza kodi kwenye mafuta *literally* unaenda kuathiri bei ya vitu vyote. Ndiyo maana leo Mwanza ninapotoka sukari ni buku mbili, buku mbili jero ndiyo bei ya sukari kule ninapotoka. Bei ya sabuni ni ngumu. Kwa hiyo, kimsingi mfumuko wa bei unaendelea kwa sababu kila mwaka ninyi mnaongeza kodi kwenye mafuta. *That way* mafuta ina *effect* kila sekta. Kwa hiyo, hamuwezi kudhibiti, mnatudanganya na ndiyo maana bei ya vitu huko mitaani tunakotoka bado ni ghalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine katika hicho kipengele cha (c) wanasema kwamba Serikali itajitahidi kuongeza mapato kufikia angalau asilimia 19.1 ya *GDP*. Hatupingi hili lakini angalieni ni utaratibu gani mtatumia kuongeza mapato bila kuumiza wananchi. Kwa shabaha kama hizi ndiyo maana leo mmelazimika kuongeza na kodi kwenye laini ya simu ambayo Watanzania wote wanapinga halifu ninyi mmeingiza pamba masikioni mnajifanya hamuoni kwa sababu ninyi mna mapato makubwa. Kwa hiyo, *what people are going through there* ninyi hamjui kwa sababu mna mapato makubwa. Tulileta mapendekezo hapa hata kwenye migodi, mafuta yanayoenda kwenye migodi yote Tanzania, *thousands and thousands of litres* wanazotumia ni *tax free*. Sasa kwa nini msiongeze kodi huko ili watu wapumue?

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. E. D. WENJE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika misingi hii ya sera, katika kipengele cha (i) wamesema kuboresha biashara. Mwanza ninapotoka na hata Mbeya juzi wafanyabiashara wameandamana, Mwanza wamenituma nije niwaambieni, hawapendi utaratibu mlioweka wa wao kupata mashine mnaita *EFD*. Hizi mashine za *EFD* ni biashara ya nani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashine hii mtu anaenda ananunua shilingi laki nane, mtaji wa mtu ni shilingi milioni moja, atoe shilingi laki nane aende anunue mashine eti mtakuja kukata huku kwenye kodi. Watanzania wafanyabiashara na wa Mwanza ninakotoka wanasema, mngewaruhusu wanunue popote pale wanapotaka kwenye *market price* halafu ije iwe *configured na system* ya *TRA*. Sasa hii *deal/mmeileta* kama mlivyoleta ile kitu ya *ma-bus* inaitwa *speed governor*. *Speed governor* ilikuwa ni biashara ya watu na hii pia imekuwa biashara ya watu na ndiyo maana mnawang'ang'aniza kwenda kununua palepale kwa wale mnaopiga nao *deal*, hii siyo sawasawa. Ninyi mnataka wafanyabiashara waandamane kila kona ndiyo mjue hawataki hili suala! Waruhusuni, kama ni biashara zenu, hii si sawasawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Katika hiyo misingi kipengele (g) wanasema kwamba mnataka kupeleka madaraka kwa wananchi, madaraka mnapelekaje kwa wananchi, hii ni porojo. *The only way* ya kupeleka madaraka kwa wananchi *is through full devolution system* ambayo sisi kama CHADEMA kama chama ndiyo tunaisimamia. Sasa ninyi mnapeleka madaraka kwa wananchi wakati kule Wabunge wanasema hapa kila siku, wakitaka hata Mwenyekiti wa Mtaa au wa Kijiji afukuzwe kazi, *DC* anaenda anarudisha halafu ninyi mnapeleka madarakani gani kwa wananchi kwa stahili hii? Hii ni porojo nytingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa tano, *paragraph 1.7*, wamezungumzia biashara nje. Hapa kuna lugha moja imetumika, ni lugha ya kimaskini, msipobadilisha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E. D. WENJE]

vitu kama hivi, mdomo huumba, mtaendelea kuwa maskini hivihivi yaani kuna ongezeko...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele yenyewe inalia kidogo lakini ni ya pili?

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Ni ya pili?

**WABUNGE FULANI:** Ya kwanza.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Ya kwanza au ya pili?

**MWENYEKITI:** Ya pili.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naheshimu Kiti chako. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Kengele yenyewe haigongi vizuri sasa hivi. Ahsante sana Mheshimiwa Wenje. Sasa nimwite Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa atafuatiwa na Mheshimiwa Mipata. Mheshimiwa Mgimwa! Yupo au hayupo?

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**MWENYEKITI:** Kama hayupo Mheshimiwa Mipata, atafuatiwa na Mheshimiwa Barwany na Mheshimiwa Kafulila.

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nkichangie katika Mpango wetu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mchango wangu kwa ridhaa yako, naomba nitoe tamko la rambirambi kwa tukio bayo lililotokea kwa wananchi wa Kijiji cha Chala kwa kumpoteza mfanyakia shara maarufu, Bwana John Mwanakatwe ambaye ametuacha usiku wa kuamkia tarehe

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. J. MIPATA]

27/10/2013. Mungu iweke roho yake mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu, katika eneo la utekelezaji, nikianzia na barabara, mimi sijaridhishwa sana na kasi ya utekelezaji wa ujenzi wa barabara zinazounganisha Mikoa ambapo unapatikana katika ukurasa wa 14. Katika ujenzi wa barabara inayotoka Sumbawanga kwenda Mpanda kupita Kanazi, kasi yake inaenda taratibu mno na haishawishi wananchi wa eneo linalohusika. Kwa hiyo, tunapoweka mipango, utekelezaji wake tunataka uende kwa kasi inayotakiwa. Wananchi mara zote tunapopita wanatuhoji kwamba kwa kasi hii mnategemea mwaka 2015 barabara hii itakuwa imeisha. Kwa hiyo, naomba Serikali itie msukumo katika ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasema Mkoa wa Rukwa unachangia sana katika mambo mbalimbali ikiwemo kukabiliana na njaa katika nchi hii. Sasa inapofika miradi yake inaenda kwa kusuasua ukilinganisha na maeneo mengine, hili jambo haliwezi kukubalika, naomba kasi iongezwe. Pia Mheshimiwa Waziri anayehusika na suala hili tunamwomba atembelee miradi hii kila mahali, akitembelea huwa kasi inaongezeka. Kwa hiyo, ujenzi ule hauridhishi kabisa, hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika suala la barabara hii na barabara zote nchini, lazima mpango ujielekeze vilevile katika kujibu ahadi za Mheshimiwa Rais. Alipokuja katika Wilaya ya Nkansi aliweza kuzungumzia juu ya barabara ambazo zinaunganisha maeneo ya mwambao ambayo ni nchi jirani na zinatajwa vizuri sana katika mpango huu kwamba kuna utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba njia za mipakani zinaimarishwa lakini barabara ya Nkana-Kala, Kitosi-Wampembe na Namanyele-Minde bado hazijazingatiwa katika mpango wowote, huu nao vilevile tunaoutarajia. Naomba Serikali ihakikishe kwamba ahadi za Mheshimiwa Rais zinazingatiwa, mpango huu lazima ujibu ahadi za Mheshimiwa Rais ili tuweze kupata maendeleo ya haraka na kujibu llani ya Chama cha Mapinduzi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. J. MIPATA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme. Kweli umeme umetekelezwa na umefika Namanyele, lakini yapo maeneo mbalimbali ambayo hayajapata umeme na wananchi wanahoji leo. Kwa hiyo, kasi ndogo ya kupeleka umeme katika maeneo yetu, inachelewesha maendeleo pia. Wananchi wanajiuliza umeme kufika tu si tatizo, lakini je, unatawanywa katika maeneo ya vijiji vinavyohusika ili wananchi waweze kuutumia? Yapo maeneo kwa mfano mwambao wa Ziwa Tanganyika, kupitia *REA* lazima umeme ufile katika maeneo yale ili kuwaokoa na umaskini wa kipato ambao unawabana wananchi wale. Wale wananchi wana rasilimali zinawazunguka, mpango unajibu hilo? Mimi sijaona mahali ambapo mpango huu unajibu suala la kutawanya umeme katika maeneo ambayo wananchi wamebanwa, ungepelekwa ungeweza kuwa ni ukombozi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo. Kupitia Suma JKT, tulipata matumaini makubwa sana hivi karibuni. Tukapatna matrekta lakini sasa naona kama haisaidiwi. Matrekta yale yameshakwisha na sasa hayasambazwi tena, nadhani Suma JKT haisaidiwi vya kutosha ili hayo matrekta yaweze kupatikana tena. Mikoa ya pembezoni kama ya Rukwa na mingineyo ukuaji wa uchumi wake unategemea kilimo, sasa ni lazima ijielekeze kuhakikisha kwamba mapinduzi ya kilimo yanaenda sambamba na *mechanization* katika kilimo, bila kufanya hivyo hatuwezi kuinua kilimo na tunajua mzigo ambao kilimo kinauchukua katika nchi hii. Watanzania wengi wanaajiriwa na kilimo, sasa kama tunategemea majembe ya mkono, hatutaweza kufanikiwa kuleta tija inayotarajwa katika uchumi na vilevile katika kuinua wananchi katika hali ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wananchi wamekopwa mazao yao na tumeピta huko vijiji wanauliza, Serikali inatukopa mazao na huku inajua hali zetu na bado inatuambia tunatakiwa sasa tulime ili tuijinue na tuinue uchumi wa nchi yetu, inawezekanaje? Tafsiri yake hapo ikoje? Kwa hiyo, tunaiombwa Serikali nayo iangalie.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. J. MIPATAJ]

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, yapo maeneo ambayo yameelekezwa katika kuimarisha kilimo cha umwagilajiji hasa katika maeneo ya pembezoni. Katika Mkoa wa Rukwa kuna maeneo ya Kate na Rwamfi, vigezo vyote vilivyokuwa vinatarajiwa vimeshafikiwa lakini mpaka sasa bado miradi hiyo hajaanza kuvuna pesa kutoka Serikalini. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ianze kuona hilo. Katika kuimarisha uchumi mpango lazima ujibu mambo muhimu kama hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine muhimu sana, ni suala la maji. Suala la maji limeelezwa sana katika mpango huu kwamba ni jambo muhimu kwa maji mijini na maji vijijini. Mji wa Namanyele leo pamoja na ahadi nyingi za Serikali bado hawana matumaini ya kupata maji wakati wote. Tunaomba, kupitia mpango huu tupate majibu ya uhakika kuhakikisha kwamba maji mjini Namanyele yanapatikana lakini siyo mjini Namanyele tu na maeneo mengine yoyote ya vijijini hasa kupitia miradi ya vijiji kumi kwa kila Halmashauri ili wananchi waweze kuondokana na matatizo makubwa ya ukosefu wa maji pamoja na kupambana na maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ni suala la mawasiliano. Mawasiliano leo lazima tuyatafsiri katika sura ya huduma muhimu sana hasa katika maeneo ya pembezoni. Eneo lote la Ziwa Tanganyika limekaa bila mawasiliano. Kuna Tarafa moja inaitwa Wampembe, imekaa haina mawasiliano kabisa. Zipo Kata za Kala, Minde na Wampembe zote hazina mawasiliano ya barabara wala mawasiliano ya simu. Naiomba Serikali na kwa kupitia mpango huu na tukijua mpango huu ndiyo lala salama katika utekelezaji wake, maana mpango unaokuja hatutausimamia utekelezaji wake, ujibu matatizo haya ya wananchi itaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Asante sana. Sasa nilisema namwita Mheshimiwa Barwany atafuatiwa na Mheshimiwa Kafulila, Mheshimiwa Anna Abdallah na Mheshimiwa Shekifu.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ambayo iko mbele yetu sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mpango ambao sasa hivi umeletwa, ni Mpango wa Maendeleo ambao unaishia mwaka 2025. Hii ni awamu yake ya kwanza. Katika kikao kama hiki tulipokuwa tunajadili mpango wa mwanzo, tulizungumza ni namna gani Sera za Kitifa zinaweza kusimamia mpango huu. Mashaka makubwa kwa Watanzania sasa na hata sisi Wabunge ni kwamba iipango hii inakwenda kwa mujibu wa awamu zilizopo madarakani. Tunaweza tukasema kwamba Mpango huu ni Mpango wa Awamu ya Nne. Hatuna uhakika hiyo Serikali ijayo ya Awamu ya Tano itakuja na mpango gani. Ni vema suala hili likaangaliwa kwa makini kwani kuna mashaka. Kuna mipango mingi ambayo imekuja kila awamu na huu sasa hivi ni Mpango huu wa Awamu ya Nne, sijui hatma itakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ambalo linaweza likaleta maendeleo katika nchi yoyote duniani, ni mzalendo wananchi wake. Wananchi wanatakiwa wawe wazalendo na tunaimbiwa hapa tuwe wazalendo, tuweze kuleta maendeleo katika taifa letu lakini uzalendo huu unapatikanaje? Mtanzania au mwananchi yeoyote duniani anakuwaje mzalendo? Lazima kwanza nchi hiyo iwe na utawala wa sheria, iwe na utawala bora na demokrasia. Katika nchi kama hiyo, kwa vyovyyote vile wananchi wake watakuwa wazalendo ndani ya Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunashuhudia mambo mangapi makubwa ambayo yanawafanya Watanzania washindwe kuwa wazalendo, washindwe kuisimamia rasilimali ya Taifa lao? Tunaona ni namna gani Watanzania leo wanavyopata kipigo, wanavyonyonyaswa na Jeshi la Polisi katika Taifa lao, unaondolewa kabisa uzalendo. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. S. K. BARWANY]

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashuhudia ni namna gani ufisadi, rushwa ambao umekithiri katika Taifa letu, ni namna gani leo tukawataka Watanzania leo wawe wazalendo, wasimamie rasilimali ya nchi yao? Hili linaleta mashaka makubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi tukawalazimisha Watanzania wetu wakawa wazalendo katika sura ya Taifa linavyokwenda sasa hivi. Kwani tunashuhudia leo, tuna taarifa kutoka katika maeneo mbalimbali jinsi wananchi wetu wanavyopata vipigo katika Operesheni Kimbunga. Kwa namna yoyote ile wanaskia kwamba kuna watu wanauza meno ya tembo katika mataifa mbalimbali huko nje lakini hatua hazichukuliwi lakini yule mwananchi wa kijiji ambaye tayari angedhibitiwa tu kwa kufuata utaratibu wa sheria, lakini tumeshindwa kuwafanya wananchi wetu wawe wazalendo katika kusimamia rasilimali ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishwaji wa jamii katika maendeleo ya Taifa lao. Hili nalo lina nafasi kubwa ya maendeleo katika nchi. Leo katika vyombo mbalimbali vya habari duniani tunaambiwa kwamba Serikali ya Dar es Salaam, mimi najiuliza, tunapoambiwa Serikali ya Dar es Salaama maana yake nini? Serikali ya Dar es Salaam wanamaanisha kwamba maamuzi yote ya Kitaifa, maamuzi yote ya maendeleo, ushirikishwaji, sauti inatoka Dar es Salaam peke yake. Wananchi katika ngazi za chini katika Halmashauri, Mikoa, Kata hawashirikishwi, wananchi wanateremshiwa tu mipango. Hata zile taratibu za kuwafanya wananchi washiriki katika mijadala ya maendeleo katika maeneo yao, hilo halipo katika utaifa wetu. Kwa maana hiyo, ushirikishwaji wa jamii katika maendeleo ya Taifa lao, hili limepotea kabisa katika historia ya Taifa letu. Leo tuna miaka 50 lakini kule nyuma tuliona mwananchi anashirikishwa katika mipango mbalimbali ya maendeleo. Tunazungumza mpango huu hapa tu Bungeni lakini ukimwuliza mwananchi wa chini kule anaufahamu vipi mpango huu, kwake ataona kama mbuzi unampigia gitaa tu, hajui kinachozungumzwa ni kitu gani. (*Makofî*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. K. BARWANY]

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mambo mengi ambayo tayari yanaonyesha kwamba mpango mzima huu unategemea pato la Taifa ili iweze kusimamia mpango uweze kuimarika. Unaangalia maeneo ambayo tayari ni vyanzo vyta mapato katika Taifa letu, kama Taifa, Serikali imesimamiaje maeneo yale? Leo tunazungumzia suala zima la kilimo. Katika nchi za SADC tayari kulikuwa na Azimio kwamba katika bajeti za Serikali, tupange asilimia 10 ya bajeti ya Serikali iende katika kilimo. Hebu tuangalie katika bajeti zetu mpaka sasa, ni asilimia ngapi ya bajeti ambayo inakwenda katika kilimo. Watanzania zaidi asilimia 80 ambao wako kule vijjini wanategemea kilimo. Watu wanalamika leo, pembejeo hakuna, tatizo la ardhi limekithiri katika maeneo mbalimbali, sasa vitu kama hivi, huwezi kuwa na asilimia 80 isiwe na mchango thabiti ambao umeandalila na Serikali kwa maendeleo ya Taifa hilo. Hivyo mzigo wa asilimia 80 ya Watanzania bado wanategemea sehemu ndogo ya mapato kuendeleza Taifa lao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna moja au nyininge, maendeleo yoyote katika nchi lazima tuhakikishe kwamba asilimia kubwa ya wananchi wake wanashirikishwa katika mpango mzima. Mpango wetu wa maendeleo ambao tayari unaweza kuwa ni chanzo kikubwa cha mapato ni kilimo. Tunategemea kilimo cha mvua mpaka sasa hivi. Juzi tulikuwa tukipitisha Sheria hapa ya Umwagiliaji, lakini sioni katika Mpango, imeelezwaje katika suala zima la umwagiliaji ambao unaweza kusaidia mpango katika maendeleo ya kilimo katika Taifa letu. Haya ni matatizo ambayo bado tunazungumzia tu kama nadharia, haionyeshi kwamba tuna mkakati wa kweli wa makusudi kabisa wa kuleta maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maendeleo ya namna mbili katika mataifa yote duniani. Kuna maendeleo watu na kuna maendeleo ya vitu. Tunaweza tukawa na miundombinu mingi, tukajenga barabara, tukafanya kila kitu lakini bado kama mwananchi wa kawaida akaishi chini ya umaskini, miundombinu ile, utajiri ule mwananchi wa kawaida haumgusi kabisa. Leo tunasema kwamba Mtanzania anaishi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. S. K. BARWANY]

chini ya dola moja. Hebu tufanye tathmini, dola moja ni Sh.1,600, Mtanzania wa kawaida anaishije chini ya Sh.1,600? Watanzania zaidi ya asilimia 60 katika Taifa letu wanaishi chini ya dola moja. Katika mazingira haya ambayo tunayaona sasa, hivi wananchi wanashiriki vipi katika kuleta maendeleo ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sula la deni la Taifa, linaathiri uchumi wa nchi. Limeshakuwa mazoea sasa, nchi inapoona kwamba ina ina tatizo la fedha, basi inakimbilia katika mataifa kwenda kukopa fedha lakini uwezekano wa kulipa fedha hizi ukoje? Bado Serikali hajatueleza mpaka sasa, kama tukisimamisha leo tusikope madeni haya nje, tutachukua muda gani kulipa deni hili na mkakati wa Serikali ukoje? Tunaambiwa tu nchi inakopesheka, inakopesheka kwa namna gani? Utaratibu gani unatumika katika kulipa madeni hayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusimame leo tuseme tusikope madeni haya, tusiwaachie urithi wa madeni watoto wetu. Nchi zingine zinawaachia watoto wao maendeleo lakini Taifa letu linawaachia urithi wa madeni. Je, tufikirie kwamba tunasimamisha sasa hatukopi nchi yoyote ile, hatuendi kukopa katika benki yoyote ile kwa sababu benki zinafanya biashara. Unapokwenda kukopa watakulubalia tu, hawana matatizo na wewe, lakini je, tukisimamisha leo tutachukua muda gani kulipa madeni hayo? Bado hatujawa na mkakati wa kina kabisa wa kuyaangalia madeni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni madeni ya nje lakini tuangalie madeni ya ndani. Katika Majimbo yetu, wananchi wanalalamika, wamekopesha Serikali mamilioni ya pesa, wamekopesha Magereza, shule na maeneo mbalimbali lakini zaidi ya miaka mitano, sita, kumi wakandarasi hawajalipwa, wale ambaao tayari wametoa huduma za jamii kule hawajalipwa pesa zao. Unamtaka yule awe mzalendo kwa taifa lake, atakuwaje mzalendo mtu kama yule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo muhimu tunaweza tukayaangalia katika mipango hii ili tuweze kuona

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. K. BARWANY]

kwamba mipango hii kweli inaweza kukidhi haja au ni katika kutengeneza tu mazingira tuone kwamba Serikali inashughulika na maendeleo ya nchi lakini katika sura hii bado haituletei picha kamili ya kuona kwamba tunaweza tukatoka hapa kwenda mbele kuitia mbele kuitia mipango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini nasema siungi mkono hoja mpaka nipate ufanuzi wa hoja hizi. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nashukuru na muda wenyewe ulikwisha. Sasa ni Mheshimiwa Kafulila, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Abdallah na Mheshimiwa Shekifu atamalizia.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja muhimu kabisa ambayo inahusu Mpango wa nchi, kimsingi ni Mpango wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijachangia, naomba niwape pole ndugu zangu wa Kigoma, kufuatia udhaifu mkubwa wa utekelezaji wa *Operation Kimbunga* ambao kwa sehemu kubwa umevunja haki za kinadamu na ninazidi kuunga mkono kwa uamuzi wao wa kuiburuzza Serikali Mahakamani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote tunapozungumza Mpango wa Bajeti, kimsingi tunatazama mambo mahsus ambayo yanahu su uchumi wa sasa kuelekea huko tunakokwenda kwa miaka mingi. Siyo tu kwamba mpango wa mwaka mmoja unapaswa kujielekeza kwenye matukio ya mwaka mmoja, lakini pia una *define* mwelekeo wa Taifa kwa miaka mingi ya baadaye. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanafahamu na dunia inafahamu kwamba *position* ya Tanzania leo kama tungepata viongozi wenye kujua fursa hizi tulizonazo, hii ilipaswa kuwa mionganoni mwa nchi kubwa sana duniani.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. Z. KAFULILA]

Bahati mbaya sana bado Watanzania wanakabiliwa na matatizo ambayo kimsingi siyo saizi yao kuyakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Marekani, ukizungumza na *investors* wa Marekani, ukizungumza na China na hata Ulaya, haya ma-*giant* matatu katika dunia yaani Ulaya, China na Amerika, wanatazama Bara la Afrika kama Bara ambalo lina ukuaji wa uchumi. Kwa hiyo, ma-*giant* haya matatu wanaangalia namna gani ya kujielekeza na kushindana katika biashara ya Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiwatazama Wamarekani wanapotazama Afrika, wanatazama Afrika Kusini na Tanzania. Ukiangalia Ulaya na China, wakizungumza uchumi wa Afrika na nafasi yao ya uwekezaji katika Afrika, wanatazama Afrika Kusini na Tanzania na ndiyo maana umesikia China imeamua kutengeneza *Logistic Centre Tanzania* itakayoyafanya Mataifa mengine ya Afrika badala ya kwenda kununua bidhaa China basi wanunue China kupitia Tanzania. Hii ni *opportunity* kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bahati mbaya sana sioni viongozi ambao wanatazama fursa kubwa kama hiyo. Tunapaswa kama Tanzania tuwe na mkakati ambao unatuongoza tushirikiane vipi na Marekani, China na Ulaya. Bahati mbaya viongozi wetu kila siku wanasaifiri wanakwenda kushirikishwa vikao badala ya wao kwenda na agenda ya kuwashirikisha Ulaya, Marekani na China, wanakuwa wao umeitwa China leo, kesho umeitwa Ulaya na keshokutwa umeitwa Marekani, ni lazima Tume ya Mipango i-*develop* mkakati wa ushirika kati ya Tanzania na hizi *giants* tatu za dunia ili kusudi Taifa hili litoke hapa lilipo na liweze kusonga mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni changamoto namba moja na msingi wa changamoto hii ni kwamba hatuna watu ambao wanapoteza muda wao kufanya kazi za Taifa hili. Tuna viongozi wengi ambao muda wanaoutenga kufanya kazi za Serikali, ni 10% mpaka 20% lakini wengi muda wao wanautumia kufanya biashara na kwenye kufanya mambo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. Z. KAFULILA]

yao ya kawaida badala ya kutenga muda wa kutosha wa kwenye kufanya kazi za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu hiyo, tumekuwa kila siku tunapanga mipango ambayo haitekelezwi. Kila siku kuna matukio ya watu kuchukua fedha za Serikali na wakihojiwa hawahitaji kujibu na wakati mwingine uchunguzi unafanyika na bado hawajibu. Nitatoa mfano mmoja, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Uchumi na Biashara. Kuna takribani zaidi ya shilingi bilioni 200 ambazo zilipotea kwenye Mpango wa *Commodity Import Support*, mpaka juzi *TRA* wanaonyesha kwamba kiasi ambacho kimerejeshwa ni shilingi bilioni 4.2 tu kati ya shilingi bilioni 216. Kama mabilioni haya yatakuwa yanapotea na hakuna hatua yoyote ambayo inachukuliwa, tangu 2008 mpaka leo *TRA* wamekusanya *only 4.2 billion* katи ya shilingi bilioni 216, tunapanga nini hapa kama siyo kuchoshana? Haiwezekani! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipanga hapa *Stimulus Package*, mpango ambao ni wa takribani shilingi *1.7 trillion*, mpaka kesho, watu waliofaidika na huo mpango, uliagiza Spika hapa kwamba majina yaje Bungeni, tujue zimetumikaje lakini mpaka leo Serikali haijaleta na hawataki kuleta. Shilingi *1.7 trillion is a lot of money*. Sasa tunapanga hapa tunachoshana, kuna watu wana kiburi, wana jeuri kwa sababu wanahisi hawawezi kuongoka madarakani, lakini laiti kama wangekuwa wanajua wanaweza wakaondolewa madarakani wasinge kuwa wana jeuri ya kiasi hiki, haiwezekani! Nchi hii kuna umaskini uliopitiliza, inawezekana ukiwa kwenye *ACH*apa usijue, nenda vijijini kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ambayo ina kila sababu ya kuwa nchi bora duniani lakini tuna mkosi wa viongozi, tuna watu ambao hawana dhamira kabisa ya uongozi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Ziwa Tanganyika nimezungumza siku zote kwamba kero namba moja inayowakabili Watanzania, kwa mujibu wa *Synovate*

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. Z. KAFULILA]

kampuni ya tano kwa utafiti duniani, ni maji tangu mwaka 2009 lakini mpaka leo tatizo la maji limekosa majibu. Mimi Jimboni kwangu inafika mahali nashindwa nifanyaje. Dunia nzima ina takribani kilometra za maji au *fresh water* za ujazo wa milioni 35. Ziwa Tanzania peke yake lina kilomita za ujazo milioni 5,800,000 maana yake 17% ya *fresh wateryote* duniani ipo Ziwa Tanganyika Kigoma lakini watu wako vijiji mita mia moja, umbali sawa na uwanja wa mpira lakini hawana mabomba ya maji, Serikali gani hii? Utawaambia nini ili waone kwamba wewe unawathamini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna viongozi ambao hawachukui hatua. Leo wamezungumza wenzangu, mmeanzisha *operation* ambayo kimsingi imeendesha mauaji na mionganoni mwa Majimbo ambayo mtu amekufa ni Jimbo langu kwenye Kata ya Kalya. Mnaanzisha *operation* za kihuni, mnaua watu kwa sababu za vitu ambavyo mmeshindwa kuvitatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wafugaji wanateswa kwenye nchi hii utafikiri ni wakimbizi. Ethiopia ng'ombe ni uwekezaji mkubwa lakini Tanzania ng'ombe ni kero na wafugaji wanakimbizwa utafikiri wao ni Wahutu wako Tanzania, utafikiri wao ni wahamiaji haramu, inawezekana wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa misamaha na inajenga mazingira mazuri kwa wawekezaji kwenye dhahabu ambao ni wezi wanatafuna Taifa hili kwa kusamehewa kodi lakini wafugaji inashindwa kuwatengeneza wawe wawekezaji. Hili ni suala la akili tu kwamba huyu mfugaji anapaswa atazamwe, wana upungufu wao lakini ni wajibu wa Serikali kupunguza upungufu wao. Wana upungufu wao lakini kazi ya Serikali ni kuangalia ni kwa namna gani inaweza ikatatua changamoto ambazo zinawakabili na kuwafanya wawe wawekezaji katika Taifa hili. Nchi ya tatu kwa ng'ombe nyingi lakini bado kuna maziwa yanaagizwa kutoka Kenya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. Z. KAFULILA]

na nchi nyingine, bado kuna nyama zinaagizwa kutoka Kenya na nchi nyingine, mnahitaji nini?

**MBUNGE FULANI:** Hata samaki.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba tutaendelea kuzungumza kwa sababu miaka ya uchaguzi hajifika, lakini ukweli ni kwamba hakuna kinachotekelawa hapa, hali ya nchi hii bado iko chini sana. Ukiangalia uchumi, mwekezaji ye yote anayekwenda kuwekeza kwenye Taifa moja ya eneo ambalo anaangalia ni *stock market* ikoje, leo *stock market* ya Tanzania ni *only 10%* ya *GDP* lakini Kenya jirani pale *40%* ya *GDP*....

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila, hiyo ni kengele ya pili. Naomba hiyo kengele muongeze sauti. Ahsante sana na sasa namwita Mheshimiwa Anna Abdallah na atafuatiwa na Mheshimiwa Henry D. Shekifu.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hoja muhimu ya mapendekezo ya Mpango wetu wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nishukuru sana ratiba hii ya Bunge ambayo kwa kweli sasa ndiyo tunaanza *budget cycle* ya mpango huu halafu tunaendelea. Hili ni jambo la kushukuru kwa sababu hata Serikali imesikia na wamewahisha kuuleta huu mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naomba niipongeze Kamati ya Bajeti, mimi nafikiri Kamati ya Bajeti imetuletea mipango mle ndani, wametoa mapendekezo mazuri sana, nafikiri mapendekezo yale lazima tuyaunge mkono haya mengine tunayoyasema ni katika kupamba gazeti lakini nafikiri wenzetu wa Kamati wametufanya kazi nzuri sana. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. A. M. ABDALLAH]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimekuwa nikifuutilia kitabu hiki cha hotuba ya Waziri halafu ndiyo ninaangalia ameandika nini katika mpango. Naomba nianzie katika utangulizi, aya ya kwanza, katika mapendekezo ya mpango anasema; vitu vinavyowekewa maendeleo ya miaka mitano ni kama yafuatavyo. Kwanza, ni miundombinu, mbili ni kilimo, tatu ni viwanda vinavyotumia malighafi za ndani na kuongeza thamani. Kwa hiyo, niliposoma hapa, nikaenda kwenye mpango kuangalia hivyo viwanda ni viwanda gani? Nataka tu nizungumzia viwanda vya ubanguaji wa korosho. Katika viwanda ambavyo vinaweza kuleta matokeo ya haraka sana ni viwanda vya korosho lakini humu ndani havikuguswa mahali popote kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana viwanda hivi siyo kwamba hatuna viwo hapa nchini na ni 12, vilijengwa na Serikali baadaye vikabinafsishwa na hao walionunua wanaviatamia kama mayai, mwisho viwanda vile vinakuwa kama mayai viza tu sasa lakini vinaatamiwa. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza humu ndani na tumeeleza kwamba lazima tuwe na mpango vile viwanda ama virejeshwe Serikali kwa sababu mpango wa ubanguaji, na wapo watu wengine wako tayari lakini tunapata shida kwelikweli. Katika viwanda ambavyo vinaweza vikaleta manufaa kwa mazao yetu kwa haraka ni korosho kwa sababu ukiisha kuibangua tunatafuna sisi wenyewe hapa na majirani zetu wengi wanaitaka lakini pia na dunia inataka korosho lakini naona hapa hata kule ku-mention ya korosho hakuna. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye ukurasa wa 48, maeneo muhimu ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo, ameeleza vizuri, Ibara ya 3.1, kwanza kuna suala la kudumisha amani na utawala bora kama msingi muhimu wa kuwezesha uzalishaji mali. Kweli amani na utawala bora ni vitu vya msingi lakini tunaipataje amani? Kuna vyombo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. M. ABDALLAH]

ambavyo vinasimamia haya mambo, humu ndani havikuguswa kabisa kana kwamba havipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakaa hapa tunavilaumu lakini kwenye mpango humu tunazungumzia amani, hivi hii amani itakujaje kwa sababu kuna watu wengine, haiwezekani tu utawala bora na amani, vyombo hivi lazima viwezeshe hwe kusimamia hiyo amani kwa sababu kuna wengine wanavunja tu amani kwa makusudi lakini kwa kuwa chombo hakina tena uwezo wa kuchukua hatua basi mambo yanakwenda hivihivi shagalabaghala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kote lakini sioni mahali ambapo vyombo vya Ulinzi na Usalama vinapewa nafasi. Hivi hawa wawekezaji watakuja kuwekeza hapa bila kuwa na vyombo imara? Hicho kilimo tunachokitaka humu tutakwenda kulima kama hakuna vyombo imara vya kuleta amani na utulivu nchini? Mimi nafikiri hilljambo pia lina kasoro na kama tunafuata miradi ya kuambiwa na wakubwa, mimi nafikiri hapa tunakosea. Sisi tunapaswa katika miradi ya nchi yetu tuhakikishe kwamba vyombo vyetu tena mimi sisemei tu labda Polisi na Jeshi lakini mpaka Mahakama, vyote hivi ni vyombo vitakavyodumisha amani hapa nchini. Mimi ni-declare interest ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, inatisha, *OCD* leo anapata lita tano za mafuta kwa siku sasa lita tano sijui atakwenda wapi? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Tat!

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Siyo tano ni tatu! Atafanya kazi gani? Halafu tunawalaumu? Sasa hivi tuna matishio haya ya majirani, wahamiaji haramu, Alshabaab na kadhalika wote wanatunyemelea...

**MBUNGE FULANI:** Maandamano!

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Maandamano na kadhalika, yote hayo ni fujo tu zinazofanywa hapa nchini.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. A. M. ABDALLAH]

Hivi vyombo tunaviwezesha vipi kwani havimo kabisa katika Mpango, mimi sijui kama kuna Mpango mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 49, unazungumzia juu ya kutumia fursa ya ongezeko la watu nchini kuleta manufaa ya kiuchumi yaani *demographic dividend* kwa kupunguza kiwango cha utegemezi yaani uwiano kati ya watoto ambao ni tegemezi na idadi ya watu wanaofanya kazi. Nimeangalia kwenye kitabu chenyewe tunasema nini juu ya jambo hili? Wenzetu wa Kamati ya Bajeti wametuambia wafanyabiashara wanaolipa kodi ni 1.7 million na milioni tano ni wafanyakazi katika watu milioni 44.9 lakini wanaolipa kodi ni chini ya milioni sita, acha watoto wadogo walio wengi. Hasa katika suala la kwamba tuna watoto wengi zaidi kuliko watu wazima wafanyakazi nalo lenyewe tunasema ni kitu kitakachotuwezesha kuendelea? Mimi lazima tueleze kabisa hili jambo ni tatizo ambalo ni lazima tuli-address, suala la walipa kodi wafanyakazi yaani sasa hivi wanaofanya kazi, kazi ni zote hata za kulima, ni wachache kuliko wanaokula, tunaowalisha ni wengi. Walio wengi hasa wakulima wanazeeka, hakuna vijana wanaolima. Sasa wanaolima ni wazee tena ni wachache halafu wanaokula ni wengi mno kuliko ilivyo kawaida. Kwa hiyo, hili nalo tulieleze na hata hao wenye uwezo wa kufanya kazi walipa kodi ni wachache sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutumia fursa ya ongezeko kubwa la watu mijini na kufanya miji kuwa vitovu endelevu vya ubunifu. Mimi nina mfano mzuri sana wa Mtwara. Mtwara sasa hivi tunaita "Mtwara Kuchele", gesi ipo na kuna kipindi kinaitwa Baragumu la Msimbati na kadhalika. Ule mji sasa unaanza kuwa wa hovskyo kweli, Mkoa umejitahidi wakawekea utaratibu wa namna ya kuendeleza ule mji, viwanda vikae wapi, maana kwa ajili ya gesi tu hata sasa hivi ni tatizo *influx* ni kubwa lakini ule mpango mpaka leo umeletwa Serikalini ili ukubaliwe ama walete mapendekezo lakini hakuna mpaka leo tangu mwaka jana. Sasa hivi tunakwenda wapi? Sasa hiyo gesi itachimbwa, viwanda vitajengwaa na kadhalika, mji ule tusipokubaliwa ikawa *planned area* kama ilivyokuwa imependekezwa, kwa kweli tutashindwa hata kuwa na maeneo ya viwanda, makazi,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. M. ABDALLAH]

michezo na kadhalika. Kwa hiyo, hilo nalo ni tatizo la upangaji wa mipango, lazima muangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia vilevile katika mpango huu, hii gesi na kadhalika, katika viwanja vyote veya ndege, Mtwara hakuna. Mtwara kiwanja kile ni kikubwa kinahitaji kuboreshwa, hebu angalieni orodha ya viwanja vilivyoko humu, hivi kuna wengine wanawezwa kulinganishwa na Mtwara lakini aah, Mtwara haimo na huko ndiko mnasema ni kwenye Baragumu la gesi. Kwa kweli sasa hivi kile kiwanja kinahitaji kuboreshwa ili kitue ndege kubwa lakini humu haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiasikia vilevile Waziri Mbarawa, anazunguka huku na huko, amesema jambo moja ambalo mimi nimelifurahia, kwamba huu Mkongo wa Taifa sasa watafikisha kwenye kila shule ya sekondari lakini humu kwenye Mpango haimo sijui tutafanyaje na hilo jambo ndiyo chimbuko la mambo yote haya ya *It* tunayoyataka, yafike kwanza shuleni, wanafunzi wajifunze wautumie huo mkongo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hiyo ni kengele ya pilii!

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Shekifu atamalizia na Mheshimiwa Amina Amour.

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nikushukuru wewe lakini pia nianze kwa kutoa pole sana kwa familia ya Mkuu wa Mkoo wa Tanga, Mama Galawa kwa kufiwa na baba yake na Mzee Galawa ni mzee mashuhuri ambaye amelitumikia Taifa hili. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, amina!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwanza kwa kusema kwamba naisifu Serikali kwa ahadi yake ya mwanzo kabisa kwamba sasa tunaanza utaratibu wa kuweka

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. DKT. H. D. SHEKIFU]

mipango na kujadili mipango mapema ili iingizwe katika bajeti. Mimi nakubaliana na utaratibu huu na unaanza kuonyesha matunda mema. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajiepusha kabisa kulaumu kwa sababu hata mtoto anapozaliwa, siku zote umpe matumaini, ukifika mahali kumkatisha tama, atashindwa hata kukaa. Mimi naamini Serikali ni sikivu, itasikia na itatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa suala la utawala bora. Utawala bora, kiungo chake muhimu ni utii wa sheria. Ukiona tunayumba sana na tunapata matatizo ni kwa sababu watu hawataki kuzingatia sheria, matokeo yake ndiyo vurugu. Sasa nawaomba Watanzania wote tusikie maneno bali tumwombe Mungu atusaidie na tuheshimu mamlaka zilizopo juu yetu kwa sababu mamlaka zote zatoka kwa Mungu, tutakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije katika uchangiaji, mimi nakubaliana na maeneo ya vipaumbele, ugharamiaji wa mipango lakini pengine nishauri tu. Kwanza, katika vipaumbele muhimu, mimi nilipoona katika kitabu hiki cha mpango wenyewe, ukurasa wa 49 tumeanza na miundombinu. Nimefarijika sana kwa sababu kwa kipindi kirefu miundombinu hasa miwili reli na bandari, tuseme ule ukweli havikupewa kipaumbele cha kwanza. Tumefanikiwa katika barabara lakini tukifanya vizuri katika reli na bandari, katika lugha ya kiuchumi ya *ki-marketing* na kwa watu waliosoma mambo ya *marketing*, kwa kweli bandari na reli ni *cash cow*, ni fedha zimelala. Tukiweza leo kufufua reli ya kati, kufufua reli ya Tanga, tukajenga bandari ya Tanga na tukatengeneza reli kwenda Musoma, majirani zetu tunaowaogopa hawawezi kushindana na sisi kwa sababu *geographical position* yetu ni nzuri sana. Umbali wa kutoka Tanga kwenda Musoma ili uunganishe na Uganda ni nusu ya safari ya kutoka Mombasa kwenda Uganda. Kwa hiyo, ukishajenga reli na ukaongeza bandari ya Tanga, umekwisha jibu tatizo lote. Ukienda Mtwara, tunazungumzia leo Mtwara panaanza kuonekana, ni chimbuko la maendeleo kwa nchi hii. Sijaona jambo la msingi lilitotajwa katika bandari na reli

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. H. D. SHEKIFU]

ile ya kwenda Mchuchuma na ni vitu muhimu sana. Kwa hiyo, nashauri sana Serikali iangalie katika mipango yake tunakwenda kwenye bajeti tuone fedha za kutosha za kutufikisha katika kuamini kwamba Serikali imeliona hili. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la umeme, mimi nafikiri yale tuliyoyazungumza yatekelezwe. Tukianza kuonyesha mfano tukatekeleza mimi naamini wananchi watakuwa na imani nasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia imezungumziwa, maeneo mengine yana matatizo, tunahitaji kuwekeza na ninaamini ahadi ya Serikali kwamba 2015 kila kijiji kitawezwa kuwa na mawasiliano itatekelezwa, tuone katika bajeti ijayo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji safi na maji taka, tumetenga fedha zionekane kweli maji yafike kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija katika kilimo na mifugo, ni ukweli kwamba kilimo ndio uti wa mgongo, tunahitaji kuwekeza lakini pia lazima tukubali kwamba katika kuwekeza katika kilimo ni lazima tujenge uwezo wa masoko. Sijaona mpango halisi wa kuonyesha tunachozalisha kitauzikaje, maana ukishaweza kuwajengea wananchi soko, umekwishawaandaa kufanya kazi. Tumejifunza mwaka huu, hifadhi ya Taifa wamenunua mazao kanda ya Kaskazini na wamenunua katika muda mfupi tani 32,000 wananchi wametulia na nina uhakika mwaka huu wataendelea kulima. Kwa hiyo, tujenge masoko tuhakikishe kwamba tutafanikiwa. Tulikwishasema kwa mfano, soko la matunda Korogwe, ile kanda ya Kaskazini yote tukiweza kulianzisha lile soko likawa zuri, tukafanya *packaging* ili kuondoa pale kupeleka *KIA* kwa ajili ya kupakiza kupeleka nje ni eneo ambalo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho katika suala la rasilimali watu, Serikali ijitahidi, tuondoe mawazo haya, kwa kweli wananchi tumefika mahali hasa watendaji, *business as usual* tuiache, tubadilike. Mataifa jirani zetu wanachukua

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. DKT. H. D. SHEKIFU]

nafasi katika kuangalia *opportunities* na kufanya maamuzi ya haraka. Tujifunze kufanya maamuzi haraka, tujifunze kuangalia *advantage* zilizoko mbele yetu tuamue, tuisite kuamua. Naiomba sana Serikali, hiyo ndiyo dawa tu katika mashindano, ukichelewa mpira mwenzako ataaingiza goli. Sasa huu ni ugonjwa ambao unatukabili kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika (b) kwa kuchangia haraka haraka, ugharamiaji wa mipango ya maendeleo. Vyanzo vya mapato ya ndani viangaliwe. Sasa hivi iko tetesi kwamba hata makusanyo ya fedha za Serikali za kodi kuna wizi. Fedha zinaonekana zimekwenda benki wanakwenda kupeleka wenyeewe lakini asilimia kubwa nasikia haifiki mikononi mwa Serikali. Sasa mambo kama haya yakisikika yachunguzwe haraka. Hizi *leakages*, huu uvujaji wa mapato, ndiyo tatizo kumbwa sana. Sasa Serikali isimamie ili kile kinachokusanywa kweli kiende katika matumizi ya Serikali. Pia matumizi ya Serikali yaende kwa mipango iliyopangwa, nafikiri tukienda hivyo nchi hii tutaikomboa na mpango huu utakuwa na maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya nje, ni ukweli tusiwe tegemezi. Mimi sikogopi sana madeni lakini madeni yaratibiwe na mtu ye yeyote duniani ambaye atasema hakopi, Marekani leo mpaka juzi imeonywa na Benki ya Dunia kwamba mbona mnakopa sana, mbona mtahatarisha uchumi wa nchi? Maendeleo yote unaona Marekani leo ni kutokana na kukopa. Sasa leo kuwa na wasiwasi tusikope, ni kuyaratibu na tuone kwamba madeni haya yanatumika kwa mambo ya msingi. Kwa mfano, leo tukizungumza reli, ningekuwa mimi nasema reli ya katika ingekuwa *electrified*, miaka mitano, kumi iliyopita maana nina uhakika kila baada ya saa moja itatoka treni Dar es Salaam kuelekea Rwanda, kuelekea Kongo hayo mapato yatakayopatikana yatalipa madeni yote haya tunayozumngumza. Tumejenga misingi gani ya kuzalisha ili tuweze kulipa madeni, hili ndio jambo la msingi na tukilizungumza tusiogope kusema na kuikosoa Serikali kama haifanyi vizuri. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. H. D. SHEKIFU]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Hebu tuwe waaminifu katika kauli zetu na matendo yetu, tutaweza kujenga uaminifu kwa wawekezaji wanaotoka nje, tusibadilikebadilike. Tuangalie maeneo mazuri ambayo hayatawanyanya wananchi wetu, tuwekeze humo na wao ndiyo dunia yote inavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho, utekelezaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi hii. Mimi niombe, kwanza nilisema hapa tukitaka tufanikiwe katika kutekeleza lazima tuamue bila uwga, kwa haraka na kwa wakati bila kuchelewa. Pili, ni lazima kufanya maamuzi kwa wakati, tusiogope kufanya maamuzi kwa wakati, tukichelewa wenzetu wanapata *advantage*. Leo hawa majirani zetu wameshaona mbele wanakutana wenyewe tunatathmini nini katika hilo?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Na hii ndiyo kengele la pili.

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Loh! Ahsante sana.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Amina Amour, msemaji wetu wa mwisho jioni hii.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati ya Bajeti, natangulia kwa kusema naunga mkono kwa asilimia mia moja maoni yote yaliyotolewa na Kamati ya bajeti.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitagusia humuhumu kwenye hiki kitabu chetu nitaanza kukiboresha. Mapato yanayokusanya ni kidogo mno, hii taarifa ipo humu na imesema Serikali itaibua vyanzo vipyta vya mapato. Mimi ninavyofahamu, tayari Kamati ya Spika imeshafanya kazi hiyo, imeshaibua vyanzo vingi vya mapato na imekwenda mbali

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. A. A. AMOUR]

zaidi kwenye sekta ya uvuvi na kusema *license* tutapata kiasi gani na *deep sea* tukienda kuvua tutapata kiasi gani. Sasa nauliza Serikali, mapendekezo hayo yako wapi, mnataka kuibua mengine, hayo mtayatoa Mbinguni? Ikiwa haya mliyoambiwa mmeshindwa kuyafanya kazi mengine mtayapata wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili linakuja kwenye deni la Taifa. Deni la Taifa limeongezeka kutoka dola milioni 12 hadi kufikia dola milioni 16. Hizi fedha hazijaenda kwenye maendeleo kwa sababu maendeleo hayajafanyika, hizi fedha hatujui zimekwenda wapi tumepewa taarifa tu. Ikiwa tunaendelea na huu mtindo wa kukopa fedha tunalipa riba nafikiri hatutafika huko tunakokwenda. Sasa naiomba Serikali itueleze hili ongezeko la hili deni la Taifa, hizi fedha zimetumika kwa kitu gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nitazungumzia misamaha ya kodi. Misamaha ya kodi imepanda kutoka asilimia nne hadi kufikia asilimia sita. Siku zote tunapiga kelele hapa tupunguze misamaha ya kodi ifikie asilimia moja ya pato la Taifa lakini leo imepanda kutoka asilimia nne hadi asilimia sita. Sababu waliyoisema ni kuwa kuna biashara ya gesi na madini. Ongezeko hili ni kubwa sana, kwa hiyo, naiomba Serikali ituletee mikataba hapa kwenye Bunge tuiione kweli hii ilikuwa ni biashara gesi na madini au vinginevyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nitagusia kwenye ajira za vijana, kila siku tunazungumza kuwa vijana tutawawezesha, tutawapa ajira lakini haya ni maneno tu. Mpaka sasa hivi wako vijana wanaranda mitaani, hawana kazi yoyote, hajulikane aliyesoma, hajulikane asiyesoma lakini wako wanaranda mitaani. Tuwe *serious* sana katika hii bajeti inayokuja, tuweke kipaumbele, katika vipaumbele tunavyoviweka na ajira ya vijana iwe kipaumbele namba mbili au tatu. Tunalipoteza Taifa la kesho kwa kuacha hawa vijana kufanya mambo yaliyokuwa hayana maana. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali hili lifanyike.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. A. AMOUR]

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kidogo habari ya *Big Result Now*. Kweli tumeanza huu mfumo wa *BRN* lakini kuna changamoto zimetukabili. Changamoto ya kwanza, hii robo ya kwanza fedha huwa zinakawia kutoka na kwa kukawia kutoka inatokana na mfumo tuliokuwa nao wa *cash budget*, tunaanza na bajeti *with zero* kwa hiyo mpaka tukusanye halafu ndiyo tutoe fedha. Kwa hiyo, naiomba Serikali tutafakari, tukae, tuje na mfumo wanaotumia wenzenetu wa *capital budget* na tukija na mfumo huo haya yote yatawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, nitazungumzia habari ya mikopo. Bado walengwa wa mikopo hawapati ile mikopo yao kwa sababu kwanza riba ni kubwa mno halafu masharti ni magumu mno. Hii mikopo inaitwa mikopo nafuu kwa maana ninayoona mikopo nafuu, wapate wale watu wenye kipato chini lakini riba ni kubwa. Kila siku tunapiga kelele kwa nini Serikali hawaii wafanyabiashara wakawaambia hizi riba wapunguze au masharti magumu wayapunguze. Mtu unamwambia alete hati ya nyumba mtu kibanda hana atakuwa na hati ya nyumba? Ni bora sasa hivi tuwasidie kweli kama kweli tunataka hawa vijana wapate mikopo au hawa watu wasiojiweza wapate mikopo, tuweze kuwasaidia kwa kutumia njia nyingine ya kuwapatia hii mikopo na kuongea na mabenki ili hizi riba zipungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nimemaliza. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona wachangiaji wa leo wanatosha, tutaendelea na kesho kwa hiyo Bunge linarejea.

(*Bunge lilirudia*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyo sema, kesho tutaendelea na ningependa Serikali ama Waziri anayehusika na Serikali, tunapojadili Mpango huu siyo

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[SPIKA]

Mpango wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango, ni wa Serikali yote. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba kesho mnakuja wote kadiri mnavyostahili. Kila mtu ana-*chapter* yake. Kwa hiyo, msije mkaona hapa ni Mheshimiwa Wassira tu ndiyo anatakiwa kujibu, hapana, kwa sababu kutakuwepo na mambo ambayo ye ye kama ye ye hana majibu ninyi ndiyo wenye majibu, kwa hiyo nategemea hivyo. (*Makofi*)

Halafu siku ya kumaliza, ndipo sisi tutakaa kama Bunge na maamuzi yetu yatakuwa maamuzi ya Bunge, hivi sasa tunashauri. Kwa hiyo na Kamati yetu ya Bajeti iendelee kuwasiliana na Serikali kuona maeneo ambayo yanazungumzwa ni vipi tunaweza kuyaweka vizuri zaidi kusudi atakapokuja ku-*sumup* Waziri ata-*sumup* kama Bunge. Kwa hiyo, haya yatakuwa ni maamuzi halali ya Serikali. Kwa hiyo, mnapoendelea kusikiliza, mjue hayo ndiyo yanayoendelea na ninaomba Serikali msidhani kama ni kazi ya Waziri wa Mipango tu, hapana, ni ninyi wote katika maeneo yenu. Kwa hiyo, naona uwepo wenu si mzuri hivyo. Kesho tutatoa maelezo kama hamtatokea kadiri inavyostahili. (*Makofi*)

Kesho asubuhi Waziri Mkuu hatakuwepo, kwa hiyo, kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu hakipo. Kwa hiyo, msije mkaamka asubuhi, kesho hajarudi safari, kwa hiyo, hatuna kipindi kile cha maswali.

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine naomba nahirishe shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.32 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 31 Oktoba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*